# UCHANGANUZI WA WAHUSIKA KWA MISINGI YA KIBABE DUME KATIKA RIWAYA TEULE ZA BEN MTOBWA

WANJOHI SIMON NGURE

Tasnifu iliyowasilishwa kwa Chuo cha Mafuzu ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili na Mawasiliano ya Chuo Kikuu Cha Laikipia.

**OKTOBA 2025**

## UNGAMO NA IDHINI

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili na Mawasiliano katika chuo kingine chochote.

Sahihi: ______________________ Tarehe: ______________________

**WANJOHI SIMON NGURE**

**MK22/2520/18**

**IDHINI**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi ili kutimiza mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili na Mawasiliano ya Chuo Kikuu cha Laikipia.

Sahihi: ______________________ Tarehe: ______________________

**Prof. James Onyango Ogola**

**Idara ya Usomilugha na Mawasiliano**

Sahihi: ______________________ Tarehe: ______________________

**Prof. Wendo Nabea**

**Idara ya Usomilugha na Mawasiliano**

# HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili au kutoa sehemu ya tasnifu hii au nakala nzima kwa njia yoyote ile bila idhini mahususi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Laikipia.

*Wanjohi S.N.@2025*

## TABARUKU

Kazi hii iwafikie Beth Wambui, Moses Wanjohi, Joy Wairimu, Grace Mukami na Paul Muraguri. Nawashukuru sana kwa michango yenu katika kufanikisha utafiti huu. Mwenyezi Mungu awape neema za milele.

# SHUKRANI

Shukrani zangu kwanza zimfikie Mola kwa majaliwa katika maisha yangu kufikia sasa. Neema yake imekuwa nguzo imara katika maisha yangu. Pia Maulana amenipa siha na uhai. Pili sitawasahau wale ambao wamekuwa kwenye mstari wa mbele kunihimiza kuchapa kazi. Ari yao kwangu imekuwa ya kunipa motisha kuhitimisha kazi yangu. Nao ni wazazi wangu Moses Wanjohi Nduriri, Jane Waturi Wanjohi, ndugu zangu kama vile Patrick Maina, Peter Murwaigi, Jael Njoki na marehemu Eshiban Nduriri. Kwa njia ya kipekee nitamhongera babangu mzazi aliyenifanya kulipenda somo la Kiswahili kwa kuninunulia nakala ya *Taifa leo* kila alipoenda Nyeri mjini. Mungu akuzidishie miaka. Mawaidha ya aila yangu yamenijengea mazingira mema ya kufanyia mradi kazi. Nawapongeza wasomi wenzangu kwa ushirikiano wao katika kutimiza malengo yangu ya kiusomi. Nao ni kama vile, Lucy Mugo, Kerryann Mburu, Nicholas Kirui, Mburu Kamau na Slyviah Ngure. Juhudi zenu za kupiga vita ubwete zilikuwa za manufaa kwetu. Maulana aendelee kuwapa moyo uo huo na pia neema za milele.

Wasimamizi wangu nawapa kongole. Prof. James Onyango Ogola ameniongoza katika panda shuka za kazi yangu hadi hitimisho lake. Moyo wake umekuwa wa thamani kwangu. Ufadhili wake umevuka mipaka ya kiusomi hadi kuwa kiongozi shupavu wa kutegemewa. Mola azidi kumtendea mema na amruzuku mara dufu kwani amekuwa mwenza na mtegemewa katika safari hii. Prof. Wendo Nabea namtambua kwa mchango wake wa kupigiwa mfano. Yeye alikuwa imara na mtenda kazi aliyenifaa sana. Mawazo yake kufikia hatima hii yamenijengea msingi thabiti wa utafiti huu. Jalali amjalie mema.

Nawapongeza wakuu wa idara wa sasa na wa zamani kwa kuhakikisha mradi wangu unapiga hatua kila uchao. Kwa njia ya kipekee nampongeza Prof. Sheila Wandera kwa kujitolea mhanga tulipoanza masomo yetu tukiwa wakembe chuoni kiusomi. Amekuwa wa msaada sana na Rabuka akupe neema za kudumu. Pia nawapongeza wahadhiri wengine katika idara kama vile Prof. Eliud Kirigia, Prof. Rutere, Prof. J. Ndambuki, Prof. Vicky Khasandi, Dkt. Nderitu na Dkt. Florence Mwithi. Sitawasahau marehemu Prof. Aswani Buliba na Dkt. Mayaka waliokuwa magwiji wa lugha.

Nafikia hatima kwa kutoa shukrani kwa Idara ya lugha na Mawasiliano ya Chuo Kikuu cha Laikipia. Imenijengea msingi wangu wa taaluma ya usomi kuwa imara. Bila kumsahau mhadhiri wa zamani wa Chuo Kikuu cha Moi marehemu Dkt. Noordin Mohammed aliyenigusa kiusomi hasa katika uhakiki wa riwaya.

# IKISIRI

Suala la jinsia limekuwa mojawapo ya masuala yaliyopewa kipaumbele na yanayotafitiwa katika taaluma mbalimbali zinazohusu maisha ya mwanadamu. Wasomi kuhusiana na masuala ya kijinsia wamekuwa wakiegemea mkabala wa kifeministi. Mkabala huu haujaweza kuangazia vile jinsia ya kiume hukandamiza jinsia iyo hiyo kwa sababu ya udhaifu kiuwezo, kimwili au kimawazo. Hivyo basi, wahusika wa kiume kufanyiana ubabedume hasa katika kazi za fasihi ni suala ambalo halijapambanuliwa kama inavyojitokeza katika jamii ya sasa. Tasnifu hii ilichanganua wahusika kwa misingi ya kibabedume katika riwaya teule za Ben Mtobwa, *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka*. Madhumuni ya utafiti yalikuwa kusawiri sura mbalimbali za ubabedume zinazojitokeza katika jamii za riwaya hizo. Pia mtafiti alitathmini vile ubabedume unaathiri jinsia katika riwaya mbili za Ben Mtobwa, *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka*. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ya ubabedume. Nadharia hii hudhirisha jinsi ubabedume hujengwa na jinsi wanaume huelekezwa kutimiza majukumu yao kupitia nguvu, utawala na udhibiti wa hisia. Mwasisi wa nadharia hii ni Raewyn Connell wa nchi ya Australia. Mihimili ya nadharia hii iliyoongoza utafiti huu ni pamoja na itikadi za jamii, uwezo, utamaduni, mgawanyo wa majukumu kiuana na sifa angama za uwezo kiume. Fauka ya hayo, ilisaidia katika uchanganuzi wa data kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Muundo wa utafiti ulikuwa wa kimaelezo na kimsingi, utafiti ulifanyika maktabani. Pia makala na majarida yaliyohusiana na suala la ubabedume katika kazi za fasihi yalipitiwa. Data ya a utafiti ilitokana na riwaya mbili husika ambapo masuala ya ubabedume yalidondolewa mintarafu ya madhumuni ya utafiti. Matokeo ya utafiti yadhihirisha sura mbalimbali za ubabedume kama vile za kitamaduni, kiuume, kiuchumi, kisaikolojia, kimaumbile na kisiasa. Licha ya hayo, matokeo ya utafiti yalibaini athari za ubabedume katika misingi ya jinsia kupitia ukahaba, dhuluma za kijinsia, utabaka wa kijinsia, utapeli, usaliti na utepetevu. Utafiti huu unatarajiwa kuwanufaisha wasomi wa fasihi, hususan wale wamebobea katika fani ya jinsia. Aidha, unatarajiwa kuongeza data iliyopo kuhusu masomo ya ubabedume hasa katika mataifa ya Afrika.

**ABSTRACT**

Gender studies is one of the disciplines that has received a lot of scholarly attention in various fields of human life. A section of scholars on gender studies have anchored their studies on feminism, whereby the domination of women by men in partriarchal societies has been spotlighted. However, such studies have failed to illuminate the social hierarchies where men dominate each other. By extension, the social male dominance hierarchy where men exercise control over fellow men is a matter that has received inadequate attention in Kiswahili literary works. The dominance is exerted as a result of physical, psychological and authoratorial weakness. This research analysed characters using a masculinity studies approach in selected Ben Mtobwa's novels thus, *Dar-es-Salaam Usiku* and *Pesa Zako Zinanuka*. The research objectives were to explore the forms of masculinities in the two novels, and to evaluate the effects of masculinities on the social fabric. The research, which was largely conducted in the library, used a qualitative research design to study the characters and themes in the novels. It was hinged on masculinity theory as espoused by Raewyn Connell. The theory shows how male gender is constructed leading to male domination in various spheres. Its tenets include power hierarchy, strength, aggression and emotional forbearance. The pillars of the theory guided in data collection and analysis in line with the objectives of the study. The results revealed that the novels treat a variety of masculinities based on tradition, nuances of the male phallus, economy, psychology, nature and politics. The results also showed the effects of masculinities on the social prism as prostitution, gender violence, gender hierarchies, fraud and indolence. The study stands to benefit an array of scholars especially those inclined to gender studies in Kiswahili. It will also add to the extant data on masculinites especially in Africa.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI .......... ii**

**HAKIMILIKI .......... iii**

**TABARUKU .......... iv**

**SHUKRANI .......... v**

**IKISIRI .......... vi**

**ABSTRACT .......... vii**

**MAELEZO YA ISTILAHI .......... x**

**SURA YA KWANZA .......... 1**

**UTANGULIZI .......... 1**

1.1 Usuli wa Mada .......... 1

1.2 Suala la Utafiti .......... 5

1.3 Madhumuni ya Utafiti .......... 5

1.4 Maswali ya Utafiti .......... 5

1.5 Umuhimu wa utafiti .......... 5

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 7

**SURA YA PILI .......... 8**

**MAPITIO YA MAANDISHI .......... 8**

2.1 Utangulizi .......... 8

2.1.1 Mapitio ya Maandishi kuhusu Sura za Ubabedume .......... 8

2.1.2 Athari ya Ubabedume kwa Jinsia .......... 16

2.2 Misingi ya Nadharia .......... 19

2.2.1 Nadharia ya Ubabedume .......... 20

SURA YA TATU .......... 24

MBINU ZA UTAFITI .......... 24

3.1 Utangulizi .......... 24

3.2 Muundo wa Utafiti .......... 24

3.3 Mahali pa Utafiti .......... 24

3.4 Kikundi Lengwa .......... 25

3.5 Uteuzi wa Sampuli .......... 25

3.6 Ukusanyaji wa Data .......... 25

3.7 Uchanganuzi wa Data .......... 26

3.8 Uzingativu wa Maadili .......... 26

**SURA YA NNE** .................................................................................... **27**
**UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA** .................................................... **27**
4.1 Utangulizi .................................................................................... 27
4.2 Sura mbalimbali za Ubabedume .................................................................. 27
4.2.1 Sura ya Kitamaduni .......................................................................... 28
4.2.2 Sura ya dhakari .............................................................................. 33
4.2.3 Sura ya Kiuchumi ............................................................................ 36
4.2.4 Sura ya kisaikolojia ......................................................................... 40
4.2.5 Sura ya Kimaumbile .......................................................................... 50
4.2.6 Sura ya Kisiasa .............................................................................. 53
4.3 Athari za Ubabedume kwa Jinsia ................................................................ 55
4.3.1 Ukahaba ...................................................................................... 55
4.3.2 Dhuluma za Kijinsia ......................................................................... 60
4.3.3 Utabaka wa Kijinsia ......................................................................... 65
4.3.4 Utepetevu .................................................................................... 67
4.3.5 Utapeli ...................................................................................... 69
4.3.6 Usaliti ...................................................................................... 70
4.3.7 Anasa ........................................................................................ 71
4.3.8 Unafiki ...................................................................................... 73
4.4 Hitimisho ..................................................................................... 74
**SURA YA TANO** .................................................................................. **74**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ...................................................................... **74**
5.1 Utangulizi .................................................................................... 74
5.2 Muhtasari wa Tasnifu .......................................................................... 75
5.3 Matokeo ya Utafiti ............................................................................ 76
5.4 Hitimisho ..................................................................................... 78
5.5 Mapendekezo ................................................................................... 79
**MAREJELEO** ..................................................................................... **80**
**VIAMBATISHO** ................................................................................... **85**
Kiambatisho I: Barua ya Chuo .................................................................... 85
Kiambatisho II: Barua ya Idhini Kutoka NACOSTI .................................................. 86

## MAELEZO YA ISTILAHI

**Itikadi**: Ni mwelekeo wa kimawazo unaodhibiti jinsi kikundi cha jamii fulani kinavyoukabili, kuufasiri na kuulewa ulimwengu wao. Kwa hivyo, ni mawazo pendwa yanayopendelea jinsia ya kiume.

**Jinsia**: Ni tofauti za kimaumbile zinazobainisha binadamu kuwa mwanamume au Mwanamke. Ni mahusiano ya kijamii na kiutamaduni yanayozingatia mgawanyo wa majukumu kwa kuangalia uume na uuke.

**Taathira:** Ni alama au hisia inayobaki kwa muda kutokana na kutokea kwa jambo fulani. Katika tasnifu hii neno hili limetumiwa kuonyesha hali yenye matokeo hasi hasa yanayoumiza anayefikiwa na jambo fulani.

**Uana**: Ni utaratibu wa kijamii unaoimarisha tofauti za matarajio na majukumu kati ya wanaume na wanawake katika jamii.

**Ubabedume:** Ni mfumo wa kijamii ambao humtukuza au kumtweza mwanamume au kumdhalilisha mwanamke. Ni hali za kihistoria ambazo hubainisha jinsi nguvu na uwezo hupatikana na kudhihirishwa katika jamii. Huonyesha mikakati ambayo wanaume hupitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine ambayo huwaweka mbele na kudhibiti uwezo wa jinsia ya kike au jinsia ya kiume isiyo na uwezo.

**Usawa wa kijinsia:** Ni hali ya kutokuwa na ubaguzi kwa misingi ya jinsia ya mtu katika nyanja mbalimbali zikiwemo mgao wa rasilimali au kupata huduma katika jamii.

**Utamaduni**: Ni mfumo wa maisha ya watu jinsi wanavyoishi na maendeleo yao ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hivyo basi, ni mila au desturi zinazodhibiti wanajamii.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Suala la jinsia huhusisha wanaume na wanawake. Harakati za kuweza kuelewa jinsia zimeleta wazo la mgawanyo wa kimajukumu. Hali hii imeibua kategoria mbili za jinsia. Jinsia imeonekana na wasomi wengi wa kisasa kama suala linalojengwa na jamii. Hoja hiyo ya jinsia ni kitambulisho ambacho kimepata umaarufu sana. Kulingana na wasomi wa masuala ya kijinsia, mawazo hayo siyo kitu tunachozaliwa nacho lakini huanza kabla ya kuzaliwa kwa mtoto. Kulingana na Connell (1995), sifa za wanaume na wanawake hazikutofautishwa kulingana na wahusika katika tamaduni za Ulaya kabla ya karne ya 18. Wanawake walisawiriwa kama wahusika wasio wakamilifu wakilinganishwa na wanaume. Kitambulisho cha kiume kilichukuliwa kama kitambulisho cha mwanadamu kwa ujumla. Anaendelea kusema kuwa wasomi kadhaa wa kimagharibi wanashikilia hoja hii hata katika ulimwengu wa kisasa. Dhana ya ubabedume iliyozinduliwa miongo miwili iliyopita imeathiri mawazo mapya kuhusu wanaume, jinsia na uwezo wa kijamii. Hali hii imeleta kiungo muhimu katika nyanja za tafiti za usomi wa wanaume.

Kulingana na Wilson (2000), ubabe dume ni mfumo ambao mwanamume huwa ndiye mwenye uamuzi, sauti ya mwisho na pia ndiye mtawala mkuu. Ni mfumo wa kijamii na mazoea yake ambapo mwanamume humtawala, humkandamiza na kumtumia mwanamke kwa manufaa yake. Anaongeza kuwa ubabedume hudhihirika kwa kejeli, masikitiko, kuumiza moyo, malumbano na kutahadharisha, taathira za uwoga, visasi, maradhi ya msongo wa mawazo na kuhalalisha maovu. Malenga (2022) akirejelea Oyewumi (1997) anadai kuwa suala la ujinsia limekuzwa na watu wa Magharibi kiasi cha kuifanya dunia nzima, Afrika ikiwemo kuamini kuwa unyanyasaji wa kijinsia unaathiri maisha ya kila siku ya wanawake. Anatoa mfano wa uana katika jamii ya Kiyoruba ambapo hakuna mgawanyo wa majukumu kijinsia. Mgawanyo huu wa majukumu hufanyika kulingana na umri. Kwa upande mwingine Oyeronke (2011) anajaribu kufafanua dhana ya umenke anapohariri makala mbalimbali yanayohusu tajriba za kimenke barani Afrika. Alichunguza makala yaliyoandikwa na wandishi kutoka maeneo ya bara hili. Anaelezea kuwa umenke huundwa na jamii.

Hivyo basi, ikumbukwe kuwa dhana ya ubabedume ilizalishwa na usomi wa masuala ya kijinsia. Ubabedume ni hali ambapo jinsia ya kiume hujaribu kushinda na kuhifadhi mamlaka dhidi ya jinsia ya kike. Dhana hii pia husaidia katika kuleta ufahamu wa vile ubabedume huzalisha uwezo kingazi miongoni mwa wanaume kwa wanawake na pia wanaume kwa wanaume. Kimsingi, jinsia ya kike hujitokeza kama vyombo vya mapenzi kwa wanaume. Hali hii hudhalilisha jinsia ya kike. Ubabedume ni seti changamano ya fikra, mitazamo, tabia na uwezo unaomilikiwa na kundi mahususi la wanajamii.

Seti hii ndiyo huratibu mfumo wa utawala na mamlaka katika jamii, hali ambayo huwaweka wanajamii katika makundi tofauti kwa mujibu wa uwezo kandamizi wa jinsia yao. Ubabedume huwa ni kifaa cha kusawiri mtazamo na hulka ambazo jinsia ya kiume hutumia kuleta kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia. Ubabedume hujitokeza mwanzoni mwa ulezi. Msimamo na mtazamo kuhusu ubabedume ni kuwa wavulana na wanaume hawajengi nafasi zao katika ombwe tupu. Hivyo basi, kuna ukubalifu katika utamaduni wa jamii ambao husisitiza ukakamavu na ushujaa katika utendaji wa majukumu yao katika jamii.

Kulingana na ripoti ya Shirika la Wanawake Ulimwenguni (2015), suala la ubabedume katika jamii mbalimbali za ulimwengu limeibua changamoto katika mijadala na makongamano mbalimbali. Tangu miaka ya tisini, kulikuwa na makongamano ya kimataifa ya kujadili suala la usawa wa kijinsia. Kwa mfano, athari ya utandawazi katika ruwaza za kijinsia na fasili ya uanaume na ujinsia wa kiume. Usawiri wa mwanamume katika jamii za Kiafrika ni suala ambalo limeibua sintofahamu katika makongamano mbalimbali kwa misingi ya uhalisia wa kuwepo uwezo-uume. Kwa kipindi kirefu jinsia ya kike imetwezwa na kudunishwa kutokana na dhuluma wanazofanyiwa na jamii iliyotawaliwa na ubabedume. Hali hii imekandamiza jinsia ya kike katika maswala ya kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kiuongozi. Katika bara la Afrika kama ilivyo katika dunia yote, mfumo dume uliotawaliwa na tamaduni umeipa jinsia ya kiume kipaumbele. Hivyo basi, ni mataifa machache yaliyofikia suala la usawa wa kijinsia. Hali hii imefanya wanawake kuwa hohehahe. Katika taifa la Kenya suala la usawa wa kijinsia halijafikiwa. Miswada kuhusu usawa wa kijinsia imewasilishwa bungeni bila kufaulu. Mataifa mengi kama Rwanda yameng’ang’ana na kufikia malengo ya usawa wa kijinsia.

Hata hivyo, mataifa mengi hayajafaulu kutimiza lengo hili. Katika taifa la Kenya, suala la usawa wa kijinsia limenakiliwa katika katiba mpya ya 2010. Zaharia (2018) akimrejelea Edell (2015), anaeleza kuwa katika jamii yenye makuzi ya ubabedume, mwanamume huwa na nguvu akilinganishwa na mwanamke katika madaraja ya kijinsia. Mwanamume huwa ni mtumwa wa ujana dume wake kutokana na kuziingiza akilini tafsiri za kiutamaduni za ujana dume. Baadhi ya tafsiri za ujana dume humfanya mwanamume kujenga ukuta usioonekana wa ubabedume ndani ya nafsi zao. Huwa mwanamume haruhusiwi kuonyesha udhaifu wake kwa jamii. Naye Wandera (2015) anadai kuwa suala la umenke limetia fora katika nyanja zote fasihi ikiwemo.

Hali hiyo inamjenga mwanamume kujiona ana uwezo mkubwa na huwa hataki mambo ya kumshusha ngazi. Hivyo kutokana na hali hii, mwanamume huwa anakwezwa na huwa na sauti kuu katika maamuzi ya kijamii. Hata hivyo, hali hii imemsukuma mwanamume kujisahau na kufikia hatua ya kufanyiana ubabe wenyewe kwa wenyewe. Hali hii imejengeka katika jamii ambapo mwanamume huweza kutoa kauli za kashfa dhidi ya mwanamume mwenziwe ili aoneshe udume wake. Jamii humpa nguvu mwanamume hata kama anaumia kwani si rahisi kujikubali kuwa anaumia kutokana na utamaduni wa jamii ulivyomkuza. Naye mwanamke katika jamii ya ki-ubabedume amechukuliwa kama kiumbe dhaifu na amepewa nafasi finyu. Morettini (2016) anapendekeza kuwe na mjadala wa umma kuhusu hulka zinazohusiana na uwezo ambazo huleta mgawanyiko katika jinsia ile ile moja ya kiume.

Katika jamii nyingi ambazo huongozwa na mfumo wa uume, elimu ya mtoto wa kiume hupewa kipao mbele ikilinganishwa na elimu ya jinsia ya kike. Katika taifa la Kenya ambapo kuna tofauti kubwa kati ya wanaume na wanawake, uharibifu wa mazingira huathiri zaidi wanawake kuliko wanaume. Usomi wa ubabedume ni mchanga zaidi au uko katika kiwango cha uchanga zaidi ikilinganishwa na usomi wa ufeministi ambao umeangaziwa kwa mapana na marefu. Ubabedume huhusishwa na uwezo wa jinsia ya kiume dhidi ya jinsia ya kike na ambao umekuwako kama ishara ya imani za kijamii. Kulingana na Anderson na Accomando (2002) ubabe dume huhusishwa na jamii inayotawaliwa na mfumo wa kiume mathalani jinsia ya kiume hupewa nafasi kuu katika mfumo wa jamii. Tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiafrika husawiri ubabedume kwa njia tofauti na fasihi ya Kimagharibi. Tafiti nyingi zimefanywa katika jamii anuwai kwa kuzingatia tanzu mbalimbalii za kifasihi hasa kuangaza sifa za kike na zile za kiume.

Matokeo ni kuwa sifa za kike hutwezwa ilhali zile za kiume huangazwa kwa mtazamo chanya.

Tanzu mbalimbali za fasihi humsawiri mwanamke na mwanamume kwa njia tofauti. Mwanamume hutukuzwa huku mwanamke akitwezwa. Wasomi na wahakiki wa kazi za fasihi wameshughulikia suala la jinsia. Kazi tofauti za kifasihi zimesawiri mahusiano ya kijinsia. Fauka ya hayo, suala la kuwepo kwa itikadi ambazo zinaongozwa na ubabedume zimeangaziwa. Mboya na wenzake (2018) katika utafiti wao kuhusu dhuluma kama kichocheo cha mzinduko wa wanawake katika riwaya ya Kiswahili, wanadai kuwa mwanamke hasa wa Kiafrika anakabiliwa na dhuluma kutoka kwa jamii inayotawaliwa na ubabedume. Utafiti wao unaonyesha vile jinsia ya kike inakandamizwa lakini inajaribu kujikomboa kutoka kwa madhila haya.

Ubabedume hujitokeza katika kazi za fasihi kwa njia tofauti kwa kutegemea utanzu. Usawiri wa ubabedume katika fasihi simulizi na fasihi andishi ni tofauti. Katika tanzu za fasihi andishi, ubabedume huonyeshwa katika vitengo tofauti. Ubabedume hujitokeza miongoni mwa wahusika au hata katika matumizi ya lugha. Kuwepo kwa ubabedume katika kazi za fasihi andishi kama vile riwayani ni suala ambalo linajitokeza. Riwaya ikiwa mojawapo ya tanzu za fasihi andishi imehusishwa na kazi ya kubuni. Riwaya imeundwa kutokana na mchango wa vipengele maalum kama maudhui, mbinu za utunzi na fani ya wahusika. Wahusika hufafanuliwa kama watu, wanyama au vitu katika fasihi. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa wahusika wakuu ndio nguzo za riwaya na wanasheheni riwaya nzima. Huwa na dhima ya kuisukuma riwaya mbele kwa sababu ya migogoro na matendo yote muhimu inayowahusu. Waandishi wa vitabu vya kifasihi wamechukua mtazamo wa jamii iliyotawaliwa na ubabedume. Waandishi wengi wa jinsia ya kiume wamewasawiri wanawake katika uhalisia wa kijamii. Hali hii inakashifiwa sana kwani inarudisha nyuma juhudi za mwanamke kujikomboa.

Kwa upande mwingine, katika kazi zizo hizo za fasihi tunapata kuwa ubabedume huwa unatumiwa kukandamiza watu wa jinsia ile ile ya kiume. Wahusika wanaume hudhalilishana kupitia ubabedume na hivyo kukosa urari na usawa katika jamii. Hali hii hufanya baadhi ya wahusika wa kiume kutwezwa na wanaume wenzao.

Katika utafiti huu tulishughulikia uchanganuzi wa wahusika kwa misingi ya kibabe dume katika riwaya teule za Ben Mtobwa ambazo ni *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako zinanuka*.

### 1.2 Suala la Utafiti

Suala la ubabedume limekuwa likiangaziwa katika kazi za fasihi. Hususan vile ubabedume unajijenga, kujiendeleza na kujishamirisha katika kazi za fasihi. Ubabedume hutumiwa kubagua na kutenga wanawake na hata wanaume kwa misingi ya itikadi na uwezo. Wanaume ambao huwa na jinsia mbili au wasio na sifa angama za kiume hubaguliwa na jamii kama inavyosawiriwa katika kazi mbalimbali za sanaa. Hata hivyo, hali ya wanaume kufanyiana ubabedume ni suala ambalo halijatafitiwa kwa kina kama inavyosawiriwa na ukosefu wa data tendeti kulihusu suala hili. Ni kutokana na pengo hili la kiusomi utafiti huu ulijikita katika kuchunguza wahusika teule kwa misingi ya kibabe dume katika riwaya za Ben Mtobwa, *Dar-es-Salaam Usiku* na Pesa *Zako Zinanuka.*

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

1. Kusawiri sura mbalimbali za ubabedume miongoni mwa wahusika katika riwaya teule za Ben Mtobwa; Dar*-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka.*
2. Kutathmini vile ubabedume unavyoathiri jinsia za kiume na kike katika riwaya za Ben Mtobwa; Dar*-es-Salaam Usiku* na Pesa *Zako Zinanuka.*

### 1.4 Maswali ya Utafiti

1. Je, ni sura zipi za ubabedume zinavyojitokeza miongoni mwa wahusika kulingana na riwaya teule za *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka?*
2. Je, ni vipi ambavyo ubabedume unavyoathiri jinsia za kiume na kike katika riwaya za *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka?*

### 1.5 Umuhimu wa utafiti

Kichocheo cha kushughulikia mada hii teule kimetokana na sababu mbalimbali. Kwanza, suala la ubabedume katika fasihi limekuwa likijitokeza lakini halijakuwa likipambanuliwa kwa undani. Riwaya hizi mbili za Ben Mtobwa zina hazina ambayo haijachunguzwa. Fauka ya hayo, mwandishi wa riwaya hizi ana upekee na ukwasi katika uandishi wa riwaya pendwa. Pia Ben Mtobwa ni mwandishi ambaye huonyesha uhai wa fasihi kwa kugusia masuala nyeti na ibuka yanayoipa jamii changamoto. Hivyo

basi, suala la ubabedume ambalo linajitokeza katika fasihi andishi linafaa lichunguzwe vile linavyojitokeza siyo tu kwa jinsia ya kiume kwa njia chanya pia kwa jinsia iyo hiyo kwa njia hasi. Suala la ubabedume limekuwa likiangaliwa tu kwa mtazamo wa kudhalilisha jinsia ya kike. Hata hivyo, utafiti huu ulinuia kuangalia kuwili katika jinsia zote.

Utafiti huu utachangia pakubwa katika uhakiki wa fasihi. Pia utafiti huu ulichangia katika hazina ya tahakiki katika usomi wa nyanja hii. Hali hii inatarajiwa kuongezea maarifa katika usomi wa ubabedume katika fasihi andishi. Fauka ya hayo, utafiti huu utazindua wasomi wengine kuangazia suala hili kwa mitazamo tofauti. Tahakiki hizi zinatarajiwa kuwa kiunzi kwa wasomi wa siku za usoni. Zaidi ya hayo, wasomi wengine watachochewa kufanya uchunguzi katika kazi zingine za fasihi baada ya kufanya uhakiki wa utafiti huu.

Watafiti, wahakiki na wasomi wengine wa masuala yanayohusu ubabedume katika fasihi watakuwa na msingi mzuri wanapofanya kazi zao. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yananuiwa kuwafaa wataalamu wengine wa fasihi na lugha katika kazi zinazohusu jinsia. Fauka ya hayo, utafiti huu utatumiwa kuhamasisha jamii kwa jumla kuhusu suala la ubabedume kwani uliangazia athari za hali hii kwa jinsia zote mbili. Kazi hii pia itachangia katika uimarishaji wa sera za kijinsia. Hii itasaidia kuimarisha utunzi wa kazi za fasihi kwa kuegemea usawiri wa ubabedume ambao unaweza kuangaziwa na wasomaji kwa njia hasi.

Hali hii itawezesha wanajamii kubuni mbinu za utetezi kwa mwanamume anayeathirika kimya kimya na ubabedume hasa katika kazi za fasihi. Fauka ya hayo, mwamko mpya utajengeka kwa jamii kutokana na madhila na mateso ya ubabedume yanayomfikia mwanamume. Hii itasaidia wanajamii kufahamu na kubaini kuwa ubabedume una taathira kwa mwanamume mwenyewe pia.

Kazi hii pia inatarajiwa kuleta mtazamo tofauti kwa watafiti wa siku za usoni ambao wataionea fahari ya kuangazia kazi zinazohusiana na suala la kijinsia. Pia wandishi wa fasihi wanatarajiwa kuzinduka kutoka kwenye katika mitazamo yao kuhusu usawa na kuandika kazi zinazoheshimu usawa wa kijinsia na kumulika mikakati inayotumiwa na wahusika tofauti kuendeleza ubabedume. Vilevile, utafiti huu unatarajiwa kumulika kutowepo kwa usawa wa kijinsia kwa azma ya kulinda kizazi cha kesho ambacho kinategemea harakati zetu sasa.

Kwa wazazi wa jinsia zote, hazina hii italeta uzinduzi katika mafunzo ya watoto wao wanaotegemewa kwa mabadiliko halisi. Kutokana na haya, kuthaminiwa kwa watoto bila ubaguzi kutasaidia kuweka kizazi cha kesho katika hali ya usawa katika nyanja za maisha. Utafiti huu ulidhamiriwa kusaidia jamii kwani utajaribu kuangazia vichocheo vinavyoendeleza ubabedume na pia kukwezwa kwa jinsia ya kiume ilhali jinsia ya kike ikitwezwa. Hali hii italeta mtazamo mpya tofauti na mitazamo ya kifeministi kwani imekuwa ikipigana na ukandamizaji wa wanawake pekee. Matokeo ya utafiti huu yalilenga kuchangia kuelewa hali halisi ya jamii kwa kuegemea kazi za fasihi kwani fasihi kama kioo cha jamii inatarajiwa kumulika uhalisia wa jamii.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa wa kifasihi na hivyo ulijishughulisha na kuhakiki riwaya mbili za Kiswahili. Kazi hii ilimulika suala la ubabedume linavyojitokeza miongoni mwa wahusika teule katika riwaya ya *Dar-es-Salaam Usiku* na Pesa *Zako Zinanuka.* Isitoshe, ilishughulikia uchanganuzi wa wahusika kwa misingi ya kibabedume katika riwaya teule za Ben Mtobwa. Kuna riwaya nyingi za Kiswahili lakini hizi mbili ndizo zilichunguzwa. Riwaya hizi pendwa zina ukwasi wa kipekee katika kuangazia masuala ya kijinsia hasa ubabedume. Mfumo wa ubabedume huwa na athari hasi na chanya kwa jinsia zote mbili. Hivyo basi, utafiti ulichunguza vile ubabedume unaathiri jinsia ya kike na hata jinsia ya kiume katika riwaya mbili za Ben Mtobwa.

Riwaya hizi zilisomwa na wahusika kuchanganuliwa kwa misingi ya kibabe dume Utafiti huu ulichunguza sura za ubabedume hususan, sura za kitamaduni, kiuchumi, kidhakari, kisaikolojia, kisiasa na kimaumbile. Pia utafiti huu ulipambanua athari za ubabedume kwa jinsia ya kiume na kike kama vile, dhuluma za kijinsia, utabaka wa kijinsia, ukahaba, utepetevu na usaliti. Utafiti ulijikita katika nadharia ya ubabedume ambayo husawiri nguzo za mfumo wa kuumeni.

# SURA YA PILI
# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandishi na msingi wa nadharia. Mtafiti alidurusu tafiti zinazohusiana na mada ya utafiti kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Alionyesha kufanana kwa tafiti hizo na utafiti wake na pia alisawiri tofauti zinazojitokeza. Fauka ya hayo, pengo la kiusomi linalotakikana kujazwa lilizingatiwa. Mapitio ya maandishi yamepangwa kwa kuegemea madhumuni ya utafiti. Aidha, nadharia na mihimili yake ambayo ni msingi wa utafiti huu ilishughulikiwa. Sehemu hii ilihakiki kazi za awali ambazo zinahusiana na utafiti huu kwa kuchanganua ubabedume katika kazi za fasihi.

### 2.1.1 Mapitio ya Maandishi kuhusu Sura za Ubabedume

Uchendu (2007) alifanya utafiti kuhusu ubabedume miongoni mwa vijana katika taifa la Nigeria hasa wale waliokuwa vyuo vikuu kutoka makabila tofauti. Vijana hawa wa jinsia ya kiume na kike walihusisha ubabedume na jinsia ya kiume. Uchendu anadokeza kuwa ubabe wa vijana wa kiume huhusishwa na sifa za kimaumbile na kisaikolojia. Kulingana na utafiti huu, sifa za ubabedume zilizojitokeza katika taifa la Nigeria ni kama vile jinsia ya kiume kuwa na nguvu za kimaumbile, ujasiri, kuwa na hadhi ya juu na ukakamavu. Kutokana na utafiti huu ilibainika kuwa uwezo wa uumeni ulijitokeza hata kabla ya ukoloni miongoni mwa jamii tofauti za Nigeria. Mila, dini, elimu na mazingira yalichangia zaidi katika ufafanuzi wa ubabedume miongoni mwa vijana hawa. Utafiti huu wa Uchendu ulikuwa hazina muhimu katika kuelewa kwa undani nadharia ya ubabedume. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwani uliangazia ubabedume miongoni mwa vijana katika vyuo vikuu huko Nigeria.

Onyango (2007) alifanya uchanganuzi wa uanaume na ubabedume katika fasihi ya watoto. Alibainisha uamilifu wa fasihi katika mchakato wa ujamiishaji hasa mgao wa majukumu kiuana. Onyango alichanganua vitabu vitatu vya watoto ambavyo vimeandikwa na Ken Walibora. Vitabu hivi ni: *Mtu wa mvua*, *Ndoto ya Amerika* na *Mgomba changaraweni*. Uchanganuzi wake ulibainisha kuwa idadi ya wahusika wa kike ni ndogo ikilinganishwa na jinsia ya kiume. Onyango alihitimisha utafiti wake kwa kutoa kauli kuwa itikadi za kijamii humjamiisha mwanamke kama kifaa. Kazi ya Onyango ni tofauti na utafiti uliofanywa kwani utafiti wake uliangazia fasihi ya watoto. Utafiti huu ulichangia kazi yetu kwani ulichanganua ubabedume katika fasihi ya

watoto. Hata hivyo, utafiti huu wetu ulichanganua wahusika teule kwa misingi ya kibabe dume katika riwaya za Ben Mtobwa.

Katola (2006) alitafiti kuhusu udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Masuala ya kimsingi aliyochunguza ni kuhusiana na jinsia katika fasihi ya Kiswahili. Alichunguza sura, picha na taswira ya mwanamke kama inavyojitokeza katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti wa Katola ulihusu udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili. Utafiti wake ulionyesha mojawapo ya udhalimu unaomkandamiza ni jamii kuongozwa na mfumo wa uwezo-kiume. Utafiti wake ulikuwa muhimu kwa mada yetu kwani tulichunguza vile ubabedume unajitokeza miongoni mwa wahusika teule katika riwaya mbili za Ben Mtobwa. Hivyo utafiti wake ulifaa kazi yetu kwani aligusia vyanzo vya ubabedume na unavyojitokeza katika sura tofauti.

Ubabedume hutawala jinsia ya kike kwa njia tofauti. Wanawake huachiwa majukumu ya nyumbani na wanaume. Mawazo haya ni kulingana na Onyoni (2012) aliyefanya utafiti kuhusu usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za *Natala* na *Mama Ee*. Fauka ya hayo, aliangazia vipengele vya fani kama vile, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha kama vinavyomsawiri mhusika wa kike katika tamthilia hizo teule. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani alijikita katika usawiri wa wahusika wa kike huku utafiti wetu ukichunguza wahusika teule kwa misingi ya kibabedume katika riwaya mbili za Ben Mtobwa. Kwa upande mwingine utafiti wa Onyoni ulikuwa nguzo muhimu kwa vile umegusia vile ubabedume unavyoendeleza ukandamizaji wa jinsia ya kike katika jamii.

Kweyu (2007) alichunguza uhakiki wa mfumo wa ubabedume na mfumo wa kijamii katika kazi za Kezilahabi. Ameshughulikia suala la ubabedume kwa undani. Anasema kuwa ubabedume umesababisha kudhulumiwa kwa jinsia ya kike. Alionyesha vile utamaduni wa Kiafrika unavyomkandamiza mwanamke. Pia katika utafiti wake alishughulikia wajibu wa wavulana katika jamii inayotawaliwa na mifumo ya ubabedume. Utafiti wake ulichangia kuchunguza wahusika teule kwa misingi ya kibabe dume katika riwaya za Ben Mtobwa.

Onyango (2015) alibainisha kuwa matangazo ya bia huwa yanaegemea ubabedume. Matangazo ya biashara ya bia yaliyoshughulikiwa yalionyesha wanaume walikuwa

vielelezo huku wanawake wakionekana kukosa usemi mkuu. Matangazo yaliyoshughulikiwa ni kama ya bia zifuatazo: *Guiness*, *Tusker*, *White cap*, *Pilsner* na *Johnnie Walker*. Pia katika makala hayo ya kiusomi yalionyesha vile wanajamii wanahusisha pombe na wanaume kulingana na utamaduni wao. Jamii nyingi hasa za Kiafrika zina majina ya wanaume yanayohusishwa na pombe. Kwa mfano, *Wamalwa*-Luhya, *Wanjoh*i-Kikuyu, *Munywoki*- Kamba, *Mwachofi*- Pwani na *Kimaywa*-Kalenjin. Utafiti huu wa Onyango ulikuwa na manufaa kwani aliangazia vile matangazo ya bia huegemea ubabedume nchini Kenya. Pia utafiti huu wa Onyango ni tofauti na uliofanywa kwani alitumia nadharia ya Uchanganuzi Uhakiki Usemi.

Methali za jamii ya Wakikuyu zinamdhalilisha mwanamke huku zikitukuza mwanamume. Ubabedume unaojitokeza katika methali hizi hushamirishwa na utamaduni wa jamii husika. Hali hii huleta mgao hasi wa kijinsia kwani kuna utengano wa jinsia zote mbili. Mwanamume alichukua nafasi ya kwanza katika shughuli zote za jamii. Gitu (2016) alitafiti ubabedume unavyojitokeza katika methali za Wakikuyu. Utafiti wa Gitu ulitumia nadharia ya ubabedume. Hata hivyo, utafiti huu ulichanganua wahusika teule kwa misingi ya kibabedume katika riwaya mbili za Ben Mtobwa. Utafiti wa Gitu ulikuwa pia na manufaa kwa kazi hii kwani alitumia nadharia ya ubabedume.

Utamaduni na ubabedume huchangia katika kudhalilishwa kwa jinsia ya kike. Asasi ya ndoa hukandamiza wanawake katika jamii za Kiafrika. Yego (2013) alitafiti kuhusu nafasi ya mwanamke katika nyimbo za Taarab. Alisawiri jinsi ambavyo jamii imetawaliwa na mfumo wa kuumeni huku mfumo wa kuukeni ukidhalilishwa. Mwanamke anadhulumiwa kimwili na kimawazo. Mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye hana usemi katika masuala ya uchumba na mapenzi. Hali hii inamfanya mwanamke kutengwa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hivyo basi, mwanamke anachukuliwa kama kiumbe dhaifu huku akipewa nafasi finyu. Utafiti wa Yego ni tofauti na wetu kwani alitumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Utafiti wake kwa upande mwingine utakuwa na mchango kwetu kwani ameangazia jinsi ubabedume unavyodhalilisha jinsia ya kike.

Nkumbo na wengine (2018) walitafiti kuhusu usawiri wa jinsia katika lugha mwiko na ya tasfida miongoni mwa jamii ya Ameru. Walitumia nadharia ya Uwezo-uume na kuchunguza istilahi za lugha mwiko na tafsida katika jamii ya Ameru. Walionyesha miktadha ya matumizi ya lugha mwiko na ya tafsida na jinsi ambavyo jinsia

inasawiriwa katika jamii ya Ameru. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha jinsi mwanamke anavyodunishwa kupitia kwa lugha mwiko na ya tasfida ilhali mwanamume anatukuzwa. Walidai kuwa udunishaji huu hutokana na utamaduni wa jamii ya Ameru. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti, imebainika kuwa mtazamo wa jinsia ya kiume hupewa hadhi kuu. Hali hii huendeleza kumkandamiza mwanamke na kumtukuza mwanamume. Hata hivyo, utafiti wa Nkumbo na wengine ni tofauti kwani uliegemea kipengele cha lugha miongoni mwa jamii ya Wameru.

Abudi (2011) katika utafiti wake kuhusu matumizi ya semi na nahau za Waluo zinazoonyesha ubaguzi wa kijinsia katika miktadha mahususi. Anaelezea ubaguzi wa kijinsia unaodokezwa na tamathali hizi kwa njia isiyo wazi na kuonyesha jinsi watumiaji wazo huakisi na kujenga uhusiano wa uwezo usio sawa kati ya wanawake na wanaume katika jamii hiyo. Licha ya kuwa Abudi alihakiki vipashio vya lugha, utafiti wake ni tofauti na huu kwa misingi kwamba utafiti huu uliangazia utanzu wa fasihi simulizi. Hata hivyo, kazi yake ilikuwa ya msingi katika kuhakiki na kuchanganua jinsi lugha na viambajengo vyake ni msingi katika usawiri wa ujinsia na udumishaji wa ruwaza za mahusiano ya kiuwezo baina ya jinsia ya kike na ya kiume. Kwa upande mwingine, utafiti wake ni tofauti na huu wetu kwani ulishughulikia uchanganuzi wa wahusika teule kwa misingi ya kibabedume katika riwaya mbili za Ben Mtobwa.

Mirikau (2011) alichunguza taswira ya mwanamke katika tamthilia zake Wamitila. Anadhihirisha namna ambavyo mwanamke ana utegemezi mkubwa wa kiuchumi na hata kifikra ilhali bado analimbikiziwa mzigo mzito katika jamii. Hii ni taswira mojawapo anayoangazia mhakiki huyu. Alionyesha sura mbalimbali za ubabedume zinavyojitokeza kwa sababu ya mfumo kuumeni. Alisawiri jinsi majukumu yamegawika kwa misingi ya kategoria za jinsia. Hata hivyo, anaonyesha namna ambavyo mwanamke mwenyewe amedhihirishwa kuwa anaweza kuongoza vyema akipewa nafasi. Hayo anayasema akiangazia taswira ya mwanamke katika tamthilia ya *Pango*. Mhakiki huyu anaeleza namna ambavyo mwandishi amefaulu kumsawiri mwanamke katika kazi yake. Kazi hii ilikuwa na umuhimu mkubwa kwetu kwani tulichunguza wahusika teule kwa misingi ya kibabedume katika riwaya teule za Ben Mtobwa, suala linalohusiana na ujinsia.

Suala la kuegemea kuume limekita mizizi katika utamaduni wa jamii na ni vigumu sana kuliondoa. Greer (2000) anadokeza kuwa, kuendelezwa kwa mfumo kuumeni kuna

sehemu mbalimbali: kwanza, katika kujamiana ni mwanamume ambaye amepata uhuru akilinganishwa na mwanamke. Lazima mwanamke amtosheleze mwanamume kingono, lakini suala la mwanamke kutoshelezwa limepuuzwa. Pili, mwanamke bado anatarajiwa aushughulikie mwili wake na jinsi anavyoonekana. Hajaruhusiwa avalie na ajionyeshe apendavyo bali amewekewa vikwazo. Tatu, mwanamke bado anamwogopa mwanaume. Suala la mwanamume kuonekana mwenye uwezo linatiliwa mkazo na wanaowafunza wanawake wawaogope wanaume visirani kama vile wabakaji. Anaendelea kusema kuwa wasichana wanafunzwa sheria za kuwa wanawake tangu utotoni na ndiposa wanakuwa na fedheha kuhusu miili yao na kupoteza uhalisia wao na haki ya kujitawala. Matokeo yake huwa ni udhaifu, kujitenga, kujidunisha na kukosa furaha. Anadai kuwa wanawake wanatakiwa kujua na kukubali miili yao na kuachana na hali ya useja.

Maclness (1998) anasema "Ikiwa kuwa mwanaume ni suala la anatomia basi suala la uume/ ubabedume ni suala la kijamii, kitamaduni na kihistoria." Mtazamo huu hushikilia kuwa mwanaume ni binadamu mwenye uwezo, bidii, nguvu, uhodari, mwenye mafanikio katika michezo na biashara. Aidha, wana nafasi muhimu nje ya majukumu ya nyumbani zaidi ya wanawake. Utafiti wake ulichangia kazi yetu kwani uliangazia suala la ubabedume. Kazi za wataalamu hawa zilijikita katika uchanganuzi wenye kuongozwa na mtazamo wa ujenzi wa ubabedume katika jamii mbalimbali; kijamii, kihistoria na kiutamaduni. Hata hivyo, kazi hii ilikuwa na mchango muhimu katika ulinganishi na ulinganuzi wa sifa tajwa katika kazi za wataalamu waliorejelewa na zile zinazobainishwa katika vipengele vya tamthilia za *Kilio cha Haki* na *Sudana*.

Richmond (1992) katika kazi yake ya ujamiishaji awali wa majukumu ya kijinsia anabainisha umuhimu wa lugha kama kiambajengo muhimu cha jamii, kwani ni kioo cha jamii hiyo kuutazama utamaduni wa jamii yao. Lugha huratibu na kuonyesha bayana mipaka ya fikra za kila mwanajamii kuhusu mielekeo, imani na maazimio yao. Alionyesha vile kulivyo na sura mbalimbali za ubabedume ikiwemo katika matumizi ya lugha. Kazi ya Richmond ni tofauti na utafiti huu kwani yeye amezingatia lugha kwa ujumla wake katika tamaduni mbalimbali. Hata hivyo, mtazamo wake ulikuwa dira katika kuhakiki lugha waliyoitumia waandishi Alamin Mazrui na Kimani Njogu katika kubainisha jinsi ujinsia na ruwaza za kiuwezo husimbwa kupitia kwa uhusika wa wahusika wa kike na wa kiume. Matokeo ya

uhakiki wa kazi hizi ulibainisha kuwa itikadi za kuumeni hutawala, hivi kwamba wahusika wanawake wamejengwa kama vifaa visaidizi ilhali wahusika wanaume huchukuliwa kuwa na nafasi muhimu, wenye kujituma, wenye uwezo, wenye hekima katika kufanya maamuzi, sio waoga, wenye vifua vipana na wenye kujihusisha na vitendo hatari. Isitoshe, wahusika wa kiume ni wengi mintarafu ya idadi katika kazi hizi kuliko wa kike. Kiishara suala hili linaakisi wingi wa wanaume katika jamii halisi na vilevile walio na mamlaka. Mwanamke amedunishwa katika jamii na amebaki kunyenyekea kwa mwanamume.

Kimondiu (2019) aliyetafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba, alibaini kuwa katika jamii ile imeongozwa na mfumo wa ubabedume. Alionyesha vile mwanamke amesawiriwa kwa njia chanya na hasi katika nyimbo za sifo za Wakamba. Pia alibaini kuwa mwanamke amepiga hatua japo ndogo katika ukombozi dhidi ya mfumo wa ubabedume. Mtafiti huyu alitumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika. Utafiti wake ulikuwa mchango mkubwa kwa kazi yetu kwani umegusia suala la migao ya kijinsia.

Riro (2006) katika utafiti wake kuhusu usawiri wa mwanamume katika nyiso za jando za Abakuria, alidhihirisha jinsi matarajio, mitazamo na mielekeo ya jamii huchukua nafasi muhimu katika kuratibu majukumu ya kiuana na kutathmini thamani ya kila jinsia. Aidha, alibaini kuwa jamii ya Abakuria humsawiri mwanamume kwa njia chanya tofauti na mwanamke. Kulingana na Riro, dhana 'mwanamume' ipo kwa misingi ya kibayolojia ilhali 'ubabedume' hutokana na mielekeo, imani na matarajio ya utamaduni wa jamii husika. Licha ya kuwa, alitumia nadharia ya ubabedume alijikita katika fasihi simulizi ya Abakuria. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwani ulichunguza wahusika teule kwa misingi ya kibabe dume katika riwaya za Dar-*es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka.*

Mwanamke husawiriwa kama pambo la kutamaniwa au kiumbe duni ambaye mahali pake ni kitandani. Ilibainika kuwa jamii ilishamiri utamaduni wa mfumo kuumeni. Senkoro (1987) alibaini haya alipotafiti kuhusu usawiri wa wahusika wa kike katika fasihi ya mfumo wa kibepari. Kazi yake ilijikita katika kuchunguza wahusika wa kike katika fasihi. Mfumo wa ubabedume humchukulia mwanamke kama chombo cha kujifurahisha na kumzalia mwanamume watoto. Utafiti huu wa Senkoro ulikuwa

wa manufaa kwani umeangazia mfumo kuumeni uliostawi katika jamii, jambo ambalo utafiti huu ulichunguza katika jamii ya riwaya mbili za Ben Mtobwa.

Mienendo ya kijinsia haijafungamanishwa na matendo tengwa bali tawi la mkusanyiko wa mienendo ya kijinsia. Connell (2011) katika makala yake alibaini kuwa jinsia ni namna mienendo ya kijamii inavyopangwa. Alichunguza uhusiano wa jinsia na mifumo ya kijamii. Mienendo hii huhusishwa na mikakati ya kuzaa na miundo ya mwili wa binadamu. Taasisi zilivyopangwa kwa misingi ya kijinsia sio tu za kijazanda bali pia zile zinazodhihirika kwa njia ya utendaji.

Anadokeza kuwa mfano wa nchi ilivyopangwa kijinsia kwa mpangilio wa mienendo kwa kuhusisha uwanja wa uzalishaji. Alibaini kuwa wanaume ndio bado wanashikilia nafasi zenye uwezo katika nchi sio sababu ya kipekee kuwa nchi inaegemea kuume bali ni matokeo yake. Anabainisha kuwa uume hujumuisha taratibu mbalimbali na mwishowe hufikia mitafaruku ya ndani kwa ndani na mabadiliko ya kihistoria. Ili kutambua jinsia kama ruwaza ya kijamii, ni lazima ionekane kama tukio la kihistoria na linalozua historia.

Kulingana na utafiti wa Onyango (2011) mwanamke katika jamii nyingi za Kenya anatarajiwa kujikakamua ili amfurahishe mumewe kingono na inadaiwa kuwa asipofanya hivyo, anampa mumewe kibali cha kutafuta wanawake wengine. Anaendelea kusema katika baadhi ya jamii za Magharibi mwa Kenya zilizoingiliana na Waganda, mwanamke ni lazima ang'ang'anie kumvutia mumewe kingono ili aweze kumsitiri dhidi ya wanawake wengine kutoka Uganda wanaoweza kumvutia. Mwanamke asiyemtosheleza mumewe kingono huonekana kana kwamba ni bure. Isitoshe, mwanamke ana majukumu mengi kama vile, kulima, kuchota maji, kutafuta kuni, kupika, mlezi na zaidi kumfurahisha mumewe kingono. Utafiti wa Onyango ulikuwa na manufaa katika utafiti huu kwani umeangazia suala la jinsia na uwezo.

Holter (2005) anabainisha ruwaza za kiuwezo katika mfumo wa utawala msonge wa kijinsia. Kategoria anazozibainisha katika mfumo huu ni mwanamume na mwanamke. Anadokeza kuwa uhakiki wa usawa wa kijinsia uchunguzwe kwa misingi ya majukumu ya kila mwanajamii katika kuhalalisha nafasi ya kila jinsia. Anasema kuwa jamii huwa na mchango mkubwa katika kuwaweka wanajamii katika kategoria sawa au tofauti kutegemea jinsia yao. Mfumo huu hujengwa na utamaduni, uchumi, saikolojia

na mahitaji ya kijamii. Vipengele hivi huwa vijenzi vya mahusiano ya wanajamii mintarafu ya ruwaza za kiuwezo. Licha ya kwamba kazi ya Holter ni tofauti na utafiti huu, mawazo yake yalikuwa mwongozo katika kubainisha ubabedume miongoni mwa wahusika teule.

Itikadi za jamii zimekuwa zikimkandamiza mwanamke. Hata hivyo, inabainika kuwa ukandamizaji huu unaonekana kukomeshwa na wimbi la mabadiliko. Mwikali (2014) alifanya uchanganuzi wa kijinsia katika vipengele vya tamthilia za *Kilio cha Haki* na *Sudana.* Mwanamke anaonekana kuzinduka na kuwa na mwamko mpya. Jinsia ya kike imesawiriwa kwa njia chanya. Inaonekana kuwa sifa ambazo jamii inatarajia mwanamume kuwa nazo mwanamke anaweza kuwa nazo ili aweze kupiga hatua kubwa maishani.

Mwanamke anajitokeza kuwa jasiri, thabiti na anayekimu familia. Kwa upande ule mwingine mwanamume anasawiriwa kama mwoga, mwenye dharau, kigeugeu, mbinafsi na mnyonge. Ijapokuwa mtafiti alitumia nadharia ya uchanganuzi uhakiki usemi na nadharia ya ishara, utafiti huu ulikuwa na manufaa kwa utafiti wetu kwani uliangazia suala la mahusiano ya kijinsia. Hata hivyo, utafiti wetu ni tofauti kwani ulitumia nadharia ya ubabedume na ulijikita katika riwaya mbili za Ben Mtobwa.

Khaemba (2013) ameshughulikia ujenzi wa ubabedume katika mivigha ya jamii ya wabukusu. Mivigha aliyochunguza katika utafiti wake ilikuwa; *Khulicha* (tohara), *Khuvita* (mafunzo kwa vijana wa kiume waliotahiriwa wakiwa bado jandoni) na *Kumuse* (sherehe inayofanywa siku tatu baada ya kuzikwa kwa mwanamume mkongwe). Katika utafiti wake alionyesha vile ubabedume hujengwa na kutiliwa mizizi na itikadi zinazomkweza mwanamume na kumtweza mwanamke. Pia alionyesha vile wanajamii hasa wanaume hutumia mbinu mbalimbali za uneni katika kuendeleza uwezo na mamlaka yao katika jamii. Kazi hii ya Khaemba ni tofauti na utafiti huu kwani alijikita katika ujenzi wa ubabedume katika miviga ya wabukusu. Utafiti huu pia ulikuwa na mchango mkubwa kuelewa dhana ya uwezo na mamlaka katika jamii inayoendeleza ubabedume. Utafiti wa Khaemba ulishughulikia ubabedume katika kipera cha fasihi simulizi nao utafiti wetu ulichanganua wahusika teule kwa misingi ya kibabedume katika riwaya mbili ambazo ni; *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka*.

### 2.1.2 Athari ya Ubabedume kwa Jinsia

Mboya na wengine (2018) wanadai kuwa jamii za Kiafrika bado zinaendelea kutatizwa na ubabedume ambao humwona mwanamke kama kiumbe dhaifu na aliyefungwa katika pingu za utegemezi wa jinsia ya kiume. Wasomi hawa walichunguza dhuluma kama kichocheo cha mzinduko wa wanawake katika riwaya za Kiswahili. Wanadokeza kuwa badala ya asasi kama vile ndoa na dini kuendeleza mshikamano, ndizo zinaendeleza utengano. Hali hii hujitokeza katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na hata kitamaduni na kumwacha mwanamke katika dunia ya upweke na jitimai. Wanasema kuwa wanawake wamenyimwa uwezo wa kujiendeleza na hata kuvumbua mapya. Kulingana na wasomi hawa, ubabedume una athari hasi kwa jinsia ya kike. Utafiti huu ulikuwa na mchango mkubwa katika kazi hii kwani uliangazia suala la ubabedume katika jamii za Kiafrika.

Ngumo (2014) alibainisha kuwa wanaume husawiriwa kama wenye uwezo katika majarida na magazeti. Mtafiti huyu alichunguza ujenzi wa utambulisho wa ubabedume katika magazeti nchini Kenya. Alidai kuwa haya yalitokana na imani za jamii. Alibainisha kuwa wasomaji wa majarida huachwa na wazo kuwa hayo ni mambo ambayo hayawezi kubadilika. Aliongeza kuwa makala mengine huonyesha wanaume kama viumbe wasiowajibika lakini mwishoni wao husawiriwa kama wenye uwezo. Anadokeza kuwa majarida husisitiza suala la ubabedume ambalo huleta kutowepo kwa usawa wa kijinsia. Utafiti wake ulidokeza kuwa wale wanaume ambao hurejelewa kama walawiti na kama 'wanawake' huonekana kuwa dhaifu na wasio na uwezo. Hali inasawiri wanawake kama viumbe duni. Pia alibaini kuwa wanaume huwa waangalifu hasa kulingana na taswira inayojitokeza kwa jamii. Alionyesha kuwa ubabedume ambao umekita mizizi miongoni mwa wanajamii umetokana na itikadi za jamii. Alitumia nadharia ya Kijamii na pia ya Uchanganuzi Uhakiki Usemi. Utafiti huu uligusia vile ubabedume unajitokeza katika majarida ya magazeti lakini wetu ulichanganua wahusika teule kwa misingi ya kibabe dume katika riwaya mbili za Ben Mtobwa.

Kimani (2003) alitafiti kuhusu suala la dhuluma dhidi ya wanawake katika fasihi ya Kiswahili. Alibainisha kuwa mwanamke anakabiliwa na dhuluma za aina nyingi kutoka kwa wanaume. Alionyesha kuwa asasi za ndoa na dini zimekuwa zikiendeleza ukandamizaji wa mwanamke. Pia, alidokeza kuwa kuna tofauti kati ya falsafa ya

wandishi wa kike na wa kiume kuhusu suala la dhuluma dhidi ya mwanamke. Fauka ya hayo, aliangazia aina za dhuluma dhidi ya wanawake na sababu zake. Alibaini kuwa dhuluma dhidi ya wanawake huendelezwa kwa kupigwa, kutukanwa na kunyimwa haki ya urithi. Alidokeza kuwa hali hii huendelezwa kupitia dharau, kuozwa bila haki, kukanwa na wazazi pamoja na vitisho. Utafiti wake pia uligusia athari za dhuluma dhidi ya wahusika wa kike. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa dhuluma husababisha kuvunjika kwa ndoa, uasi wa dini na hata vifo. Zaidi ya hayo ni kuwa hali ya utamaushi hujitokeza na kujazwa hofu. Alidai kuwa dhuluma hizi zimeendelezwa na itikadi ambazo humpendelea mwanamume akimnyanyasa mwanamke. Pia alidokeza kuwa dhuluma dhidi ya mwanamke zinatokana na maumbile yao. Alibaini kuwa dini na ndoa ni miongoni mwa asasi zinazotumiwa kuwanyanyasa wanawake. Utafiti huu ulikuwa na mchango katika kazi yetu kwani umeangazia athari za dhuluma kwa mwanamke. Utafiti wake ni tofauti kwani alitumia nadharia ya Mtazamo-kike.

Muchenje na wengine (2018) walichunguza nyimbo za Bendi ya *Webuye Jua Kali* ya Mkoa wa Magharibi nchini Kenya. Utafiti huo ulinuia kufahamu sifa za wanaume halisi. Kutokana na utafiti huo ilibainika kuwa wanaume hupewa hadhi ya kuwa wanaume halisi kutokana na jitihada zao za kukandamiza wanawake. Ilibainika kuwa wanaume huwa na nafasi kuu na uwezo huku wanawake wakiwa watumishi na viumbe waliodharauliwa katika jamii. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa suala la ubabedume bado liko na linapokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Katika nyimbo hizi wanawake wamesawiriwa kwa njia hasi.

Wao wanaonyeshwa kama viumbe ambao hawana usemi, wasio na maarifa, wasiowajibika na viumbe waliochukiwa katika jamii. Kwa upande mwingine wanaume wameonyeshwa kama wawajibikaji, wasemaji, watawala na wanadamu walio na maadili ya hali ya juu. Ni kumaanisha kuwa wanaume ndio huwa na sifa halisi za binadamu. Wanawake wamesawiriwa kama malaya huku wanaume wakionyeshwa kama wateja. Hivyo basi, mwanamke anakandamizwa na mfumo wa ubabedume ambao unampa mwanamume uwezo. Utafiti huu ulikuwa na mchango mkubwa kwani uliangazia ubabedume katika nyimbo teule za bendi ya *Webuye Jua Kali*. Kwa upande mwingine ulikuwa tofauti kwani ulijikita katika kipera cha fasihi simulizi na ulitumia nadharia ya Uchanganuzi Uhakiki Usemi.

Ubabedume katika jamii nyingi za Kiafrika huwanyima wanawake haki kwa kuwatengea wanawake nafasi finyu iliyo na hadhi ya chini. Riro (2015) anadai kuwa jamii imekweza mwanamume na pia kuonyesha mfumo wa kingazi katika majukumu. Pia jamii imempa mwanamume mamlaka makubwa na kufanya mwanamke kuwa mtegemezi. Anasema kuwa mfumo wa ubabedume haumruhusu mwanamke nafasi yoyote ya uongozi na hubaki kuwa kiumbe kitegemezi wakiwa na watoto kwani mume ndiye kichwa cha familia. Utafiti huu unaonyesha wanawake wanakandamizwa na hupitia maonevu mengi. Majukumu ya mwanamke katika mfumo huu yanabaki ya nyumbani hasa kumpa mwanamume huduma.

Fauka ya hayo, wanapoolewa wanakuwa mali ya mwanamume, kulea watoto na hata kupika. Kulingana na mtafiti huu ni bayana kuwa ubabedume katika jamii mbalimbali za ulimwengu ni suala ambalo limeibua changamoto katika mijadala na makongamano mbalimbali. Anaendelea kusema kuwa ubabedume hujitokeza katika hali mbalimbali mintaarafu ya mitagusano ya kijamii. Majukumu yao yanazunguka jikoni bila kuhusishwa na masuala ya kiuchumi na kisiasa. Utafiti wake unaonyesha kuwa nguvu za jinsia ya kiume hudhibiti wanawake. Utafiti huu ulikuwa na mchango kwa kazi yetu kwani umengazia athari za ubabedume kwa jinsia ya kike.

Wandera (2015) alitafiti taswira za kimenke katika hadithi za *Abanyala(Mumbo*) wa Kenya. Anaonyesha mwanamke kibyongo katika hadithi za Abanyala ambaye anawaokoa watoto wake na mumewe kutokana na shemejiye ambaye ni jini. Jini anatishia kuangamiza maisha yao. Mwanamke anaonekana kigogo katika familia baada ya kukata minyororo ya ubabedume. Wandera anaonyesha nafasi ya mwanamke ilivyodunishwa katika suala la kidini.

Katika dini ya Kiislamu anadai kuwa wanawake hawakuruhusiwa kushiriki shughuli zozote za Uislamu hadi wakati palipozuka mmoja wao kutoka taifa la Nigeria aliyepigania haki ya kushirikishwa kwao. Utafiti huu ulichangia kazi yetu uliangazia vile mwanamke anajaribu kujikwatua kutoka kwa minyororo ya ubabedume. Alitumia nadharia ya umenke na masimulizi. Wandera (2015) akirejelea Veit-wild na Naguschewski (2005) anadai kuwa fasihi ya kiafrika ina aina na vijiaina vya fasihi, na kwamba hakuna njia moja ya kutazama fasihi hii.

Wamitila (2006) aliuzungumzia utamaduni wa kimagharibi na wa jamii nyinginezo kuhusiana na kumtukuza mwanamume zaidi na kuonekana ni mwenye kukandamiza mwanamke. Alisisitiza kauli kuwa utamaduni huo unatazamwa kama unaoegemezwa kuumeni. Utamaduni huu humkweza mwanamume huku mwanamke akikwazwa. Wamitila ameendelea kwa kumweleza mwandishi Kate Millet aliyeandika kitabu cha *Sexual Politics*. Katika kitabu hiki aliwashambulia vikali baadhi ya waandishi maarufu wa kiume kwa namna walivyosawiri wahusika wao wa kike. Amewataja waandishi kama D.H. Lawrence, Henry Miller, Norman Mailer na Jean Genet. Alibainisha kuwa miundo ya kijamii na asasi zake zinashirikiana kumkandamiza mwanamke. Utafiti huu wa Wamitila ulisaidia katika upambanuzi wa athari za ubabedume kwa jinsia.

Muleka (2016), alichunguza mahusiano ya kijinsia na jinsi mtoto wa kike anavyoshirikishwa katika jamii miongoni mwa Wafrika kupitia hadithi. Alibaini kuwa mtoto wa kiume huthaminiwa sana kwa mujibu wa hadithi alizozichunguza. Katika hadithi za Wanakhatandi miongoni mwa Abukusu, mada ya diskosi ya ubabedume inajitokeza pale ambapo inapotajwa kuwa Wanakhatandi amelaaniwa kwa kuwa na watoto wa kike pekee. Inaonyesha kuwa mtoto wa kiume alipewa kipaombele. Utafiti huu unatupa mtazamo wa jamii ya Abukusu kuhusiana na suala la ubabedume.

Waiganjo (2014) akimrejelea Simone De Beauvoir anashambulia asasi ambazo zinachangia kumkandamiza mwanamke. Mtafiti huyu alichunguza upeketevu wa wanawake katika riwaya teule za Said A. Mohammed. Katika utafiti wake alibaini kuwa asasi zinazomkandamiza mwanamke ni kama vile dini, ndoa na utamaduni. Dini humkandamiza mwanamke kwa kumfundisha kunyenyekea. Ndoa nayo imejengwa kwenye misingi na imani ya uwezo mkubwa alionao mwanamume akilinganishwa na mwanamke. Hatimaye anaishambulia mielekeo ya kitamaduni ya kumfanya mwanamume kama kaida ya binadamu kielelezo. Kulingana na mtafiti huyu ni kuwa utamaduni anamokulia mwanamke una mchango mkubwa katika kumdhalilisha. Utafiti huu ulikuwa na mchango mkubwa kwani ulichunguza asasi zinazomkandamiza mwanamke.

### 2.2 Misingi ya Nadharia

Nadharia yoyote ile ya kihakiki ni nyenzo ya kutusaidia kulifikia lengo fulani. Uteuzi wa nadharia mojawapo kwa mhakiki hufungamana na lengo alilo nalo mhakiki huyo.

Dhamira ya kuweko kwa nadharia ni kumwezesha mhakiki kuyaangazia masuala mbalimbali kwa kina na kwa mpangilio maalum, (Wamitila 2002). Katika utafiti huu, mtafiti aliongozwa na nadharia ya ubabedume. Katika sehemu hii mtafiti alishughulikia mwasisi wa nadharia ya Ubabedume pamoja na historia yake. Pia aliangazia mihimili ya nadharia hii pamoja na vile nguzo hizi zilitumika katika utafiti.

### 2.2.1 Nadharia ya Ubabedume

Nadharia ya ubabedume ilianza miaka ya 1980. Mwasisi wake ni mwanasosholojia Raewyn Connell. Connell (1980) anabaini kuwa dhana ya ubabedume iliasisiwa mara ya kwanza katika ripoti za usomi kuhusiana na ubaguzi wa kijamii katika shule za upili nchini Australia kisha ikapambanuliwa zaidi na Connell mwaka wa 1987. Nadharia hii ni muhimu katika masuala ya kijinsia. Hii ndiyo nadharia yenye ushawishi mkubwa katika usomi wa wanaume na uwezo wao. Nadharia hii inatoa uchambuzi muhimu wa jinsia ya kiume na kike na vile jamii huipa jinsia ya kiume kipaumbele. Nadharia hii hurejelea uwezo wa kingazi katika jamii iliyotawaliwa na umenke. Jinsia ya kiume hushindana kuwa katika nafasi ya kwanza. Nadharia hii hujaribu kuhalalisha uwezo wa jinsia ya kiume dhidi ya jinsia ya kike. Ubabedume huonekana kama njia ambayo huipa jinsia ya kiume nafasi kuu katika jamii na hudhihirisha uwezo wa mwanamume kwa mwanamke.

Nadharia hii hujaribu kufafanua ni kwa nini wanaume hukwezwa kimajukumu ikilinganishwa na jinsia ya kike. Kulingana na Gitu (2016) nadharia ya ubabedume hujaribu kuelezea vile jinsia ya kiume huchukua nafasi kuu katika majukumu ya kijamiii ikilinganishwa na jinsia ya kike au kikundi kingine cha watu wengine wa jinsia ya kiume wanaobaguliwa. Pia Gitu (2024) anatoa maelezo ya ubabedume kutokana na mawazo ya kiulaya. Maelezo haya yanasawiri mwanamume kama mtu jasiri, anayefoka na pia anayetawala wanawake.

Isitoshe, nadharia hii inajikita katika maumbo ya utambulisho wa jinsia ya kiume kwa kuzingatia jamii, maandishi na maelezo ya kihistoria. Kulingana na Wells na Holland (2001), wasomi kama Robert Bly wa Marekani waliendeleza nadharia hii. Kichocheo kikuu cha hali hii kilitokana na uhakiki wa jinsia ya kiume na utawala wa wanaume unaoathiri kila sehemu ya jinsia ya kike pamoja na mageuzi ya miaka ya 1960. Huu ulikuwa wakati wa upeo wa mgogoro wa itikadi za kijamii nchini Marekani ambazo zilitaka kuangaziwe upya majukumu ya kijinsia. Mihimili ya nadharia hii ni:

itikadi za kijamii, uwezo, mamlaka, utamaduni na mazingira. Nadharia ya hii hufafanua sifa mahususi anazostahili kuwa nazo mwanamume, (Kimmel,1997). Hali hii hujengeka mintarafu ya uwezo na mafanikio ya mwanamume. Uwezo huu hubainishwa kwa njia tofauti.

Pia hudhihirisha vile mwanamume hupanda ngazi kiutawala kufikia uamilifu na nafasi yake katika jamii. Kuhusu mgao wa majukumu, Brannon na David (1976) wanatoa kauli kuwa wanaume hujaribu kutojihusisha na majukumu yanayochukuliwa kuwa ya kike. Fauka ya hayo, katika utekelezaji wa majukumu ya kiume, mwanamume hudhihirisha uwezo, mafanikio na nafasi yake ya kutegemewa katika jamii. Aidha, wanadai lazima mwanamume awe shupavu, mvumilivu, ajiamini na kujitegemea. Kulingana na Muchenje (2018) nadharia ya ubabedume hubainisha nguvu na mamlaka inayomilikiwa na jinsia ya kiume. Mamlaka haya hutokana na utamaduni wa jamii husika. Dhakari na wenye kuimiliki ambao ni wanaume hufungamanishwa na chimbuko la nadharia ya uwezo-uume.

Mwenye dhakari huchukuliwa kuwa bora kuliko wale ambao hawana. Hili linatokana na dhakari kuwa ngumu, kubwa, thabiti na yenye nguvu pamoja na uwezo wa kupoteza ubikira na kutia mimba.

Mihimili ya nadharia hii ni:

1. Kwanza kuna itikadi za jamii. Itikadi za kijamii ambazo huongoza mawazo kwamba utawala wa mwanamume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha. Mhimili huu ulikuwa mwafaka katika kuchunguza vile jamii katika riwaya za Ben Mtobwa huratibu mahusiano ya kijinsia na ruwaza za kiuwezo baina ya kiume na ya kike.
   Connell (2005) anasema kuwa mhimili wa itikadi za kijamii hubainisha aula, nguvu, uhodari na uhayawani wa mwanamume kupitia mamlaka yake.
2. Pia kuna utamaduni. Utamaduni ambao huakisi ujumla wa maisha ya jamii ikilinganishwa na mahusiano na matarajio ya jamii kuwahusu. Utamaduni, lugha, imani na desturi huwezesha wanaume kuwa watawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za raslimali kama ajira, pesa, uongozi, ardhi au hata dini. Utamaduni huhusisha imani na desturi ambazo hutamalaki katika mfumo mzima wa jamii. Kuhusiana na mhimili wa utamaduni, Knights (1999) na

Harwood (2000) katika kazi ya Izugbara wanauona uume unakuzwa na kuendelezwa na tamaduni za jamii. Nguzo hii ilikuwa muhimu katika kupambanua wahusika katika riwaya husika kwani mchango wa utamaduni uliangaziwa vile unashamirisha ubabedume.

Mhimili huu pia uliongoza mtafiti kutathmini namna ubabedume huendelezwa na kushamirishwa na mahitaji ya utamaduni.

3. Isitoshe, kuna mgawanyo wa majukumu kiuana. Hivi kwamba kuna majukumu ambayo yametengewa jinsia ya kike na mengine jinsia ya kiume. Mgao huu wa majukumu pia hudhihirisha mgawanyo wa mamlaka na uwezo wa kijinsia. Wanaume huweka utambulisho wao katika sura na mfano wa Mungu ili wajipendelee.

   Mhimili huu ulikuwa muhimu kupambanua wahusika teule katika riwaya husika vile wametengewa majukumu kwa misingi ya kiuana. Mhimili huu pia ulimwongoza mtafiti katika kubainisha namna majukumu katika jamii yanavyoendeleza ubaguzi wa kijinsia na ruwaza za kiuwezo. Fauka ya hayo, nguzo hii ilitumiwa kutathmini nafasi ya kila mwanajamii katika mchakato mzima wa malezi na makuzi.
4. Kuna sifa angama za uwezo kiume. Hizi ni sifa ambazo sharti mwanamume awe nazo. Baadhi ya sifa hizi ni: uhuru, ushujaa, ustahimilivu, ujasiri, ukakamavu, kutaka makuu, ushindani, kudhibiti mambo, kutoonyesha mihemko ya kike na sifa zingine. Mhimili huu ulikuwa mwafaka katika kuchanganua wahusika teule katika riwaya husika kwa kuangazia kuwepo kwa sifa hizi na jinsi zinavyoendeleza ubabedume. Pia ulitumiwa kutathmini namna wahusika hudhihirisha ubabedume kwa kutegemea nafasi, uongozi na mamlaka.
5. Dhana ya jinsia ya kiume kupewa hadhi ya juu. Hali hii imeundwa na jamii kwani wanaamini lazima mwanamume ajihisi mwenye hadhi ya juu kuliko mwanamke. Mhimili huu ulisaidia kusawiri hadhi ya jinsia ya kiume ikilinganishwa na ya kike.
6. Nguzo ya mwisho ni jinsia ya kiume kuwa na uwezo, ukakamavu na hali ya kutawala jinsia ya kike. Hii inasisitiza wanaume kutumia maumbile, hisia na uwezo wa kifedha kutawala wanawake. Hali hii pia imejengeka katika viwango vya wanaume kwa wanaume. Mhimili huu ulisaidia kuchunguza sura mbalimbali za ubabedume hasa vile wanaume hutweza wanaume wenzao. Mhimili huu ulikuwa muhimu kwani mtafiti alichunguza kuwepo kwa hali hii na vile inavyoendeleza ubabedume.

Mihimili iliyotumika katika utafiti huu ilikuwa mitatu. Hizi nguzo nazo ni: Itikadi za kijamii, utamaduni na sifa angama za uwezo-kiume. Mihimili hii iliweza kubainisha kuwepo kwa ubabedume miongoni mwa wahusika teule katika riwaya husika za Ben Mtobwa. Mihimili ya nadharia ya ubabedume ilitumiwa katika utafiti huu kuhakiki sura za ubabedume. Pia mihimili ilisaidia kuchunguza athari za ubabedume kwa jinsia. Nguzo za nadharia hii zilisaidia kuchunguza ikiwa kweli katika riwaya za Ben Mtobwa, *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka* kuna ubabedume miongoni mwa wahusika teule. Mtafiti alitumia kutumia nguzo hizi zote katika utafiti wake.

### 2.2.2 Udhaifu wa Nadharia ya Ubabedume

Nadharia hii ina udhaifu ya kwamba mawazo yake yameegemea Ulaya zaidi. Hii inakwaza matumizi yake katika maeneo mengine. Hata hivyo, nadharia hii ni kigezo muhimu katika utafiti huu. Nadharia hii inaangazia itikadi za kijinsia zinazotumika katika jamii.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alishughulikia ukusanyaji data, uteuzi wa sampuli na mbinu za utafiti. Babbie (1999) anadai kuwa, mbinu za utafiti ni jumla ya kanuni, taratibu, sheria na miongozo ambayo hufuatwa hatua kwa hatua katika kukamilisha utafiti uliokusudiwa kufanyika. Pia alilenga kutoa maelezo kuhusu muundo wa utafiti. Imetoa maelezo kuhusu mbinu mahususi zilizotumiwa katika kukusanya na kuchanganuliwa data kwa kuegemea madhumuni ya utafiti. Zaidi ya hayo, mahali pa utafiti na uteuzi wa sampuli zimeangaziwa.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Kuna mbinu na mikabala mingi ya uchanganuzi wa data lakini utafiti huu uliegemea mkabala wa kimaelezo. Mkabala huu wa kimaelezo ni wa kujadili au kufafanua. Utafiti huu uliendelezwa kwa muundo wa kiuthamano. Mtafiti alisoma vitabu, makala na majarida yanayohusiana na ubabedume katika fasihi. Mtafiti alitoa maelezo ambayo yanahusiana na suala la utafiti. Kulingana na Makini (2015), utafiti wa kimaelezo ni ule unaotegemea maelezo katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data zake.

Muchenje (2018) akirejelea kauli ya Defranzo (2011) anasema kuwa utafiti huu wa kimaelezo msisitizo wake huwa upo katika kuelewa mambo yanayosababisha kutokea kwa jambo. Hivyo basi, utafiti huu ulitoa maelezo ya ubabedume miongoni mwa wahusika teule na vile kuna utwezaji wa wanaume kwa wanaume katika riwaya ya *Dar-es-Salaam Usiku* na Pesa *Zako Zinanuka* . Kwa kifupi data ilikuwa matini kutoka kwa riwaya hizi mbili.

## 3.3 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Utafiti wa maktabani ni bora kwa sababu humfanya mtafiti kutumia muda wake vyema kwa kuliendea jambo ambalo angetaka kuliangazia bila vizuizi vya kupoteza wakati kwa kushughulikia masuala mengine yasiyohusiana na utafiti kama ilivyo nyanjani, (Kothari, 2008). Sababu ya kuteua mahali hapa ni kuwa palimsaidia mtafiti kutambua pengo la kiusomi na pia aliweza kupitia mapitio ya maandiko yanayolingana na mada ya utafiti. Eneo la utafiti huchaguliwa kulingana na lengo kuu la utafiti na ni lazima mahali hapo pawe na data itakayotumiwa katika kufikia malengo ya utafiti husika (Omar, 2014).

Fauka ya hayo, data ilipatikana kwa urahisi maktabani. Kazi hii iliangazia wahusika teule kwa misingi ya kibabedume katika riwaya mbili za Ben Mtobwa. Utafiti pia ulichanganua wahusika hao kwa kufuata mihimili ya nadharia ya ubabedume na madhumuni ya utafiti.

**3.4 Kikundi Lengwa**

Kazi hii ya kiakademia ililenga riwaya zote za mwandishi huyu zinazodhihirisha ubabedume. Waandishi wengi wameonyesha ubabedume hasa katika kazi za sanaa. Hata hivyo, utafiti huu ulilenga jamii ya riwaya za Ben Mtobwa. Riwaya hizi zilichaguliwa kwani zimeandikwa na mwandishi mmoja mwenye tajriba katika masuala ya fasihi. Fauka ya hayo mwandishi huyu alikuwa na upekee na ukwasi katika kazi za fasihi hasa katika riwaya pendwa. Zaidi ya hayo, riwaya hizi zilizolengwa zilikuwa na wahusika teule wenye sifa za ubabedume.

**3.5 Uteuzi wa Sampuli**

Sampuli katika utafiti huu iliteuliwa kimakusudi. Kulingana na Nabangi(2017), sampuli ya kimaksudi humpa mtafiti fursa ya kuchagua sampuli anayofikiria itampa data anazotaka. Hivyo basi, mtafiti aliteua riwaya mbili za Ben Mtobwa nazo ni, *Dar-es-Salaam Usiku na Pesa Zako Zinanuka.* Ben Mtobwa ni mmoja wa wasanii wa riwaya pendwa ambao wameipa fasihi ujumi wa kisasa. Riwaya hizi mbili zilichaguliwa kwani ziliandikwa kitambo lakini zimepitia mabadiliko katika machapisho ya hivi karibuni. Fauka ya hayo, riwaya hizi zina turathi ambazo haijachunguzwa. Mtafiti alichunguza wahusika teule kwa misingi ya kibabe dume. Riwaya hizi mbili ndizo mtafiti alitarajia zingempa data aliyoisaka. Sampuli hii ilimsaidia mtafiti kupata sura za ubabedume na athari za ubabedume kwa jinsia.

**3.6 Ukusanyaji wa Data**

Kulingana na Buliba na wengine (2013), ukusanyaji data ni shughuli muhimu sana katika utafiti wowote. Data ndiyo malighafi ya utafiti. Data iliyokusanywa hutumika kujibu maswali ya utafiti. Data ilihifadhiwa katika vitabu na maktabani. Mtafiti alisoma vitabu, makala na majarida yanayohusiana na utafiti huu. Pia alisoma riwaya mbili ambazo ni; *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka* kwa kina huku akidondoa matini ambazo zitatumika kuchanganua ubabedume miongoni mwa wahusika teule. Katika maktaba, mtafiti alifaidika katika kutambua pengo ambalo linahitaji kutafitiwa. Maktabani pia mtafiti alifanya mapitio ya maandishi ili kutambua maoni ya wasomi

wengine kuhusiana na suala ambalo lilitafitiwa. Pia alitambua changamoto ambazo watafiti wengine walipitia na mapendekezo ya watafiti hawa kuhusiana na suala la utafiti. Msingi wa ukusanyaji wa data ulihusisha pakubwa matumizi ya maktaba.

### 3.7 Uchanganuzi wa Data

Mtafiti alitumia mbinu ya uchanganuzi matini. Matini hapa ni makala yalisomwa na kuandikwa. Data ya kimsingi ilikuwa katika riwaya zifuatazo mbili ambazo ni: *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka.* Mihimili ya nadharia ya ubabedume ilikuwa kielelezo katika kuchanganua wahusika hao teule katika riwaya husika. Kwa kuzingatia masuala aliyodondoa, alitoa maelezo kuhusiana na ubabedume miongoni mwa wahusika teule katika riwaya husika. Data za utafiti huu ziliwasilishwa kwa njia ya madondoo na kisha kupambanuliwa kwa kutolewa maelezo ya kina yatakayoweza kujibu maswali ya utafiti . Hili lilifanyika kwa kuongozwa na madhumuni ya mtafiti. Kazi hii ilifanywa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya ubabedume na madhumuni ya utafiti. Kwa kuzingatia nguzo za nadharia hii pamoja na madhumuni ya utafiti, mtafiti aliweza kuangazia vipengele mbalimbali kuhusiana na ubabedume. Jambo hili lilimsaidia mtafiti kutambua ikiwa kweli kuna ubabedume miongoni mwa wahusika teule katika riwaya hizi mbili za Ben Mtobwa. Vipengele vilivyochanganuliwa ni pamoja na: sura mbalimbali za ubabedume na athari za ubabedume kwa jinsia.

### 3.8 Uzingativu wa Maadili

Maadili ni sheria zinazoongoza hulka za wanadamu katika mahusiano yao. Maadili haya huwapa haki wale wanaotagusana na mtafiti katika harakati za kufanya utafiti. Utafiti huu ulifuata kaida za maadili ya utafiti. Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba walengwa hawatapata madhara yanayoweza kudidimiza kazi ya mtafiti anapofikia upeo. Mtafiti alitafuta vibali vya kushiriki utafiti maktabani. Pia kabla ya kukusanya data mtafiti alitafuta idhini kutoka kwa kwa Chuo Kikuu cha Laikipia na Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi Nchini (NACOSTI).

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Katika jamii nyingi, mfumo wa ubabedume humpa mwanamume kipaombele huku mwanamke akichukuliwa kama msaidizi anayemwauni mwanamume. Mtazamo huu hufanya wanaume kuwa kileleni katika mamlaka huku wanawake wakidhalilishwa. Jamii imeweka asasi za kijamii katika mpangilio unaoipa jinsia ya kiume uwezo wa kudhibiti jinsia ya kike. Hivyo basi, mwanamke anabaki kuwa hayawani asiye na mtetezi wa haki zake. Baadhi ya wandishi wa fasihi humulika suala hili na kuliweka wazi hasa vile mwanamke anagandamizwa na mfumo wa kuumeni. Hali hii inaonekana katika dunia nzima wala si katika bara la Afrika. Ukandamizaji huu huwa hautatuliwi kwani mwanamke hukosa usemi wowote katika jamii.

Baadhi ya waandishi wa kazi za sanaa huangazia mfumo wa ubabedume wakidhihirisha changamoto ambazo jinsia ya kike hupitia. Wanafasihi pia huwachora wahusika wa kiume wakidhihirisha ubabedume katika uhalisia wa jamii. Hivyo basi, katika kuangazia suala la ubabedume kwa kina mtafiti aliangazia kazi za Ben Mtobwa. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa mintarafu ya madhumuni ya utafiti na mihimili ya nadharia ya ubabedume. Katika nadharia ya ubabedume, utafiti ulizingatia mihimili kama vile itikadi za jamii, utamaduni, mgawanyo wa majukumu kijinsia na uwezo. Kuambatana na madhumuni ya kwanza ambayo yalichunguza sura mbalimbali za ubabedume. Pili, mtafiti alichunguza athari za ubabedume kwa jinsia katika riwaya teule za Ben Mtobwa. Data ilikusanywa na kuchanganuliwa kutoka katika riwaya mbili teule mathalani, *Dar-es-Salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka*.

## 4.2 Sura mbalimbali za Ubabedume

Sehemu hii ilishughulikia lengo la kwanza la utafiti huu ambalo lilikuwa usawiri wa sura mbalimbali za ubabedume miongoni mwa wahusika katika riwaya Dar-es-Salaam Usiku na Pesa Zako Zinanuka. Mihimili ya nadharia ya ubabedume ilitumika katika uchanganuzi. Aina hizi za sura za ubabedume ni kama vile: sura za kitamaduni, sura ya dhakari, sura ya kiuchumi, sura ya kisikolojia, sura ya kimaumbile na sura ya kisiasa.

### 4.2.1 Sura ya Kitamaduni

Utamaduni ni mambo anayokubali mtu kuwa ni ya kweli na anayopaswa kuyaheshimu hasa katika dini au ni maoni ya moyo yanayofanya mtu awe na mkabala fulani juu ya kitu. Katika jamii nyingi mamlaka ya wanaume huhalalishwa kwa misingi ya kitamaduni. Wanaume huonekana wa thamani zaidi huku wanawake wakionekana viumbe dhaifu wasio na uwezo. Katika jamii nyingi hasa za Kiafrika mwanamume huwa ndiye kiongozi wa familia naye mwanamke kama msaidizi. Hivyo kijazanda mwanaume huwa kichwa cha familia naye mwanamke ndiye shingo ya kusaidia kichwa. Hivyo imani kama hizi huipa jinsia ya kiume uwezo mkuu huku mwanamke akiwa kiumbe dhaifu. Kulingana na Ponera (2014) utamaduni ni jumla ya matendo, mawazo na mifumo ya maisha na kiashiria cha utambulisho wa mtu katika jamii husika. Anaendelea kudai kuwa ni mkusanyiko wa mawazo na falsafa za watu, desturi, mila, siasa, uchumi na lugha. Ali (2018) naye anadai kuwa utamaduni ni jinsi binadamu anavyokabili maisha katika mazingira yake. Frosh na wenzake (2002) wanaendeleza msimamo na mtazamo wao kuhusu ubabedume kwa kusema kuwa wavulana na wanaume kwa ujumla hawajengi nafasi zao kutokana na ombwe tupu bali hujengwa na utamaduni wa jamii. Ni utamaduni wa jamii ambao husisitiza ushupavu na ushujaa katika utendaji wa majukumu yao katika jamii.

Hivyo basi, inajumuisha ujuzi, imani, maadili, sheria na desturi ambazo mtu anajipatia kama mwanajamii. Utamaduni wa jamii umekuwa asasi ambayo imemdhulumu mwanamke na hata kuleta mgawanyo wa majukumu kijinsia. Hali ambayo hata imebuni mpangilio wa kifamilia kingazi. Mwanamume anaachiwa majukumu ya kukimu na kulinda familia naye mwanamke akiachiwa masuala ya kinyumbani na malezi. Mfumo huu unafanya wanawake kuwa chini ya wanaume daima dawamu. Hivyo mwanamke amechukuliwa kama kiumbe duni kisicho na thamani. Kilonzo (2015) akirejelea Matei na Nyonje (2010) ambao wanadai kuwa yapo majukumu mbalimbali ya kijamii ambayo huhusishwa na jinsia mahususi. Wanaendelea kuamba kuwa katika jamii za Kiafrika mwanamume anatarajiwa kuwa jogoo au simba huku mwanamke akitarajiwa kudumisha heshima na uadilifu.

Katika riwaya ya *Dar-es-salaam Usiku* ukurasa wa 2 tunadokezewa kuhusu mhusika Rukia. Rukia alikuwa mtoto msichana aliyeachwa akiwa mtoto mchanga na mamake. Rukia akiwa tu limbukeni alionekana akipitapita kwenye sehemu za burudani akijaribu

kuteka wanaume ili ajipatie riziki. Hivyo basi, Rukia aliamini kuwa wanaume ndio waliokuwa wazalishaji mali. Hali ya kuwateka wanaume inasawiri vile wanaume huwa na ashiki ya kujihusisha na wanawake wengi. Rukia katika umri wake mdogo tunamtarajia awe anasoma lakini tunampata katika sehemu za burudani. Taswira tunayoona hapa ni kuwa utamaduni unafanya jinsia ya kike iamini kuwa wao wako katika ngazi ya pili katika familia. Ndiposa mhusika kama huyu anatembelea sehemu ya burudani ili awe kivutio cha wanaume. Haya yanasawiriwa na mihimili wa nadharia mathalani wa itikadi za jamii ambao huonyesha vile utawala wa mwanamume umehalalishwa katika ngazi za kijamii.

Katika riwaya hii pia tunaelezwa kuhusu wateja wa mamake Rukia walipokuja kumtafuta nyumbani kwao. Wateja hao walikuwa wa jinsia ya kiume na hata waliangalia Rukia kwa tamaa ya mahaba lakini walisita kwa sababu ya utoto wake. Taswira tunayoona hapa ni ya wanaume wakijihusisha na wanawake wengi. Mila na desturi zinakubali mwanamume mmoja kuwa na wanawake wengi. Jambo hili katika jamii nyingi huonekana kama ni ufanisi wa aina yake. Hata hivyo, wanawake walikosa kuruhusiwa kuwa na wanaume wengi kwani hili lilikuwa mwiko. Uwezo wa wanaume kujihusisha na wanawake wengi linatumiwa kudhalilisha wanawake. Jamii huamini kuwa bora mwanamume awe na uwezo wa kutunza wanawake, anaweza kuoa wengi. Wanawake nao wameamini suala hili kama uhalisia na ndiposa hawajali hata wakichukua nafasi yoyote katika orodha. Hivyo basi, usemi wa mwanamke katika mapenzi hukabiliwa na nguvu za kiume. Itikadi kama hizi za kibabedume humpa uwezo mwanamume hata kumtendea mwanamke unyama. Haya yalipambanuliwa kwa misingi ya mihimili ya nadharia yaani itikadi za jamii na utamaduni. Haya pia yanadhihirishwa katika riwaya io hiyo:

> *Wateja wa mama yake walipokuja kumtafuta na kumkuta yeye walimtazama kwa tamaa…. Wakaondoka zao huku wakimeza mate uk.3*

Tunaona kuwa wanaume walikuwa na ashiki ya mahusiano mengi na wasichana kama Rukia. Tamaa hii ilifanya wawe na tama ya mapenzi na wasichana nje ya ndoa. Hata hivyo tunaona waliogopa kujihusisha kimapenzi na wakembe kama mhusika Rukia.

Pia tunaelezwa kuwa kulikuwa na mwanamume mmoja aliyemfuata Rukia akiwa na kiu ya mapenzi. Alikuwa mwenyeji sana katika dunia ya starehe na matumizi. Alikuwa

na pesa za kutumia na ingebidi atafute wa kutumia naye. Alijiingiza katika raha za dunia hasa ulevini. Suala la kutafuta kipusa ili kujiburudisha linaonyesha vile wanaume wanapendezwa na vimada. Jinsia ya kiume inaonekana kuwa na moyo dhaifu sana katika masuala ya kimahaba. Sura ya kitamaduni inajitokeza hasa kutokana na wanaume kupenda kujihusisha na wanawake wengi. Wanawake wanajidhalilisha mbele ya waanaume na kujishusha hadhi. Wanawake huwa tuli mbele ya waume wao. Wanaume huwekwa mbele katika masuala ya kuongoza jamii. Nafasi ya mwanamke katika jamii huwa finyu sana. Hivyo mwanamke huwa anabaguliwa katika jamii yenye imani za ubabedume.

Mhusika Peterson alifurahia maisha ya anasa na vidosho mitaani. Peterson hakushinda bila kupata mwanamke wa nje. Peterson alikuwa ameoa Mama Sonny hata kama hakutosheka na penzi lake. Alijiingiza katika raha za ulimwengu na kuacha mkewe akiwa hayawani. Hali ya afya ya Mama Sonny hata ilidorora kwa sababu alitelekezwa na Peterson. Jambo lile linajitokeza hapa ni kuwa wanaume huwa na tamaa ya wanawake wengi lakini ndoa asilia huenda ikatelekezwa. Fauka ya hayo, uwezo wa kujihusisha na wanawake wengi unahusisha mwanamume kuwa kichwa cha familia akiwa mchumi nao wanawake wakiwa wasaidizi. Msukumo ambao hufanya wanawake kujihusisha na wanaume hata kama ni nje ya ndoa ni ari ya kutimiza mahitaji ya kiuchumi. Wahusika wa kiume kama Peterson walionekana kama watumizi katika maeneo ya burudani wakiwa na falsafa kuwa 'ponda raha kufa kwaja'. Utamaduni wa kijamii kuchukulia mwanamume kama kichwa cha familia naye mwanamke kama msaidizi unafanya mwanamke awe mtegemezi daima dawamu. Hivyo basi, Peterson alikuwa kielelezo cha wanaume watamaduni wanaosawiri uwezo wao kupitia matumizi ya hela nyingi mitaani. Wahusika kama Peterson aliwaona wanawake kama maua ya kurembesha na chombo cha burudani. Wanaume kama Peterson huwa hawatarajii chochote kama malipo kwa wanawake kwani wao sio wasaka riziki. Hali hii inathibitishwa kwa misingi ya mihimili ya itikadi za jamii na pia utamaduni. Haya yanasawiriwa na mhusika Peterson:

> *Huyu hakuwa msichana wake wa kwanza nje. Anaweza kuwa wa mia moja au mia na moja. Asingeweza kukumbuka idadi kamili. Uk. 15*

Katika kumbi za burudani ungepata meza yenye wanaume wanne na mwanamke mmoja. Tukio hili linaonyesha vile mwanamke alijidhalilisha na kuwa mtegemezi. Imani za kitamaduni zilifanya wanawake kuabudu wanaume.

Katika riwaya hii tunaona vile wahusika wa kike walivyokandamizwa na jamii iliyoamini ubabedume. Kwa mfano, Nunu alipopiga kelele kuhusu masaibu yake na kueleza ukweli, alisutwa, akatukanwa na kupigwa mithili ya punda. Fauka ya hayo, aliugua na hata kuwa na wazo la kutoroka. Hali hii inaonyesha vile mwanamke anadunishwa na imani za kitamaduni ambazo zimepitwa na wakati. Mwanamke anaonekana kama kiumbe ambaye ni msaliti. Mtazamo huu hasi unatumiwa na asasi za utamaduni kurudisha nyuma juhudi za wanawake kujikomboa kutoka kwa minyororo ya mfumo wa ubabedume. Hivyo basi wanawake wanabaki ngazi ya pili katika mpangilio wa kifamilia. Kasumba hii ya wanaume kuwa mwanamke hawezi kuongoza hukolezwa sana katika mawazo ya wanajamii na hata kuathiri jinsia ya kike vibaya. Zaidi ya hapo ni kuwa maamuzi ya wanawake huchukuliwa yenye dosari. Haya yanasawiriwa katika mhimili wa utamaduni.

> *Meza ile inao watu watano. Wanaume wanne mwanamke mmoja. Huyu mama yeye anaonyesha kuwa kalewa zaidi ya wenziwe. Au ni mwema zaidi yao.uk.25*

Wanawake wanasawiriwa kama viumbe dhaifu katika jamii. Hali hii ya kuona wanaume watano wakihudumia mwanamke mmoja inaonyesha hayo. Wanawake kujiingiza katika raha kunapalilia mahusiano yao na wanaume wengi.

Katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka,* Kandili walipokuwa wakisalimiana na Bon Kolo kwa simu alimuuliza kama amebadilika na kuwa mkewe. Kauli hii inaonyesha imani za kitamaduni zinavyodunisha jinsia ya kike. Mwanaume aliye na udhaifu anachukuliwa kama kiumbe duni na kufananishwa na mwanamke. Hapa kulingana na utamaduni mwanamke anaonekana kama kiumbe kisicho kikamilifu. Hata katika maandiko ya Bibilia mwanamke anasawiriwa kama kiumbe dhaifu anayeshawishika haraka mathalani Hawa katika shamba la Edeni. Kurejelewa kwa mwanamume na kuitwa ‘mwanamke’ kunadhalilisha mhusika huyo wa kiume.

Kandili alimwona Dora kuwa mzinifu aliyemsaliti na kujihusisha kimapenzi na mtu mwingine nje ya uhusiano wao. Kandili alikerwa na tukio hili kwani kulingana na utamaduni mwanamke hakuruhusiwa kujihusisha kimapenzi na wanaume wengi.

Utamaduni uo huo uliruhusu mwanamume kuwa na mahusiano na wanawake wengi. Jamii imetenga jinsia zote mbili huku jinsia ya kike ikigandamizwa. Mwanamke aliyejihusisha kimapenzi na wanaume wengi alirejelewa kwa jina la kuchukiza 'kahaba'.

Mwelekeo huu wa kutazama jinsia ya kike kama jinsia iliyo katika nafasi ya pili katika maamuzi hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hali hii huchangia katika kuweka mipaka mikubwa ya kingazi katika jamii. Mwanamume anayejihusisha na wanawake wengi hurejelewa kama mteja. Jamii inayoongozwa na mfumo wa kuumeni huhusisha uzinifu na jinsia ya kike huku jinsia ya kiume ikiangaziwa kwa mtazamo chanya. Wanawake huonekana kama viumbe duni ambao hustahili kuachiwa majukumu ya kinyumbani. Hili linasawiriwa na mhimili wa nadharia na ni dhana ya jinsia ya kiume kupewa hadhi ya juu. Haya yanaonyeshwa katika riwaya hii:

> *Yatazame mavazi yake! Utazame mwili wake! "Shauri ya umalaya," Kandili akanguruma tena, uk 78*

Mawazo pendwa katika jumuiya ya riwaya hizi ni kuwa mwanamume anaonekana mkamilifu huku wanawake wakiwa viumbe waovu. Hivyo jamii inaonekana kuwa inathamini sana wahusika wanaume huku wahusika wanawake wakibaguliwa na kudunishwa kwa misingi ya itikadi za kijamii. Jinsia ya kiume inaonekana ikipewa hadhi ya juu huku jinsia ya kike ikipewa hadhi ya chini. Kuna wakati Rukia, aliletwa na bwana fulani aliyemshughulikia kimapenzi bila kumwachia chochote. Mhusika kama huyu aliwadharau wanawake kwa hali zozote zile. Alikuwa na mtazamo sawa na wa Peterson ambaye alidunisha hata mkewe.

Rukia na Peterson walipokuwa na migogoro, Peterson alimwacha Rukia aendelee kuangua kilio bila hata kumtuliza. Hali hii inasawiri vile jamii yenye misingi ya kitamaduni inachukulia mwanamke kama kiumbe dhaifu. Rukia alionekana kama tambara mbovu mbele ya Peterson. Hata hivyo, wakati Peterson alikuwa na hamu ya mapenzi Rukia alimshughulikia kwa hali na mali. Picha inayojitokeza ni kuwa wanaume huthamini sana wanawake wakiwa na uchu wa mahaba lakini wakati hakuna wanawake wanadharauliwa.

Uchanganuzi huu umesawiri vile jamii imeweka misingi ya kitamaduni hasa katika mahusiano ya kimapenzi na majukumu ya kijinsia. Wanawake wamesawiriwa kama

viumbe ambao wako katika lindi la uhitaji na hivyo kuwa wategemezi kwa wanaume wasiowajali. Wanaume wanaonekana ndio waamuzi wa masuala ya kijamii kwani wanawake wanasawiriwa kama viumbe wasio wakamilifu. Pia kwa sababu ya kaida za kitamaduni wanaume wanaonekana kama wenye usemi mkubwa ikilinganishwa na wahusika wa jinsia ya kike. Hivyo utamaduni umetumika kuleta mgawanyo wa kijinsia katika jamii.

### 4.2.2 Sura ya dhakari

Dhakari ni kiungo cha mwili cha uume. Kiungo hiki huchukuliwa kuwa chenye nguvu. Urefu wa dhakari huwa na umaarufu kwa sababu huwa inachukuliwa kuwa chombo cha uwezo wa jinsia ya kiume. Umbo la dhakari la ubenuzi hukipa hiki kiungo nguvu, uthabiti na uwezo. Dhana ya ubabedume huhusishwa na kiungo cha dhakari. Kiungo cha dhakari hudhihirisha uwezo wa ubabedume hivyo kudhalilisha jinsia ya kike. Uwezo wa jinsia ya kiume huhusishwa na kiungo cha dhakari. Kulingana na maoni ya Riro (2015) akirejelea Brannon na David (1976) anadai kuwa mwenye dhakari hupewa hadhi ya juu. Hivyo basi huchukuliwa kuwa bora zaidi ya wale ambao hawana kiungo hiki. Anaendelea kusema kuwa binadamu anayezaliwa na kiungo hiki hukuzwa katika jamii kama raslimali yenye manufaa makubwa kwa jamii.

Mhusika Rukia katika *Dar-es-salaam Usiku* Uk.3 alidai kuwa hakuwa mgeni kwa lolote na aliwahi kushuhudia mama yake akitupwa chali kifudifudi. Aliendelea kusema kuwa aliogopa mamake akilia wakati wa ngono bila kufahamu ilikuwa raha. Raha hii ilichangiwa na upenyezi wa dhakari. Rukia alikuwa na umri mdogo sana kushuhudia mambo ya utu uzima. Mamake Rukia alikuwa amekubali kudhalilishwa na ubabedume. Uwezo wa dhakari hukadiriwa na utendakazi wake kwani mwanamume ambaye kiungo chake cha dhakari huwa na udhaifu huonekana ovyo. Fauka ya hayo, jamii hutukuza wanaume ambao hutumia kiungo cha dhakari kama ishara ya uwezo wao. Wanawake huwa wamekubali kutawaliwa na wanaume ambao huwa wanadhihirisha uwezo wao kupitia kiungo cha dhakari. Raha ambayo mamake Rukia alikuwa anashangilia ni upenyezi wa dhakari. Hali inaonyesha vile wanawake huwa wanakubali kutawaliwa na wanaume. Uwezo wa dhakari huwa kitambulisho cha ubabedume. Mhimili wa nadharia ya Ubabedume ambao ni itikadi za jamii ulisaidia katika uchanganuzi.

Rukia alidai kuwa hakuwa mgeni sana kwa mchezo huo. Wakiwa na mtoto wa jirani walifanya kama ‘mama’ kila alipoondoka mathalani, walijifungia chumbani. Hata kuna

siku alichelewa kurudi nyumbani na akanajisiwa na vijana wawili walevi. Hao walikuwa na kitu kikubwa, kitu kigumu na chenye joto kilichopenyeza kwa taabu katikati ya miguu yake. Uwezo wa dhakari kupenyeza katika mwili wa jinsia ya kike unaambatanishwa na ufanisi kwa mwanamume. Upenyezi huu wa dhakari unathaminiwa sana katika itikadi za jamii za Kiafrika. Utendakazi mwafaka wa kiungo cha dhakari unatumiwa kama kigezo cha kubainisha mwanamume halisi katika jamii. Pia upenyezi wa kiungo cha dhakari unatumiwa kugandamiza jinsia ya kike. Kiungo cha dhakari hutawazwa sana na huonekana cha umuhimu sana hasa kwa jinsia ya kiume. Mwanamume asiye na kiungo thabiti cha dhakari huonekana dhaifu na huonekana ovyo. Pia shahawa ambayo dhakari hutoa wakati wa kujamiana huonekana kama njia ya kumdhoofisha mwanamke. Uchanganuzi huu ulisaidiwa na mhimili wa nadharia ambao ni utamaduni. Nguzo hii husawiri vile ubabedume huendelezwa na mahitaji ya kitamaduni. Katika dondoo hii riwaya ya *Dar-es-Salaam Usiku* :

> *…Walimtia mweleka na kumfanyia 'kama mama'. Kwanza alihisi maumivu makali. Kisha maumivu yalipungua. Nafasi yake ikachukuliwa na faraja kubwa. Mtu wa pili alikuwa na kitu kikubwa na kigumu zaidi.( Uk. 4)*

Tunaelezwa kuwa Rukia alipofanya mapenzi na bwana fulani alihisi maumivu makali kutoka kichwani, mgongoni na katikati ya miguu yake. Alikuwa amechafuka kila upande. Hali hii inaonyesha athari ya dhakari kwa jinsia ya kike. Athari hii ya dhakari inaonekana hasi. Maumivu makali haya yanaambatanishwa na changamoto ambazo jinsia ya kike hupitia kwa kutawaliwa na jinsia ya kiume. Pia kuchafuka huku kwa mwili kunaweza kulinganishwa na kudhalilishwa kwa jinsia ya kike katika jamii inayotawaliwa na ubabedume. Jamii ambayo hutawaliwa na ubabedume hukandamiza jinsia ya kike. Rukia kama kiwakilishi cha jinsia ya kike anaonekana kama kiumbe duni mbele ya bwana huyu. Mwanamke anasawiriwa kama kiumbe dhaifu na cha burudani. Kiungo cha dhakari kinatumiwa kuburudisha wanaume na wanawake pia. Hili lipambanuliwa kwa msingi wa nguzo ya nadharia ya ubabedume mathalan utamaduni. Haya yanasawiriwa katika riwaya hii:

> *Alichokumbuka ni kuamka kesho yake, saa tatu za asubuhi, uchi kama kama alivyozaliwa, chali juu ya kitanda hicho. Alipojaribu kuinuka alihisi maumivu makali toka kichwani, mgongoni na katikati ya miguu yake. Uk.66*

Uwezo wa kiungo cha dhakari huwakilisha ushujaa wa kiume. Kiungo hiki kikikosa kuwajibika mwanamume huonekana kama mbumbumbu. Mwanamume huyu huonekana kama gumegume. Tunaelezwa kuwa kuna wakati Mama Sonny katika uk. 74 riwaya ya *Dar-es-salaam Usiku* alijaribu kumshika na kumgeuza Peterson. Rukia alikuwa amemaliza kila chembe ya ushujaa wa kuume. Hivyo Peterson alipoondoka alimwacha Mama Sonny amejilaza kifudifudi akilia. Hali hii ya kiungo cha uume kukosa kuwajibika katika upenyezi ilichukuliwa kama njia ya kushusha hadhi uwezo wa mwanamume. Uwajibikaji wa kiungo cha dhakari katika itikadi za jamii kiliashiria uwezo. Hivyo uwajibikaji wa dhakari katika itikadi za jamii uliweza kujenga au kubomoa hadhi ya mwanamume. Kiungo cha dhakari hurejelewa kwa majina tofauti katika jamii. Majina haya huwa yanaonyesha nguvu au uwezo kiungo hiki. Umbo lake pia hufanya wanajamii kukipa kiungo hiki ishara ya uwezo. Kulingana na nadharia ya Ubabedume hasa mhimili wa itikadi za jamii ambao huhalalisha utawala wa mwanamume kwa njia zozote zile.

Isitoshe, Nunu alionelea kuwa yeye ndiye alifanya Peter ajione mwanamume halisi. Nunu alimpapasa mzee Peter mpaka kiungo cha dhakari kikawa kimesimama kwa uthabiti. Kuwepo kwa uthabiti kwa kiungo cha dhakari kunahusishwa kwa ufanisi. Peter alisherehekea ushindi kwa sababu ya kiungo cha dhakari kuwa imara. Katika imani za jamii nyingi mwanamume ambaye huwa na udhaifu kwa kiungo cha dhakari huonekana hafifu. Mwanamume ambaye kiungo chake cha dhakari huwa imara hujiona bingwa katika jamii.

Dora alidai kuwa alikuwa na njaa kubwa ya kumsaidia Kandili. Jambo hili lilimpumbaza Dora mpaka akajikuta uchi huku uume wa Kandili ukifanya jambo la ajabu mwilini mwake. Jambo hili geni aliwahi kuliona katika picha za ufuska. Kitendo hiki cha Kandili kilimfariji na kusahaulisha mateso yote ya mwili na roho. Hii njaa kubwa na kiu ya kushiriki ngono ilimliwaza Kandili Maulana.

Wanawake wanaonekana kuipa dhakari uwezo kwa kuitukuza na pia kuitazama kama dawa mjaarabu kwa changamoto zao. Kiungo hiki cha dhakari kinaonekana kama kitulizo kwa mwili wa mwanamke. Imani za jinsia ya kike ni kuwa upenyezi wa kiungo cha dhakari ni njia ya kuwapa raha. Pia kiungo hiki cha dhakari huonekana kama ishara ya nguvu kwa mwanamume yeyote. Hili lilichambuliwa kwa msingi ya nadharia ya Uume.

Itikadi za kijamii zinakipa kiungo hiki cha dhakari nguvu. Dhana ya ubabedume huhusishwa na kiungo cha dhakari. Dhakari huchukuliwa kama uhai na ufu kwa mwanamume. Ukosefu wa uthabiti katika kiungo cha dhakari husababisha udhaifu wa mwanamume katika jamii. Upenyezi wa dhakari unathaminiwa sana kitamaduni na hutumiwa kudhulumu mwanamume.

### 4.2.3 Sura ya Kiuchumi

Uchumi ni mali iliyopatikana kutokana na amali za nchi au watu. Ni mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi. Katika jamii nyingi mwanamume huonekana kama mchumi huku mwanamke akiwa mtegemezi. Mwanamume huwa ndiye kitega uchumi cha familia huku wanawake wakiwa wategemezi wa kipato hicho. Hali hii imefanya jamii kugawa jamii kuwili. Jinsia ya kiume huwekwa katika tabaka la juu lenye uwezo huku wanawake wakiwekwa tabaka la chini mathalani la wanyonge walio dhaifu. Wanaume halisi hubainishwa kwa uwezo wao kiuchumi na usimamizi wa kifamilia. Katika jamii mbalimbali mwanamume halisi anafaa kuwa mwakilishi mwema na pia kiongozi bora mwenye kuajibika. Mwanamke aliyeolewa katika familia yenye ukwasi hufaharika sana.

Mtafiti aling'amua kuwa katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* Uk.63 Kandili Maulana alikuwa mkwasi sana. Wengi walinong'ona hata wasiomfahamu walidai kuwa alijaliwa kuwa tajiri. Alikuwa mfanyabiashara maarufu wa madini. Alikuwa na madini kama vile almasi, dhahabu, rubi na zingine nyingi. Ukwasi wake ungeweza kumridhisha, kumstarehesha na kumtosheleza. Uwezo wa kiuchumi wa Kandili unamuweka katika tabaka la wenye navyo. Uwezo huu wa kiuchumi pia ulikuwa kivutio cha wanawake kama vile akina Dora. Mali alizokuwa nazo zilimwezesha kuwatimizia mahitaji wanawake wengi. Hivyo basi, utajiri wake ulimwezesha kutegemewa na wanawake kama kitega uchumi chao. Imani kuwa uwezo wa kiuchumi ni kivutio cha wanawake hufanya wanaume kuwa wazinifu.

Mali nyingi katika jinsia ya kiume huwageuza baadhi yao na kuwa wakware na hivyo kuyumbisha mikataba ya ndoa. Hii inasawiri sura ya kiuchumi katika ubabedume. Katika riwaya ya *Dar-es-salaam Usiku* Uk.27, Rukia aliona kuwa Peterson alimpotezea sherehe zake siku tatu na kumwacha mikono mitupu baada ya kushiriki ngono. Kulingana naye kitendo hiki hakikuwa cha kiungwana. Mwanamume anaonekana kama ndiye mmiliki wa nyenzo za uzalishaji mali huku wanawake wakiwa wahitaji.

Wahusika kama Peterson wanatumia ukwasi wao visivyo kwa kuwateka na kuwanasa wasichana mbalimbali ili kushiriki ngono. Itikadi ya wanawake ni kugawana na wanaume ukwasi wao wa mali. Hata hivyo, baadhi ya wanaume walikuwa barakala na walitumia ukwasi wao visivyo. Wahusika kama Peterson walitumia uwezo wao wa mali vibaya wa kudhalilisha wahusika wa kike. Hata wakati Rukia alipokosa hela kutoka kwa Peterson aliona kama ni dhuluma. Katika sura ya kiuchumi, wanaume hasa wakwasi wanatumia uwezo wao kuteka wahusika wa kike kupitia mahaba. Hivyo basi uwezo wa kiuchumi wa wanaume unatumiwa kuendeleza ubabedume. Hili linawiana na vile nguzo ya utamaduni katika nadharia ya Ubabedume inavyosawiri.

Wanawake pia nao walikuwa na nafasi ya kuwateka wanaume kupitia miili yao. Wanawake walijua kutumia mavazi na miili yao kuteka wanaume waliokuwa na uwezo mkubwa wa kiuchumi. Rukia alipopewa dhahabu na bwana fulani alipanga vile angetumia mwili wake kumpa shukrani. Wanaume walitumia uwezo wao wa kiuchumi kuwatunza wahusika wa jinsia ya kike baada ya kushiriki mapenzi nao. Mpangilio wa kingazi unajitokeza katika jamii kutokana na wanaume kumiliki nyenzo za uzalishaji mali huku wanawake wakiwa ngazi ya wategemezi.

Wanaume ambao hawakuwa na uwezo mzuri wa kiuchumi walionekana wanyonge. Imani ya wahusika wa kike ilikuwa ni kujihusisha na wanaume waliokuwa mamwinyi. Mwanamume ambaye hakuwa anaeelewa haraka Rukia alikesha naye usiku kucha na kuteketeza pesa zake. Hivyo Rukia alijifanya mjanja na kumwibia mwanamume huyo. Hivyo wahusika wa jinsia ya kike waliamini uwezo wa kiuchumi wa wanaume. Mathalani wangefanya chochote kile ili kuwateka kihisia. Kulingana na itikadi za jamii mwanamume ambaye hakuwa na uwezo wa kiuchumi alionekana kiumbe duni.

Rukia alitembelea hoteli nyingi kubwa na hazingepita dakika tano kabla ya bia au nyama. Silaha kubwa ya wanaume kuteka vipusa ilikuwa pesa. Daima alichagua wanaume wake kwa makini. Rukia aliondokea kuwa malkia wa wazuri wote. Hata wengi walimpigania kwani kila mwanamume alimtamani. Rukia aliwalaghai pesa zao. Rukia alikuwa na msimamo kuwa hakutaka kuolewa mapema. Alitaka kuponda raha katika umri wake mdogo. Tunaona kuwa uwezo wa kiuchumi wa wanaume unakuwa kivutio cha wahusika wa kike.

Pia tunaona kuwa wahusika wa kike walitumia njia za utapeli kuwaibia na kuwahadaa wanaume. Wasichana wa mitaani kama akina Rukia hawakupenda kuolewa kwa sababu wangefungwa katika asasi ya ndoa na kukosa uhuru. Pia katika ndoa wasichana waliogopa kwa sababu waliona kama wangemilikiwa na mwanamume. Hali hii walionelea iliwakosesha nafasi ya kutalii dunia ya raha. Wahusika kama Rukia walikataa kufungwa katika minyororo ya ndoa. Wahusika wa kike kama Rukia waling'ang'ana kuwahi umwinyi waliokuwa nao wanaume. Hivyo basi, mwanamume alijitokeza kama ndiye mtafuta riziki naye mwanamke ndiye mlaji. Hili linatiliwa mizizi na nguzo ya utamaduni katika nadharia ya Ubabedume.

Hasira alidai kuwa ni watu wachache sana waliokuwa huru katika nchi husika. Hasira alidai kuwa walikuwa watumwa wa watu wachache sana. Walijitahidi katika harakati kumwaga damu ili kupata uhuru lakini mamwinyi walineemesha watoto na hawara wao. Hasira alidai kuwa wao na Hasara walikuwa kama punda wa kuwatumikia wengi. Waliishi kwa dhiki kubwa kama walalahoi. Hasira na Hasara wanasawiri picha ya mgawanyo wa matabaka ya kiuchumi kwa sababu ya umiliki wa mali. Wahusika kama hawa wasio na uwezo mkubwa wa kiuchumi walibaguliwa na kudhalilishwa sana. Matajiri walitumia uwezo wao wa kifedha kuwatumikisha mafalahi katika utumwa. Wanyonge wasio na uwezo wa kiuchumi waliachwa kama vijakazi.

Wahusika wa kike walifanya biashara haramu ili kujimudu na kujitajirisha. Wanawake kama Nunu waliacha mahusiano ya wanaume wasio na pesa kwani waliwatoroka kama ugonjwa wa tauni. Ilibainika kuwa Nunu angejenga nyumba, kununua gari na hata kuwaweka watumishi kwa pesa za wanaume. Jamii inajengwa na imani kuwa wanaume ni wenye mali. Wanaume ambao ni dhaifu kiuchumi walionekana kama tambara mbovu.

Wanawake nao waliwabagua wanaume kutokana na umiliki wa mali kiuchumi. Hivyo basi, wanaume wanabaki kuwa wachuma riziki wanaotegemewa na jamii. Wahusika wa jinsia ya kiume wenye pesa hudharau wasio nazo. Peterson ni mmoja wa wale walijiona mbele kwa sababu ya uwezo wa kiuchumi. Angetumia uwezo wake wa kifedha kukidhi njaa na uroho wake. Alitumia uwezo wake wa kiuchumi kutimiza ashiki yake ya mahaba. Pia uwezo huo wa kiuchumi ulifanya awe na majivuno ya aina yake. Uwezo wa kiuchumi ulifanya mwanamume kuwa na ubabedume kwani alitawala wasio na uwezo kiuchumi.

Katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* Kandili alijipata katika panda shuka aliponyang'anywa msichana na Bon Kolo. Bon Kolo alikuwa na uwezo mkubwa kiuchumi na Kandili hangeshindana naye. Hali hii ilimsumbua sana kimawazo. Uwezo wa kiuchumi ulionekana kama kigezo cha kuwanasa warembo wengi mitaani. Bon Kolo alikuwa kivutio cha wapenzi wengi kwa sababu ya uwezo wa kifedha. Haya yanajitokeza katika riwaya hii:

> *Kandili akaduwaa. Hakutarajia mabadiliko kama hayo. Mshangao uliongezeka alipomwona Maua akiinuka na kucheka kidogo kabla hajasema: Umempata darling? You are really a smart boy.'' Uk.5*

Kalulu alikabidhiwa kazi zenye wadhifa ambazo zilimwezesha kupata marupurupu ambayo hakuyapata katika majumba ya starehe kama wengine. Kalulu aliona kuwa alikuwa ametosheka kwani alikuwa na chochote kile ambacho mwanadamu angehitaji kama pesa au starehe. Uwezo wa kiuchumi huambatanishwa na kazi ambazo mhusika hufanya. Kazi ambazo ni za kiwango cha chini huonekana kama ni za wanyonge huku kazi za haiba kubwa zikionekana ni za mamwinyi. Kazi za hadhi ya juu hufanya mhusika kuwa na ubabedume huku akidhalilisha wale wa tabaka la chini. Hii inaonyesha sura ya kiuchumi ya mwanamume.

Maua alipenda sana Kandili kwa kuwa alikuwa na pesa za kutosha. Alionelea kuwa wangeishi raha mustarehe. Hata hivyo, Kandili hakutaka kuoa kwani alidai kuwa ndoa ingempotezea uhuru. Alidai kuwa hangeweza kustarehesha wanawake wengi. Alisema kuwa alistarehesha wanawake wengi huku wakimwita mpenzi lakini ilikuwa njia ya kumpumbaza. Hali ya Maua kupenda Kandili kwa sababu ya mali inasawiri itikadi za wanawake kuhusu wanaume. Wanawake wana imani kuwa wanaume ni wachumi wa mali. Hali hii ilifanya wanaume watambulikane na kuheshimiwa na wahusika wa kike. Pia wanaume wanatumia uwezo wao wa kifedha kuendeleza ubabedume.

Kwa mtazamo wa ubabedume, wanawake huwa viumbe dhaifu wasio na maana. Wanawake huonekana kama viumbe wategemezi katika jamii. Peterson alifikiria jinsi ya kumjengea mwanamke kahaba nyumba lakini jambo hili lilimpa mawazo changamano. Hali ya mwanamke kuitwa kahaba au malaya ni kudhalilisha jinsia hiyo. Peterson aliwaza na kujiona kuwa mpumbavu kwa kufuata viruka njia na kumwacha mkewe. Mwanaume hukandamiza wahusika wa kike kwa kuwaona kama viumbe duni.

Mwanamume mwenye uwezo mzuri kiuchumi hupata nafasi ya kuendeleza sera za ubabedume.

Katika itikadi nyingi, mwanamke huwa amekubali kuwa katika ngazi ya pili katika familia. Hali ya kukubali hufanya kuchukuliwa kama kiumbe duni. Tunaelezwa kuwa Mzee Mwarabu alihudumiwa kwa mahaba na Rukia. Huyu Mzee Mwarabu alimpa hela kidogo jambo lililomkasirisha Rukia. Hivyo mwanamke aliamini mwanamume ni mwenye uwezo kiuchumi na angefaa kumpa donge nono baada ya kumpa uhondo wa kimapenzi. Itikadi za jamii za kibabedume zilichukulia mwanamke kama chombo cha burudani. Mwanamume aliabudiwa sana katika jamii na kutukuzwa. Uwezo wao wa kiuchumi wa wanaume ulitumika kukandamiza wanawake.

Tunaelezwa kuwa Bon Kolo hakuwa mkono birika alitoa pesa za matumizi bila kuongea. Hata Maua alidai kuwa uhusiano wake na Bon ulikuwa sababu ya pesa. Maua alidai kuwa wanaume walikuwa wa aina tatu. Kundi lililopendwa kwa dhati, waliokuwa wazuri kwa sura na umbo na pia waliofuatwa kwa sababu ya uzito wa mifuko yao. Jinsia ya kike hivyo huhusisha jinsia ya kiume na umiliki wa mali. Mwanamume anaaminika katika jamii kama mzalishaji mali huku mwanamke akiwa mtegemezi.

Harakati za kujiinua kiuchumi hufanya wahusika kuendeleza uozo wa kijamii. Bon Kolo alitaka Kandili aingilie njama za ufisadi hasa katika mauzo ya dawa ya *Oxton*. Alijaribu kumshawishi kwa maneno matupu lakini hakukubali. Hivyo basi, alitumia hela nyingi alizokuwa nazo. Wanaume huendeleza ubabedume kupitia uwezo wa kiuchumi. Kandili kwa sababu ya uhitaji wake alishawishika. Mwanamume mwenye mali nyingi hutumia uwezo huo hata kuhadaa watu wengine. Mwanamume anatumia uwezo wake wa kiuchumi kumtawala mwanamke. Uwezo wa kiuchumi wa mhusika wa jinsia ya kiume unatumiwa kukandamiza jinsia ya kike. Kulingana na nadharia ya Ubabedume kuna mgawanyo wa majukumu kiuana. Mwanamume anaachiwa jukumu la kusaka riziki huku mwanamke akiwa mtumishi au msaidizi wa nyumbani. Mihimili ya itikadi za jamii, utamaduni na jinsia ya kiume kuwa na uwezo imesaidia katika uchanganuzi wa sura ya kiuchumi.

### 4.2.4 Sura ya kisaikolojia

Jinsia ya kiume huhusishwa na sifa kama vile ukakamavu na ujasiri. Kisaikolojia wavulana wanaweza kulinda wanyonge, wanaweza kukomboa, wenye msimamo thabiti

na wenye busara. Wanaume pia huhusishwa kwa mapenzi na wanawake wengi. Ulevi chakari pia huhusishwa zaidi na wanaume kuliko wanawake. Kulingana na Uchendu (2005), ubabedume katika vijana huhusishwa na maumbile, masuala ya kijamii na sifa za kisaikolojia. Kisaikolojia wanaume wanaweza kuleta ukombozi kwani wao ni jasiri. Frosh na wenzake (2002), wanadai kuwa sifa zingine ambazo husawiriwa na wanaume ni kuwa wakakamavu, walevi na wanaojihusisha katika mapenzi na wanawake wengi. Wanawake katika jamii wanatarajiwa kuwa watu watulivu, wapole, watiifu, wanyenyekevu na waaminifu kwa waume wao.

Tunaelezwa kuwa Wakenya walimfanya Rukia kama chombo duni kilichotendewa ustaarabu hadharani na ukatili sirini. Wanaume wanajitokeza kama viumbe wahuni waliotendea wasichana sampuli ya Rukia unyama. Kila mwanamume alihitaji kumtesa mwanamke ili kuonyesha ukakamavu wake. Mwanamume alimdunisha mhusika yeyote wa kike. Ujasiri wa wahusika wa kiume uliwapa uwezo wa kukandamiza jinsia ya kike. Kulingana na mhimili wa nadharia ya ubabedume ambao ni sifa angavu za mwanamume, jinsia ya kiume inafaa kuwa na ushujaa, ujasiri, ustahimilivu na kuwa huru.

Mwanamume anajitokeza kama mhusika mwenye ujasiri na ambaye haogopi. Tunaelezwa vile Kandili alikuwa anapambana na wadudu akingojea windo lake kwenye kiza kirefu katika riwaya ya *Dar-es-salaam Usiku*. Fauka ya hayo, hata alijaribu kunyatanyata gizani kufikia windo lake Bon Kolo Uk 91. Hulka hii ya kukabili windo lake bila kuogopa gizani inadhihirisha ujasiri unaosawiri ubabedume.

Bon Kolo alikuwa mwenye sifa nyingi zilizomfanya kuwa mashuhuri. Alijulikana sana kwa matumizi na hakuna aliyemzidi katika starehe. Jina lake lilikuwa maarufu katika hoteli za kifahari na sahihi yake ilipatikana katika vitabu vya wageni. Fauka ya hayo, aliandamana na wasichana wazuri wengi. Hivyo hakuhurumia noti yake katika matumizi. Mhusika huyu alihusishwa na starehe nyingi na wanawake wengi hali ambayo ilidhihirisha ubabedume. Mali nyingi ambazo wanaume humiliki wakati mwingine huyumbisha mikataba ya ndoa zao. Fauka ya hayo, unyenyekevu wa mwanamke ukilinganishwa na ukakamavu wa wanaume hufanya wanawake kujazwa woga na hivyo kudunishwa.

Ubabedume wakati mwingine hufanya wahusika wa kiume kufanya vitendo vya maovu. Ujasiri wa wanaume hugeuza wahusika hao na kutenda vitendo vya njama za ufisadi. Kandili alikubali kujihusisha katika njama za ufisadi kwani rohoni alijiambia hana hiari. Hivyo aliendelea kuwadhulumu wananchi bila kuwa na hisia za utu. Alihisi kama alikuwa akifanya dhambi kubwa lakini fikra za utu za kujali wengine zilitoweka. Yeye aliona kama alikuwa na nyota ya jaha kwani alipokea maelfu ya pesa. Alionekana mwenye falsafa kuwa uoga ni teke liwezalo kufukuza bahati. Kandili alikosa utu na kuwahini wengine haki zao za kibinadamu. Hulka kama hizi za Kandili zinaonyesha alikuwa mkakamavu kwani alikosa kuogopa chochote. Kupitia vitendo vyake vya kukiuka haki za kibinadamu tunaona vile ubabedume unaweza kukithiri katika jamii. Hili pia linasawiriwa na mhimili wa nadharia ya Ubabedume. Hizi ni zile sifa angavu za mhusika wa jinsia ya kiume.

Utamaduni wa Kiafrika hutambua uwezo wa mwanamume kumrai mwanamke kimapenzi. Mwanamume hupewa hadhi ya juu katika harakati za kuendeleza mapenzi. Mali nyingi za wanaume wakati mwingine huwafanya kuwa wazinifu. Hali ya mwanamume kuhusishwa na wanawake wengi huwa imehalalishwa katika jamii. Kandili Maulana alikuwa na safari nyingi za ughaibuni. Huko ng’ambo alishughulikia mambo ya kibiashara na kujistarehesha na wasichana wa kizungu.

Hawa viumbe inasemekana walikuwa muhali kupatikana. Hivyo walikuwa wameadimika sana. Hulka ya Kandili kujistarehesha na wasichana wengi inaendeleza ubabedume. Wanaume kama hawa wanajihusisha katika anasa za dunia na kufurahia mambo yasiyo na mwelekeo. Hivyo katika misingi hii wanawake wanakuwa viumbe wanaodhulumiwa na dhulumati.

Pia tunaambiwa kuwa Nunu aliolewa na mzee aliyemzidi umri kwa zaidi ya miaka sitini na mitano. Pia huyu mzee alikuwa na wanawake wengine watano. Mzee huyu alikuwa katili hivyo Nunu aliandamwa na kila aina ya taabu katika asasi ya ndoa. Wakati wa usiku, mume wa Nunu alimtesa na kumpapasa huku akimwita ‘malaya’. Mchana wasichana wa yule mzee walimsengenya Nunu bila sababu (uk 169). Fauka ya hayo, wageni waliofika kwa mzee walimwangalia kwa jicho la tamaa.

Zaidi ya hayo, Nunu alipopiga kelele na kuelezea ukweli alisutwa, akatukanwa na kupigwa kama mnyama. Vitendo hivi vinaonyesha mwanaume kama kiumbe katili. Pia

wanawake wanachukuliwa kama viumbe wasio na hisia na wasiofahamu haki zao. Kuwadhulumu wanawake na kuwaona kama hayawani ni kukiuka haki zao za kibinadamu. Wanawake wanaonekana kama wasio na usemi kama inavyosawiriwa na unyama anaotendewa Nunu. Vitendo vya wanawake kupigwa, kutukanwa na kudharauliwa vinaendelezwa na jinsia ya kiume. Pia tunaona vile huyu mzee alivyokuwa na wanawake wengine watano kama njia ya ufanisi. Uwezo wa wanaume kuwa na wanawake wengi ni itikadi inayotazamwa kwa jicho la utajiri. Mwanamume kama huyu huheshimika kwa kupewa hadhi ya juu kuliko wanaume wenye mke mmoja. Hili linadhihirika katika mhimili wa utamaduni katika nadharia ya Ubabedume.

Ubabedume huanzia utotoni. Makuzi ya ubabedume huendelezwa hadi katika umri wa utu uzima. Vijana katika ujana wao hufanya majaribio mengi katika harakati za kuonyesha ubabedume. Tunaelezwa kuwa Kandili alikuwa anasoma kidato cha tatu alipopendana na Dora binti mmoja wa walimu wake. Msichana huyu alikuwa kivutio kwake. Dora alijitoa kimwili kwa Kandili. Baadaye alitambua kuwa alikuwa amepachikwa mimba. Dora aliacha shule baada ya kujulikana alikuwa na mimba. Tamaa ya mapenzi ya vijana kama Kandili inasababisha madhila kwa Dora. Jamii nayo inaonekana kana kwamba inabagua watoto kijinsia kwani Dora alifukuzwa shuleni. Mfumo wa uumeni unakandamiza mwanamke huku mwanamume akikwezwa.

Bon Kolo alidai kuwa hakuwa amemwona Maua kwa muda wa siku tatu. Alimfanyia mzaha kwa kudai kuwa alikuwa amemteka na pia kumwazima. Naye Kandili alidai kuwa hakumpenda malaya kama yule kwani ni tamaa na uroho zilimfanya amkubali. Wanaume wanadhalilisha wanawake na hata kuwatukana kwa majina mabaya. Jina la malaya linakandamiza jinsia ya kike kwani wanaonekana kama viumbe wasio na thamani. Pia kauli ya Kandili kuazima Maua kwa wengine ni mtazamo hasi kwa jinsia ya kiume kwa kike. Hali hii inaonyesha mwanamke amedharauliwa katika jamii. Uwezo wa jinsia ya kiume unampa uhuru hata wa kumiliki mhusika wa kike. Tamaa ya mapenzi hasa kwa kujihusisha na wanawake wengi inasawiri maenezi ya ubabedume. Mwanamke anaachwa kama kiumbe ambaye hana usemi katika jamii. Mwanamume hivyo basi anajitokeza kama mtu wa hadhi ya juu huku mwanamke akisawiriwa kama mtu wa hadhi ya chini.

Kulingana na imani za ubabedume mwanamke humilikiwa na mwanamume. Pia mwanamke huonekana kama chombo cha burudani kwa mwanamume. Wanaume

huamini kuwa mwanamke ni kiburudisho chao. Ndiposa Bon Kolo alipomuuliza Kandili kama alikusudia kumwoa Maua, Bon alidai kuwa Maua alikuwa tunu ya Mola kwa makapera. Hivyo aliamini kuwa Maua 'malaya' aliyepatikana kwa urahisi kwani hakuwa amefungwa katika minyororo ya ndoa. Pia hakuwa amefungwa katika uhusiano na dume moja lenye wivu. Wanawake hapa wanachukuliwa kama maua ambayo uzuri wake hujitokeza kwa muda na baadaye hufifia. Mwanamke ambaye hajaolewa huonekana kama kiruka njia cha kutimiza ashiki wanaume.

Kamkanda alipolazwa hospitalini alienda kutembelewa na Maua. Daktari aliyekuwa akimhudumia Kamkanda alikumbuka kuwa msichana huyu hakuwa mgeni kwani alikuwa ameuona uso wake mara nyingi na kuutamani. Baadaye daktari aliandamana na Maua baada ya kuvutiwa naye. Walienda katika hoteli ndogo nadhifu walikofurahia chupa za bia na pia Maua akamhudumia daktari kimahaba. Daktari alitamani kila sehemu ya umbo hilo (Uk 56-57). Tunaelezwa kuwa daktari alikuwa na uchu wa kimapenzi hasa alipoona uchi wa Maua. Mwanamume anajitokeza kama kiumbe mpenda anasa na starehe. Pia daktari kama kiwakilishi cha wanaume anafurahia kujihusisha na wanawake mitaani. Fauka ya hayo,wanaume wanabidhaaisha wanawake na kuwaona kama viumbe duni. Wanaume wanaposhiriki mapenzi na wanawake wengi huonekana kama mabingwa katika jamii husika. Hili linawiana na nadharia ya ubabedume chini ya mhimili wa sifa angavu za kiume.

Wanawake hujitokeza kama viumbe dhaifu wakati mwingine. Wao huchukuliwa kama wanyonge na hukosa msimamo thabiti. Kandili alikuwa kivutio cha wasichana. Kandili naye angepumbazwa na maumbo ya wanawake. Wakati mmoja Kandili alipumbazwa na umbo halisi la msichana fulani na hata akaliacha gari lake na kuanza kumfuata yule kipusa (uk 75). Hulka hii inaonyesha azma aliyokuwa nayo Kandili ya kutaka kumiliki wasichana wengi. Wanaume wenye ushawishi wa vidosho wengi huonekana wakiwa mibabe katika jamii. Wanaume katika hali hizi hudhalilisha jinsia ya kike na ndiposa Kandili bado alifurahia mahaba ya Dora ili kutimiza ashiki yake. Hata hivyo, wakati walikutana na Dora baada ya kumtelekeza alimwona akiwa wa hadhi ya chini. Kandili alidai kuwa ukahaba ulikuwa umemwadhibu. Kandili kama wanaume wengine alionyesha tamaa, uroho na ubinafsi.

Wanawake hupitia wakati mgumu maishani. Wanaume hujaribu kuonyesha nguvu zao kwa hali zozote zile. Wanawake hudharauliwa na kutusiwa sana. Tunaelezwa kuwa

Dora alikuwa na changamoto ya kuwaepuka vijana wa kiume waliokuwa wakimtamani. Tunaelezwa kuwa kuna mwanamume mmoja mroho aliyemfuata hadi nyumbani. Waroho kama hao walithubutu hadi kumwita mwenda wazimu na majina mengine machafu. Tabia hii ya kutusi wanawake ni njia ya kuonyesha nguvu za wanaume. Ndiposa hata Kandili alimrejelea Maua kama malaya. Jina hili linadunisha mwanamke na kuchukulia kama huwa anafanya vitendo vya uzinifu akiwa pekee yake. Wanaume hurejelewa kama wateja huku wanawake wakiitwa 'malaya' jina ambalo linadhalilisha. Hili linawiana na nguzo ya utamaduni.

Sifa mojawapo wa wanaume ni kupenda raha. Bon na Kandili walipenda starehe. Anasa zao zilihusisha unywaji wa pombe na kufurahisha warembo. Hulka hii ya wanaume ilisawiri sifa angavu za jinsia ya kiume. Hali hii ilionyesha uwezo kujistarehesha na wapenzi na pia ubwagiaji wa pombe. Wahusika hawa wawili walipendezwa na dunia ya raha isiyo na mipaka kwa mahusiano ya kimapenzi. Wanaume wanajitokeza kama viumbe ambao huchukulia utambulisho wa uwezo wao ni mahusiano mengi ya kuwateka wasichana wa mitaani. Pia wanaume wanajitokeza kama wahusika barakala wanaochukua nafasi adimu za udhaifu wa jinsia ya kike kuonyesha uwezo wao.

Wanaume hujitokeza kama wahusika wabinafsi. Wahusika hawa ambao hutawaliwa na ubabedume huwa hawakubali mwanamke kujihusisha na wanaume wengine. Mawazo pendwa katika jamii huwa mwanamume ni wa wanawake wengi huku mwanamke akitarajiwa kuwa wa mwanamume mmoja. Mawazo haya ya kijamii hutumiwa kudhalilisha wahusika wa kike. Peterson alipompata Rukia na mwanamume mwingine alipigwa na butwaa. Aliamini kuwa sasa Rukia alikuwa malaya. Alishindwa vile angemletea mwanamume mwingine mpaka akakasirika. Peterson anasawiriwa kama mhusika anayekandamiza jinsia ya kike kupitia kwa hulka yake ya kukasirishwa na Rukia. Matarajio ya jamii iliyotawaliwa na ubabedume ni kuhalalisha mtazamo kuwa jogoo huwa anahudumia koo wengi. Hali hii hudunisha wahusika wa kike. Kulingana na mhimili wa itikadi za jamii, uongozi wa mwanamume na hulka zake zimehalalishwa katika sehemu zake za maisha.

Nunu alijua tumaini la mtoto lilikuwa mbali sana ndipo alipolazimika kujivua hadhi kiasi kwa kushiriki mapenzi na mpishi Mzee Kautipe. Baada ya siku chache za mikutano ya siri dalili za uja uzito zilijitokeza. Vitendo hivi vya siri vilileta matokeo ya kuzaliwa kwa Peterson. Mzee Kautipe alikubali kushawishika na kumzalia Nunu mtoto.

Mzee Kautipe alionyesha ubabedume kupitia umahiri wake wa kusababisha uja uzito jambo ambalo Peter alikuwa ameshindwa. Kisaikolojia mhusika Peter alionyesha udhaifu na kuonyesha hakuwa mwanamume halisi. Mwanamume halisi hutarajiwa kuhudumia kimapenzi mkewe na hata kuwahudumia vimada wa nje.

Jinsia ya kiume huona wanawake kama vyombo vya burudani. Ushujaa na nguvu za wanaume huonekana kupitia mahusiano na huduma kwa wanawake wengi. Hata hivyo, hata baada ya wanaume kufurahia mahaba ya wahusika wa kike huwakejeli na kuwarejelea kama makahaba. Hii ni kwa sababu huwa wametimiza haja yao kimapenzi. Ndiposa Maua alidai kuwa Kandili alikuwa machachari kwa ngono jambo lililomfurahisha. Hata hivyo, baada ya hayo yote Kandili alidai kuwa wanawake hawakuwa 'watu'. Aliendelea kusema kuwa Maua alikuwa amenena maneno yale yale kwa mpinzani wake Bon Kolo. Hivyo aliwaona wanawake kama viumbe dhaifu wasiokubalika kuitwa watu. Kauli hii inaonyesha vile jamii kupitia kwa wanaume wanakandamiza jinsia ya kike.

Jinsia ya kike huonekana kama jinsia ambayo haiko kwenye ngazi za binadamu. Mienendo ya Kandili na Bon Kolo kufurahia na kujihusisha na wasichana wengi inasawiri ubabedume. Fauka ya hayo, Bon Kolo na Kandili wanafanyiana ubabedume kupitia kipute cha kunyang'anyana wasichana kama Maua. Katika harakati zao wanadunisha na kudharau wanawake.

Uzinifu mara nyingi huhusishwa na jinsia ya kike. Jamii huhusisha ukahaba zaidi na wahusika wa kike. Wanaume wanaoponda raha na kujihusisha na wanawake wengi huonekana masogora katika jamii. Wao hutambulikana huku wahusika wanaoshiriki mapenzi yayo hayo wakiitwa makahaba. Peterson alimwona Rukia kama muasherati mkubwa kulingana na muda alioishi duniani na elimu aliyopata mitaani. Pia aliamini kuwa mwanamke mzuri ni yule malaya mzuri. Mtazamo wa Peterson uliongozwa na wivu kufikiri kuwa Rukia angewavutia wanaume wengine ili wapate uhondo aliokuwa akifurahia. Hivyo Peterson alikuwa na mtazamo hasi kwa jinsia ya kike. Kulingana na nguzo ya utamaduni, ubabedume huendelezwa ili kuyatimiza mahitaji ya kimsingi.

Katika jamii za Kiafrika wanaume wanaoshiriki uzinifu hurejelea wahusika wa kike kama makahaba. Kinaya ni kuwa wanaume hao hao ndio hushiriki mahaba na vidosho wa kila aina. Mzee Kautipe alidai kuwa Nunu hakuwa mama wa kusifika. Hii ilitokana

na vitendo vya kujihusisha na wanaume wengi kimapenzi. Kinaya ni kuwa Nunu aliwahi kushiriki mapenzi na mzee Kautipe katika nyumba ya Peter. Nunu aliwavuta wafanyakazi hadi maliwatoni ili washiriki kimapenzi. Mwanamke alidhalilishwa kwa tuhuma za ukahaba huku mwanamume akiachwa bila hukumu. Imani ya wale huwa wanaendeleza ubabedume huwa wanawake ni viumbe dhaifu. Pia wanawake ndio wanajitokeza kama viumbe duni kwani wanashawishi wanaume kushiriki mahaba. Wanaume huwa na mtazamo kuwa mwanamke ni chombo cha mapenzi. Kwa mtazamo huu mwanamke anasawiriwa kama chombo cha kufurahisha jinsia ya kiume. Jambo hili huwa limehalalishwa katika jamii husika.

Wanaume wakati mwingine huonyesha utesi na adhabu kwa jinsia ya kike. Mara nyingi hili hutokea wakati mwanamume hutambua mwanamke hapendi kutulia na bwana mmoja. Hulka hii hutawaliwa na mawazo ya ubinafsi na pia udhibiti. Matamanio ya mwanamume ni kumiliki mwanamke kwa njia zozote zile.

Tunaelezwa kuhusu mume fulani alipoona uume wake hautoshelezi alimvizia Rukia alipolala na kumdidimiza chupa ya soda. Kuna mwingine alimhadaa kushiriki mapenzi kumbe alikuwa ameficha wanaume wengine watano. Vitendo hivi vya kihaini vinaonyesha udunishaji wa jinsia ya kike. Wanaume wanaonekana kudharau wahusika wa kike. Hali hii inaonyesha vile mwanamke anasawiriwa kama kiumbe duni kinachokandamizwa na jinsia ya kiume. Pia inaonekana kuwa mwanamke amefungwa katika ngome ya utegemezi na uhitaji.

Wahusika wa kiume ambao huwa hawaonyeshi sifa bainifu za kiume hudharauliwa na kuonekana kama walio na hulka za kike. Wanaume kama hawa hubaguliwa na pia hudunishwa na wanaume wenzao. Mitagusano yao na wahusika wenzao wa kiume huwa nadra kwani hushushwa hadhi. Ndiposa Hasira alidai kuwa aliwapenda watoto wenye roho ya kiume. Hivyo aligandamiza watoto waliosawiri udhaifu uliohusishwa na jinsia ya kike. Katika jamii nyingi za Kiafrika watoto wa kiume hutukuzwa na kuheshimiwa. Watoto hawa wa kiume hufanyiwa sherehe za ndovu kumla mwanawe wakilinganishwa na jinsia ya kike. Watoto wa kiume huhusishwa na sifa bainifu kama vile ushujaa, ukakamavu na pia ujasiri. Mtoto hata wa kike anayeonyesha sifa kama hizi husifiwa na hutambulikana. Hili linawiana na mhimili wa sifa angavu za kiume katika jamii.

Mwanamke katika jamii iliyotawaliwa na ubabedume huwa na nafasi chukivu na finyu katika maamuzi ya kijamii. Mwanamume huwa ndiye mwamuzi wa kila jambo. Mwanamke huwa hana usemi wowote katika jamii. Itikadi za kuumeni humtukuza mwanamume huku mwanamke akitwezwa. Mwanamke hukabiliwa na dhuluma nyingi kutoka kwa jinsia ya kiume. Mwanamke hubaki kiumbe kisicho na usemi. Mwanamke hufungwa katika utumwa wa kutumikia mwanamume. Bw. Peter hakutaka kusikia jina la mkewe Nunu katika riwaya ya *Dar-es-Salaam Usiku*. Hii ilitokana na tabia ya kusaliti penzi lao. Peter aliwabagua wanawake na kuwaona kama viumbe wasio na hadhi yoyote. Hii ni kutokana na hali kuwa jinsia ya kiume imepewa hadhi ya juu. Haya yanasawiriwa katika uk.80:

*Hakuwa mama wa kujivunia ... uk.80*

Mwanamke anasawiriwa kama tambara mbovu lililo na hadhi ya chini. Mwanamke anadhalilishwa sana na kupewa hadhi ya chini.

Hivyo kulingana na dondoo hii mwanamke anayejihusisha na wanaume wengi anaonekana kama mzinifu ilhali mwanamume anakosa hatia.

Mwanamke alijitokeza kama chombo cha kutimiza ashiki ya kimapenzi. Mwanamume alikuwa na uhuru wa kipekee hata wa kujihusisha na wanawake wengi. Mwanamke hakuwa na uhuru huo kwani alidhulumiwa vibaya. Gloria aliona kuwa mume wake hakumhitaji tena. Mapenzi yake yalitoweka kidogo kidogo yakawa yameisha kwani aliingilia uasherati. Hata wakati fulani alishindwa kumchangamsha kimapenzi bila mafanikio. Jambo hili lilikuwa kama tusi la mwisho kwa mwanamke. Peterson alishindwa kumtimizia mkewe mahitaji ya kimapenzi. Jambo hili lilipaliliwa kutokana na uasherati wake mpaka akatelekeza Gloria. Hivi kwamba Peterson alitamani aende kwa Rukia baada ya kutofautiana na Gloria. Peterson aliwadharau na kuwadhalilisha wanawake. Wanawake wanajitokeza kama vyombo vya kuhudumia wanaume.

Mwanamume amepewa uwezo katika jamii hivi kwamba mwanamke anaogopa kutomtimizia mahitaji. Ni kana kwamba mwanamke amejazwa uoga na hana usemi. Ndiposa tunaona Gloria akidorora kiafya baada ya kutelekezwa. Minyororo ya ubabe dume ilimfunga mwanamke katika maamuzi. Jamii imewapa wanaume hadhi ya juu kama pia inavyosawiriwa katika mhimili wa nadharia.

Suala la mwanamke kuonyesha uchovu huchukuliwa kama ubwete. Mwanamke hutarajiwa kuwa mchapa kazi aliye na bidii. Mwanamke anayesawiri uchovu katika masuala ya kinyumbani na kimahaba huonekana duni. Wanaume wengi wenye misimamo ya kibabe dume hutarajia kushughulikiwa na wanawake hata wakati hali zao za siha ni mbovu. Peterson alikuwa anadai kuwa Rukia hakustahili kuonyesha uchovu wowote kwani kuna wakati alilala na mabwana wanne. Mabaharia hao walimhudumia Rukia lakini baadaye walimtangaza katika sehemu za starehe. Mwanamke anajitokeza kama chombo cha kujifurahisha. Mwanamke anajitokeza kama mtegemezi katika jamii. Mwanamume anatumia ushujaa wake kushinikiza mwanamke amtimizie haja zake. Hivyo mwanamke anakosa kuhusishwa katika maamuzi kwani yeye anachukuliwa kama kiumbe tofauti.

Katika itikadi za Kiafrika mwanamume anaweza kuhudumia wanawake wengi. Hulka hii ya kujihusisha katika anasa za wasichana wengi huonekana kama umahiri. Uwezo wa mwanamume kudhibiti wasichana wengi huhusishwa na ufanisi. Hasira kama kiwakilishi cha wanaume alipendwa sana na wanawake. Kila mwanamke aliyepatana naye alionyesha dalili za kumpenda. Kila alipotupa mtego hakukosa kunasa. Wengi walianguka kitandani mwake walioolewa na wasioolewa.

Hali hii inaoonyesha vile Hasara alijihusisha na wanawake wengi kwa sababu ya mizizi ya ubabedume. Tunavyobaini ni kuwa itikadi za Kiafrika huthamini sana tabia ya kuwa na wanawake wengi. Jambo hili huonekana kama jambo la kifahari. Pia uwezo wa kuwa na wanawake wengi husawiri uwezo na hadhi ya juu katika jamii. Wanaume wenye uwezo wa kumiliki wake wengi husifika kwa umahiri wao. Hata hivyo, wanaume hawa hutarajiwa kukidhi mahitaji ya jamii yao husika.

Mwanamume asiyetimiza mahitaji yake ya kindoa huonekana dhaifu. Wanaume kama hawa hubaguliwa na kuonekana dhaifu. Mwanamke hutarajia mwanamume amtimizie mahitaji yake ya kingono. Ikiwa hili halitendeki mwanamume hata yeye hujiona dhaifu. Ushujaa na ukakamavu kupitia ubabedume huwa umetoweka. Ndiposa Rukia alidai kuwa hajazoea kulala na wanawake wenzake (uk 141). Jambo hilo lilimkasirisha Hasara mpaka akamwadhibu vikali baada ya matusi. Mwanamume anayekosa uwezo mzuri wa kuhudumia mwanamke kingono huonekana duni. Wakati mwingine hurejelewa kama wanawake. Usemi kama huu hutumiwa kudhalilisha jinsia ya kike. Naye mwanamume ambaye hujihusisha na wanawake wengi kimapenzi huonekana

kama mkamilifu. Mwanamume halisi ni yule huwa anatimizia mahitaji ya wanawake wengi kwa hali zozote zile.

Tamaa ya kumiliki wanawake wengi huleta msukumo kwa wanaume ili watimize haja zao. Wakati mwingine harakati hizi huleta hali ya ukinaifu kwa wanaume. Tandabelua hizi za kusaka wanawake wengi huwa na hatima. Tunaona kuwa Peterson alikuwa alikishawishi wanawake wengi kimahaba akiwa na azma ya kufanya ngono. Hata hivyo alikinaishwa na wanawake wazuri. Kabla ya kukinaishwa na wanawake wazuri hakuna wakati angekosa kujaribu bahati kwa mwanamke aliyepita mbele yake. Hulka hii ya kusaka wanawake wengi inahusishwa na ubabedume. Hili linathibitishwa na mhimili wa nadharia ya Ubabedume ambao ni itikadi za jamii.

Katika sehemu hii ya utafiti wetu ulibaini kuwa wanaume hujitokeza kama viumbe wakakamavu hali ambayo hufanya wanawake kuwaogopa. Zaidi ya hayo wanaume wanajitokeza kama viumbe wapenda raha na wenye busara katika maamuzi. Wanawake nao wanasawiriwa kama viumbe wanyonge wanaopatiwa nafasi finyu katika maamuzi ya kijamii. Pia itikadi za jamii za kuumeni zimeonekana kumkuza na kumtawaza mwanamume huku mwanamke akidhoofishwa kwa kunyimwa haki zake. Katika sura hii ya kisaikolojia uwezo wa mwanamume kumiliki wanawake wengi unatambuliwa na kuonekana kama kigezo cha ufanisi.

### 4.2.5 Sura ya Kimaumbile

Katika itikadi za Kiafrika mwanamume hufaa kuwa mwenye nguvu, sauti nzito na mwenye kufoka. Mwanamume hustahili kuwa na sauti ya kuogofya. Uchendu (2005), anadai kuwa kimaumbile wavulana wanastahili kuwa na sauti nzito inayoweza kufoka, mtindo maalum wa mavazi, upekee wa kimapenzi, sura ya kutisha na nywele fupi. Mwanamume kimaumbile huwa ameumbwa kama mtu mwenye nguvu na mwenye sauti nzito.

Wanaume wanajitokeza kama watu wenye nguvu na ujasiri ambao wanaweza kufanya vitendo vya kinyama. Sifa bainifu za wanaume kimaumbile zinawapa uwezo wa kufanya vitendo vya kiajabuajabu. Mtafiti alibaini kuwa Hasara alikuwa amepewa jukumu la kumtoa uhai Peterson. Hulka kama hii ya kumtoa mtu uhai ilihitaji nguvu na ujasiri wa aina yake.

Peterson alipoona Mzee Kautipe amekawia kumpa habari kuhusu mamake alimzaba kofi moja baada ya lingine. Peterson alifoka na kumfukuza Kautipe kwa sababu ya utovu wa adabu. Kitendo cha Peterson kumzaba kofi Kautipe kinahusishwa na nguvu za wanaume. Peterson alitumia nguvu zake baada ya kukasirika. Wanaume hutumia nguvu zao za kimaumbile kudhulumu wengine. Pia sauti ya kufoka ya Peterson inadhihirisha ubabedume katika jinsia ya kiume. Hili linasawiriwa katika nguzo ya sifa angavu za uwezo kiume. Peterson alionyesha maumbile yenye nguvu kwa kumchapa Mzee Kautipe:

> *Kautipe alilazimika kusita kwa kofi jingine, kali zaidi, ambalo lilitua barabara katika uso wake.uk 154*

Nguvu za kimaumbile wakati mwingine hufanya wanaume kuwa katili. Ukatili wa wanaume hufanya wao kudhalilisha hata wanaume wenzao. Ndiposa Nunu alichukia babake wa kambo hata kumtandika karibu kumuua. Nunu alimchukia babake huyo wa kambo kama alivyochukia ibilisi. Babake wa kambo alinguruma nyumbani na alikuwa zaidi ya muuaji. Mngurumo huu huambatanishwa na sauti nzito ya jinsia ya kiume. Babake Nunu alidhihirisha ubabedume kupitia sifa za kikatili. Mwanamume ambaye hukosa sifa hizi angavu za nguvu na sauti nzito huonekana dhaifu sana. Mwanamume anajitokeza kama kiumbe mwenye nguvu kimaumbile. Nguvu hizi zinatumika kama kitambulisho cha mwanamume halisi. Kupitia mapigo ya wanaume kwa wanawake maenezi ya ubabedume huendelezwa. Mwanamume ambaye huwa na nguvu za kumkomesha muhibu wake hutambulikana. Mambo haya huwa yamehalalishwa katika jamii kama inavyosawiriwa katika mhimili wa itikadi katika nadharia ubabedume,

Peterson mara nyingi alimfokea Rukia hasa kutokana na udadisi wa mahusiano ya nje na Hasara katika riwaya ya *Dar-es-Salaam Usiku* Uk 174-175. Hata alimtukana wakati mwingine na kumdhalilisha. Sauti hii nzito ya kufoka inatambulisha jinsia ya kiume na pia kuendeleza ubabedume. Utambulisho wa mwanamume huhusishwa na masuala kama sauti nzito ya kufoka. Wanawake huhusishwa na sauti hafifu na nyororo. Wanaume ambao huonyesha udhaifu wao kupitia nguvu zao hudharauliwa kwa kuhusishwa na wanawake. Jamii za Kiafrika hutambua nguvu za mwanamume kama kiongozi wa familia. Hutarajiwa kuonyesha uwezo wa kulinda himaya yake kupitia nguvu za kimaumbile. Katika mchezo wa mieleka wanaume wengi ambao hushinda

hutukuzwa sana. Mwanamume dhaifu kimaumbile huwa hatarini hata ya kunyang'anywa muhibu wake.

Wanaume pia hutumia ubabedume kudhalilisha wanaume wenzao. Wanaume wenye nguvu nyingi hukandamiza wale ambao hawana uwezo. Bon Kolo alikuwa akimdhalilisha Kandili na kumtusi akimrejelea kama kuku hafifu. Kumwita kuku hafifu ni njia ya kumkandamiza Kandili. Fauka ya hayo, kipigo ambacho baadhi ya wanaume hupokea hutokana na nguvu za kimaumbile za kiume. Nguvu hizi huwa ni za viwango tofauti na wale wenye nguvu zaidi huwa washindi. Kandili akiwa mmoja wa wale walipokea pigo nzito mpaka kuanguka kama mzoga. Bon na Kandili walifanyiana ubabe wakitaka kudhihirisha uwezo wao. Hulka ya Bon kumzaba Kandili ilidhihirisha nguvu kupitia maumbile ya wanaume.

Pia Bon alikuwa akimtukana Kandili ovyo ovyo kwani alimdhalilisha. Hulka hii ya Bon ilisawiri wanaume vile huwa wanaona wanaume wenzio kama chombo duni. Bon alionekana mwenye nguvu kimaumbile na pia kutamalaki kwa uwezo wake. Mwanamume alitarajiwa kuonyesha ujasiri hata wakati alikabili mambo yoyote mazito. Hili lilipambanuliwa kwa msingi wa mhimili wa sifa angavu za uwezo kiume. Nguvu za kimaumbile za wanaume wakati mwingine hutumiwa kwa njia hasi. Bon Kolo alikuwa akisimamia mali iliyokuwa ikipakiwa katika kiwanda cha Oxton. Wanaume sita wenye nguvu nao walikuwa wakifanya kazi kimyakimya na kwa uangalifu mkubwa kwenye kiza totoro. Bon Kolo alikuwa anahusika katika biashara haramu.

Kanda wa Kamkanda naye alitaka kufichua siri hii akiwa amejificha ndani ya magunia. Nguvu za kimaumbile za wanaume zinatumiwa kuendeleza uozo wa jamii. Biashara hii haramu iliwanyima nafasi watoto kupata dawa ya kuwatibu ugonjwa wa palala. Wanaume wanageuka kuwa mahaini kwa kudhulumu jamii hasa watoto.

Mwanamume asiye na usemi katika mahusiano ya kimapenzi au ndoa huonekana dhaifu au aliyetawaliwa. Wanaume wengi hutumia uwezo wao wa kiuchumi na nguvu za kimaumbile kuendeleza madhila kwa jinsia ya kike. Kandili alizoea kumfokea Dora akimuuliza ni kwa nini alimkimbia. Sauti hii imara ya kufoka huambatanishwa na wanaume. Wanaume kama hawa hutambulikana katika jamii na huonekana wakiwa wakakamavu. Mwanamume ambaye hukosa kufoka huonekana akiwa na ila. Sauti ya

kufoka huwa njia mojawapo ya kutambulisha mwanamume halisi. Sauti ya kufoka hutumiwa kudhihirisha ubabedume kama njia ya kudhibiti mwanamke.

Katika sura hii ya kimaumbile wanaume wanajitokeza kama viumbe wenye nguvu, wenye sauti za kufoka na jasiri. Sifa hizi za kimaumbile ndizo zinatumiwa kutambulisha sifa za mwanamume aliyekomaa. Hali inatumiwa kudhalilisha wanawake. Nguvu za wanaume pamoja na sauti nzito ya kufoka zimetumiwa kukandamiza wanawake na pia wanaume wanaochukuliwa dhaifu. Sifa hizi za kimaumbile huwa zimetambulikana katika jamii na kuhalalishwa. Kulingana na mhimili wa nadharia ya uwezo-kiume, kuna sifa angavu za uwezo wa kiume ambazo lazima mhusika wa kiume awe nazo kwani akikosa yeye huonekana gumegume.

### 4.2.6 Sura ya Kisiasa

Siasa ni mchakato ambao huendelezwa katika jamii ukiwa na azma ya kupata viongozi au watawala. Ni mfumo katika jamii ambao huhusisha uchaguzi wa watawala katika eneo fulani. Ondoro (2021) akimrejelea Adero (2005) anadai siasa ni dhana ambayo inatumiwa kuelezea mfumo wa kuendesha masuala yanayokumba jamii katika taifa fulani. Sura ya kisiasa inajitokeza hasa katika mahusiano ya watawala na watawaliwa. Siasa ni shughuli ambayo huzalisha viongozi wa kisiasa katika serikali au upinzani.

Suala la uongozi huwa ni tata kwani wanawake huwa hawaaminiki katika nafasi za uongozi palipo na wanaume. Mapendeleo haya ya uongozi huwa msingi katika jamii inayotawaliwa na ubabedume. Mali na uongozi huwa ni mambo mawili ambayo hupumbaza na kuleta athari hasi kwa wanaume. Kuna uhusiano wa karibu katika siasa na uwezo wa kiuchumi. Viongozi wenye uwezo mkubwa wa kiuchumi huwa na nafasi kubwa ya kujitokeza katika shughuli za kisiasa. Wanasiasa ndio huongoza nchi. Wanasiasa mara nyingi huwa na uwezo mkubwa wa kiuchumi. Watu wengine huamini kuwa pesa ndizo hutawala nchi. Wananchi pia huamini kuwa maneno hujaa hila, ujanja, unafiki na tamaa ya uongozi. Uwezo wa kiuchumi wa wanasiasa huwapa nafasi ya kuchaguliwa kama viongozi. Viongozi huonekana kama walinda mali ya umma. Siasa huandamana na uwezo wa kiuchumi wa mhusika. Viongozi huonekana kama watetezi wa haki za umma lakini wakati mwingine hugeuka na kuwa wafisadi na katili. Wanaume wanaoendeleza ubabedume huanza kwao nyumbani mpaka katika siasa za kitaifa. Hii ni kwa kuwa kuna mgawanyo wa majukumu kiuana.

*Wanasiasa wanaongoza nchi. Lakini wenye pesa wanaoitawala.(Uk 82)*

Wanasiasa wanatambuliwa kama viongozi wa taifa. Hata hivyo, wale wenye uwezo wa kiuchumi huongoza mamlaka ya taifa. Uongozi na uwezo wa kiuchumi ni mambo mawili yanayoambatana. Juhudi za jinsia ya kiume kutawala jinsia ya kike huendelezwa na taasubi zao za kiume kutoka nyumbani hadi uongozi wa kiserikali. Uhalisia wa kijamii hujitokeza wazi kwani wanawake hushikilia nafasi ndogo za uongozi ikilinganishwa na wanaume. Jambo hili linatokana na itikadi za jamii kama ilivyo katika nguzo ya nadharia ya Uwezo-uume.

Wanasiasa hutumia uwezo wao wa kisiasa kujijengea jina na pia sifa sufufu. Azma ya mwanasiasa huwa ni kunyakua madaraka. Uongozi mara nyingi katika jamii inayoamini ubabedume huwa umetengewa jinsia ya kiume. Wanasiasa wakati mwingine hutumia njia chafu kuwahi nyadhifa za uongozi. Tunaelezwa kuhusu mhusika Kalulu aliyeazimia kujijengea jina na kupata madaraka. Hivyo alianza harakati za kugombea ubunge wa wilaya. Kalulu alikuwa na elimu ya kutosha hivyo hakuwa na shaka vile angekabili wapiga kura. Alifahamu wapiga kura walihitaji ahadi hewa na sauti zenye mvuto. Almuradi alikuwa na pesa za kampeni hakuogopa.

Kalulu ni kiwakilishi cha wanasiasa ambao hutumia nafasi zao kujinyakulia uongozi. Mwanamume anatumia ubabedume kukabili vizingiti vyovyote vile ili kujinyakulia uongozi. Wanasiasa hutumia njia chafu kuhadaa wapiga kura. Pia waandishi wa habari wenye njaa huhongwa ili kuandika habari kwenye vyombo vya habari zilizojaa chuku.

Mafanikio ya mwanamume yeyote ni kuwahi nyadhifa kuu za uongozi. Mwanamume anayejiingiza katika ulingo wa kisiasa na kufanikiwa huonekana bingwa. Kalulu alidai kuwa mwanamume alihitaji mafanikio kupitia umaarufu wa kutosha. Kandili alikuwa na mali ya kutosha na alijiona kama mfalme. Mwanamume anasawiriwa kama kiumbe anayetaka kuonyesha uwezo kwa kutumia hela nyingi. Jamii nyingi za Kiafrika humtukuza mwanamume kupitia mila na desturi zao. Uongozi wa jinsia ya kiume katika nyadhifa za uongozi husifiwa. Katika uwanja wa kisiasa mwanamke ananyimwa haki zake na hivyo kukandamizwa. Siasa ni mojawapo ya vyombo vinavyotumiwa kumgandamiza mwanamke. Tunaona kuwa katika hali nyingi za kisiasa mwanamume anajitokeza kama mshindi hasa kutokana na uwezo wa kiuchumi na itikadi za kijamii. Kupitia utambulisho wa mwanamume kama kiongozi wa familia, uongozi wa wanaume

kisiasa huhalalishwa katika jamii. Nao wanawake hupigwa vita na kutusiwa katika harakati za kusaka uongozi. Hivyo basi, wanaume hutumia mikakati tofauti kusambaratisha kampeni za wanawake kufikia upeo wa utawala.

## 4.3 Athari za Ubabedume kwa Jinsia

Ubabedume huwa unaathiri jinsia zote mbili mathalani ya kiume na kike. Katika ukitaji wa mizizi ya ubabedume, jinsia zote huathirika hasa kwa njia hasi. Athari hizi huchangia katika ukandamizaji wa jinsia husika. Pia maenezi ya ubabedume huleta mgawanyo wa kijinsia na utengano. Matabaka mawili huibuka katika jamii hasa jinsia ya kiume ikiwa katika tabaka la wenye navyo nayo jinsia ya kike ikiwa tabaka la wasio navyo. Athari za ubabedume katika jinsia huwa kama vile ukahaba, dhuluma za kijinsia, utabaka wa kijinsia, usaliti, ubaguzi wa kijinsia, utepetevu, utapeli, anasa na pia unafiki.

### 4.3.1 Ukahaba

Suala la kuelezea ukahaba huwa tata sana. Ufafanuzi wake hutegemea elimu na mtazamo wa mtu. Katika jamii nyingi hasa za Kiafrika, ukahaba huhusishwa na jinsia ya kike. Kahaba hurejelewa kama mhusika wa kike ambaye hudhamiria kushiriki ngono ili apate mapato ya kujimudu kimaisha. Ukahaba huonekana kama unahusishwa na umaskini katika jamii.

Ukahaba huwa ni hulka ya mwanamke ambaye huwa na mahusiano mengi ya kingono na wanaume wengi. Nabea (2021) alipambanua wajibu wa makahaba katika uchumi wa kisiasa. Alidokeza kuwa makahaba hutumiwa kuendeleza njama za ufisadi. Hivyo basi, makahaba hawa husawiriwa kama viumbe ambao hutafuta mapato kutoka kwa mamwinyi. Wao hutumiwa na wakwasi kufanikisha maovu ya ufisadi. Ukahaba ni dhana ambayo hutumiwa kudhalilisha jinsia ya kike.

Wanawake ambao hujihusisha kimapenzi na wanaume wengi huitwa makahaba. Jina hili huwa linatumiwa kukandamiza jinsia ya kike kwani kisawe chake ni umalaya. Ukahaba huonekana ukiendelezwa na wahusika wa kike wenye mapato ya chini kama njia ya kujiinua kiuchumi. Azma ya makahaba ni kupata riziki baada ya kushiriki ngono na mwanamume. Katika riwaya ya *Dar-es-Salaam Usiku*, mamake Rukia alikuwa akijihusisha kimapenzi na wanaume wa kila aina. Tunaambiwa alikuwa amepatikana na bwana wa asili ya Kizungu. Baadaye alitoroka ili kutafuta ‘soko’ badala.

Baada ya mamake Rukia kutoroka, wateja wake wa kiume walikuja kumtafuta huku wakimezea mate. Hulka ya mamake Rukia kuhusishwa na wanaume wengi husawiriwa kama ukahaba.

Mamake Rukia alikuwa akizimbua riziki kupitia kushiriki ngono na wanaume wa kila aina. Wanaume hawarejelewi kama makahaba lakini hurejelewa kama wateja. Jamii huwa na mapendeleo kwa jinsia ya kiume kwani wanawake ndio huwa wanadhalilishwa kwa kuitwa makahaba, malaya au viruka njia. Mtazamo wa jamii ni kana kwamba wanawake hushiriki mapenzi wakiwa pekee yao. Je, katika jamii nani huanzisha mchakato wa mapenzi? Wanaume huwasha moto wa mapenzi na hivyo basi hawafai kupendelewa.

Miji mikuu na pia vitongoji duni huwa ni mazingira mahususi ya kuendeleza ukahaba. Miji mikuu huwa na watu wa matabaka yote na wakati mwingine siyo matabaka yote huweza kujitafutia riziki. Vitongoji duni katika miji na mashambani hupalilia kuwepo kwa mazingira mazuri ya kuendeleza ukahaba. Suala la uhitaji na utegemezi hufanya wahusika wengi wa kike kushiriki ukahaba. Ukahaba huu siyo azma ya kushiriki ngono tu lakini lengo kuu ni kusaka tonge. Tunaelezwa kuhusu jiji la Dar-es-Salaam kulikokuwa na majumba ya sinema yaliyotumika kustarehesha watu. Tunaambiwa makahaba walikuwa wakijiuza huko mitaani na katika mabaa. Tabia ya msichana kujihusisha kimapenzi na wanaume wengi husawiriwa kama ukahaba. Hata hivyo, hali ni tofauti kwa mwanamume ambaye hujihusisha na wanawake wengi. Yeye huonekana kama mteja au mhudumu. Itikadi za jamii humpendelea mwanamume katika hali zote. Makahaba hufanya vitendo vyao siyo kwa mapenzi lakini ni msukumo wa gharama ya maisha. Makahaba hata katika jamii huchukuliwa kama wahalifu na hukamatwa bila hatia yoyote. Haya yanasawiriwa katika riwaya hii:

> *Hali kadhalika malaya walikuwa wakijiuza huko na huko katika mitaa na mabaa… (uk 20)*

Wanaume hujaribu kupigania wanawake makahaba mitaani. Msukumo wao huwa ni urembo wao. Makahaba nao huwa wanavutiwa na mabwanyenye wenye uwezo wa kiuchumi. Tunaelezwa vile Rukia aliandamwa na wanaume wengi katika mji wa Mwanza.

Hata wengine walimpigania. Hata wakati fulani kuna mwanamume mmoja alimtukana na kujaribu kumpiga. Hata alipohamia mji wa Arusha, Rukia aliendelea kuwalaghai na kuwakamua pesa wanaume. Hivyo Rukia aliendeleza ukahaba wake kupitia kushiriki ngono hivyo kupata kipato. Wanaume nao wanaonekana kama wenye kuendeleza uwezo wao kwa kushiriki mapenzi na makahaba wengi.

Uwezo wa kiuchumi wa mhusika wa kiume humpa kipao mbele katika kuwahi wasichana makahaba. Tunaelezea kuwa Rukia alikuwa anatumia njia zozote kupata pesa kutoka kwa wanaume walioshiriki mapenzi nao. Rukia alitumia hila na ujanja kushawishi wanaume wampe fedha. Rukia anaendeleza ukahaba kwa kutumia mwili wake kupata pesa kutoka kwa wanaume. Wanaume wengi huwa wanataka kumiliki kahaba mmoja jambo ambalo huwa ngumu katika michakato ya kijamii. Hata hivyo, suala kuu linaloibuka ni je, kuna wanaume makahaba? Au kwa kuwa wanaume hawapokei hela zozote kutoka kwa wahusika wa kike huo sio ukahaba?

Wasichana makahaba hasa katika ujana wao huonekana wakiwa bora zaidi. Wale waliokonga huwa si kivutio cha wanaume. Wasichana hawa huteka wanaume wenye mihela. Kila mwanamume hujaribu kung'ang'ania nafasi ya kuwahi wasichana hawa. Rukia alikuwa zaidi ya ua nzuri. Vitendo vyake na harakati za kuendeleza ngono zilikuwa za kupigiwa mfano. Rukia alikuwa na shabaha ya kumstarehesha Peterson. Rukia angejitolea kwa hali na mali kwa Peterson ili amfurahishe. Peterson alimwona Rukia kama kahaba tupu, umalaya ulitoka nyweleni hadi kuchani. Hii inaonyesha vile Rukia alikuwa kupindukia. Hata hivyo, Peterson hata ndiye aliyezidisha uasherati kwani alikuwa na mazoea ya kuchukua wanawake wengi mitaani. Peterson naye alitumia uwezo wake kiuchumi kuwateka wanawake wengi akiwemo Rukia. Wanawake hasa makahaba walivutiwa na uwezo wake wa kiuchumi.

Wasichana makahaba huwa dawa mjaarabu kwa wanaume ambao ndoa zao huwa zinayumbayumba. Pia wasichana hawa huwa kama chombo cha burudani kwa wanaume hasa nje ya ndoa. Uwezo wa kushiriki ngono na wasichana wengi huonekana kama ushujaa katika jamii. Wakati mwingine makahaba huwafurahisha wanaume zaidi ya vile wanavyopokea mapenzi katika ndoa zao. Grace alikuwa na azma ya kumpokonya Mama Sonny mume. Hivyo alitumia nafasi ambayo ndoa ya Peterson na Mama Sonny ilipokuwa inalegalega.

Peterson alikuwa na tabia ya kushiriki mapenzi nje ya ndoa na hivyo kuendeleza ukahaba. Ukahaba huwa unashamiri hasa wakati kuna migogoro ya kifamilia. Wanaume hupata nafasi adimu ya kustareheshwa. Hata hivyo, ukahaba hufanya mwanamume kukosa kuajibika katika ndoa yake asilia.

> *Grace akijua hivyo alizidisha mahaba katika macho na sauti yake (uk 110)*

Hulka ya ukahaba hutumiwa kudunisha wanawake. Wanawake hutusiwa na kudharauliwa kwa kuitwa makahaba. Kauli hii ya kuitwa wanawake makahaba hujumlishwa kwa jinsia ya kike yote. Nunu hakuwa anatambulishwa kwa vile alikuwa kahaba. Alikuwa akijistarehesha na wanaume wengi. Mzee Peter hakutaka kusikia jina hilo likitajwa katika nyumba yake kwa sababu ya uasherati. Wanaume walifurahia mahaba ya akina Nunu huku wakitosheleza ashiki yao. Nunu alidunishwa na hata kukosa kutambuliwa katika jamii. Alionekana kama kiumbe kisicho na hadhi yoyote. Ukahaba wake ulifanya hata mumewe awe na hisia hasi kwake. Wakati mwingine azma ya mwanamke kupata mtoto katika ndoa humsukuma nje ya ndoa. Mume wakati anaposhindwa kutimiza mahitaji ya ndoa huonekana kama gumegume. Hali hii hufanya wanawake kuwa waasherati. Mwanamke ambaye hushiriki uasherati hubaguliwa katika jamii na huonekana ovyo kama tunavyotazama katika riwaya:

> *Tatizo lilikuwa mama. Mwanamke akaamua kuwa malaya. Aliwazoea wengi, akajistarehesha nao kwa namna mbalimbali. (uk 114)*

Jina hili malaya ni jina la kudharau na kudunisha wanawake. Kujihusisha kimapenzi kwa wanaume kwa wanawake wengi ni kana kwamba ni jambo lililohalalishwa. Hata hivyo, mwanamke anayejihusisha na wanaume wengi hudunishwa kwa kuitwa kahaba au malaya au kibiriti ngoma.

Wahusika kama Rukia walilazimika kulala na mabaharia wanne. Aliwahimili wote kimapenzi japo alihisi maumivu. Rukia alikuwa kivutio cha wengi. Tabia ya Rukia kushiriki mapenzi na wanaume wengi inasawiri ukahaba. Ukahaba hutumiwa kushusha hadhi wahusika wa kike. Ufukara na hali ya kuporomoka uchumi husukuma wahusika wa kike katika lindi la ukahaba. Rukia kushiriki mapenzi na mabaharia wanne ni suala linasawiri kudorora kwa hadhi ya mtoto wa kike. Hata kauli kuwa Rukia alikuwa kivutio cha wengi inaonyesha maenezi ya kina ya ukahaba katika jamii. Hata hivyo,

tunaona wanaume baada ya kushiriki ngono na makahaba kama hawa huwatangaza na kuwadhalilisha.

Makahaba huweka ndoano kunasa wateja walio na mihela. Nia yao kuu huwa ni kujitajirisha na kujitosheleza kiuchumi. Tunaelezwa kuhusu mzee wa Kiarabu aliyevunja safari ya kwenda Pemba na kwenda kushiriki mahaba na Rukia katika nyumba za wageni. Mwarabu huyo tunaambiwa hata alikosa kutembea baada ya Rukia kumpa mirindimo usiku kucha ya mapenzi. Rukia alionyesha umahiri kwa kumhudumia mzee huyo wa Kiarabu. Hapa Rukia anajitokeza kama kahaba anayemhudumia mzee huyo. Tamaa ya mapenzi husukuma jinsia ya kiume kuendeleza ukahaba. Nao wahusika wa kike huonekana kama viumbe dhaifu wanaotumiwa vibaya. Rukia alishiriki mapenzi na mzee ambaye hawakuwa wanajuana. Wahusika wote wawili wanajidhalilisha sana. Rukia pia hakuwa wa mwanamume mmoja lakini alitumia urembo wake kunasa wengi hata akina Hasara.

Jamii huwa na itikadi zinazodhalilisha jinsia ya kike. Wahusika wa kike huonekana kama wakosefu hata wakati jinsia zote mbili huchangia dosari fulani. Ni kana kwamba jinsia ya kiume huwa jinsia teule isiyo na makosa yoyote. Mzee Kautipe alijihusisha kimapenzi na mamake Peterson. Kitendo hiki pamoja na hulka zingine zilifanya kurejelewa kama ‘mama ambaye hakuwa wa kujivunia’. Usemi huu unatumiwa kudunisha jinsia ya kike huku jinsia ya kike ikiwa huru. Ni kana kwamba Nunu alishiriki mapenzi akiwa pekee yake.

Wanawake hupokea dhuluma nyingi kutokana na vitendo vyao vya ukahaba. Wengi hutendewa unyama, dharau na hata udunishaji. Wengine hata hutiwa mbaroni baada ya kukamatwa na walinda usalama. Peterson alifurahia kula uroda na Rukia. Peterson alidai kuwa Rukia alikuwa kahaba mkubwa. Aliamini kuwa mwanamke mzuri ni malaya kupindukia na ndiposa alitelekeza Gloria na kukimbilia vimada wa nje. Hulka hii ya kupendelea wanawake wa nje inaendeleza ubabedume. Mwanamume ambaye huwa na uwezo wa kudhibiti wanawake wengi huonekana mahiri. Maua na Kandili mara nyingi walikuwa wakigombana. Kandili hakumpenda Maua kwani alimwona mvivu. Kandili kama wanaume wengine hakumweka rohoni. Aliamini mwili wake ulikuwa kivutio cha wanaume wengine.

Mwanamume huonea wivu mhusika wa kike hasa anapotambua ana uhusiano wa kando. Mtazamo huu hutawaliwa na wivu. Kauli kuwa mwanamume huwa hamweki muhibu wake rohoni ni tamko la kuonyesha unafiki wao. Unafiki huu hufanya wanaume wakitimiza haja zao huwatupa vimada kama Maua katika kaburi la sahau. Hivyo mwanamke kahaba hutumiwa kama gurudumu la akiba.

### 4.3.2 Dhuluma za Kijinsia

Dhuluma ni kitendo cha kumnyima mtu haki au stahiki yake kwa kumtendea maovu. Ni tendo la kufanya mambo yaliyo kinyume cha haki, uonevu, hiana au ukatili. Dhuluma za kijinsia huwa ni ukandamizaji unaondelezwa kwa wanaume na wanawake katika jamii. Kimani (2003) akimrejelea Johnston (2002) anabaini kuwa dhuluma ni maonevu ya kimwili, kijinsia, kihisia na matumizi ya lugha yanayotolewa kwa mtu kwa namna ambayo inamvunjia heshima na kumnyima haki zake za kibinadamu. Utamaduni huwa asasi moja ambayo hutumiwa kuendeleza dhuluma za kijamii. Pia asasi ya ndoa hutumiwa kuendeleza dhuluma za kijamii. Brinkman na wenzake (2016) wanadai kuwa dhuluma za kijinsia zimekuwa zikiendelea hasa kwa wanaume isipokuwa tafiti chache zimeangazia suala hili.

Jinsia ya kike mara nyingi hutendewa dhuluma na jinsia ya kiume. Pia jinsia ya kike huendeleza madhila kwa jinsia ya kiume. Mara nyingi katika jamii ya sasa dhuluma za kijinsia huendelezwa kuwili. Kupitia vitendo vya kikatili, matumizi ya lugha na kunyimwa kwa haki ni baadhi ya mambo ambayo hutumiwa kuendeleza dhuluma za kijinsia. Tunaelezwa kuhusu Rukia alivyobakwa na vijana wawili walevi katika riwaya ya Dar-es-Salaam Usiku. Ubakaji wa jinsia yoyote ile huchukuliwa kama dhuluma kwa jinsia husika. Ubakaji ni hulka ambayo inahusishwa na ukatili ambao huendelezwa kwa jinsia. Ubakaji wa Rukia unaonyesha vile jinsia ya kike hudhulumiwa. Suala la mapenzi huwa ni makubaliano ya wawili wamependanao. Ubakaji huu huweka kovu katika mwili wa mwathiriwa na hata wakati mwingine huleta msongo wa kimawazo. Waathiriwa hukosa kukubali matokeo ya kitendo cha ubakaji kwani huwa wameshinikizwa. Madhila kama haya husawiri vile jinsia ya kiume hutumia ubabedume kudhulumu jinsia ya kike. Haya yanasawiriwa katika riwaya hii teule:

> *Njiani alikutana na vijana wawili walevi. Walimtia mweleka na kumfanyia kama mama kwa zamu. Kitu kikubwa, kitu kigumu na chenye joto kilipenya kwa taabu katikati ya miguu yake (uk 6)*

Katika starehe za wanaume, suala la tamaa ya mapenzi hujitokeza. Wakati mwingine jinsia ya kiume hutumia ubabe wao kuendeleza mateso. Tunaelezwa kuhusu wanaume walivyojaribu kumtesa na kumwadhibu Rukia. Kuna yule alijaribu kumvizia Rukia kwa kumdidimizia chupa ya soda kama uume wake haukutosheleza. Hiki kilikuwa kitendo cha kihaini kwa jinsia ya kike.

Wanaume wanageuka kuwa wanyama na kuwaona wanawake kama vyombo duni. Fauka ya hayo, kuna yule angemlevya na kumletea mbwa wake au hata mwingine kumwandalia wanaume watano. Vitendo kama hivi vya kikatili vya kufanyiwa mapenzi na wanaume watano au kushiriki mapenzi na wanyama vinaonyesha dhuluma ya kijinsia. Huu ni ukandamizaji ambao umepitwa na wakati katika kipindi cha sasa.

Jukumu la kumtunza mke huwa ni la mume. Pia mke ndiye huwa anatunza mume wake. Mume ambaye hukosa kujukumika katika jamii huonekana ovyo. Pia vilevile mke ambaye hutelekeza mumewe husutwa sana na jamii. Mume ambaye hukosa kuangazia maslahi ya mkewe huwa hatambuliki katika jamii kwani huonyesha dosari. Mwanamume ambaye hukosa kuwajibikia mkewe husawiriwa kama ambaye anadhulumu jinsia ya kike. Peterson alikosa kumwajibikia mama Sonny baada ya kwenda mitaani kujistarehesha na akina Rukia. Tunaelezwa kuwa chakula kilimshinda, njaa ilimtesa na hamu ya kutunza mwili ikakosa. Na ilionekana kile kilichobaki ni talaka. Mateso aliyopitia mama Sonny yalitokana na dhuluma za kijinsia zilizoendelezwa na Peterson.

Katika tamaduni za Kiafrika mwanamke huwa hana usemi katika jamii. Mwanamke huwa kama mali iliyomilikiwa na mumewe. Hata huwa ni vigumu sana mwanamke kumwambia mumewe au mwandani kuwa amechoka. Wajibu wa mwanamke huwa ni kumtosheleza kihisia mumewe. Wanawake ambao hukosa kuwajibikia wanaume huchukuliwa katika jamii hukosa kutambuliwa. Kwa mwanamke wa sampuli ya Rukia ilikuwa mwiko kudai amechoka. Matarajio ya mwanamume yalikuwa ni kuhudumiwa kimahaba na wahusika kama Rukia bila kuonyesha dalili ya uchovu. Mwanamke pia alijidhalilisha na kujiona kama kiumbe duni.

Dhuluma za kijinsia hujisawiri kupitia ukatili unaondelezwa na jinsia ya kiume. Kupigwa, kuteswa, maonevu na kutusiwa ni baadhi ya ishara za dhuluma za kijinsia. Peterson alimzaba kofi mzee Kautipe aliposita katika harakati za kumwelezea kuhusu

mamake kwani alidaiwa hakuwa mama wa kujivunia. Kuzabwa kofi kwa mzee Kautipe kunasawiriwa vile hata jinsia ya kiume inaweza kuendeleza madhila haya kwa wenzao. Peterson anaonyesha ukatili kwa mzee Kautipe kwa kumdhulumu. Pia vile Nunu alidaiwa hakuwa 'mama wa kujivunia' inaonyesha kukandamizwa kwa jinsia ya kike.

Hulka ya Nunu kujihusisha kimapenzi na wanaume wengi ilisawiri kushushwa hadhi kwa mwanamke. Ni kana kwamba alishiriki mapenzi akiwa pekee yake. Mtazamo huu unaonyesha jamii vile hudhulumu jinsia ya kike. Katika maisha ya ndoa dhuluma za kijinsia huendelezwa sana. Wanaume hutumia uwezo wao wa kingazi katika jamii kuendeleza madhila kwa wenzi wao. Tunaelezwa vile Nunu aliandamwa na shida nyingi katika maisha ya ndoa. Aliteswa na bwanake na pia kumwita malaya. Pia wale wake wenza walimsengenya Nunu na kumchukia. Fauka ya hayo, walimwonea wivu. Nunu alipitia dhuluma hizi za kijinsia zilizoendelezwa na jinsia zote mbili. Dhuluma kama vile kusengenywa na chuki ziliendelezwa kwa Nunu. Pia wanawake waliendeleza kijicho. Ubabedume unatumiwa kuendeleza dhuluma kupitia mateso na taathira zingine. Katika mfumo wa jamii, dhuluma za kijinsia mara nyingi huwa zimekubalika. Utamaduni hasa wa Kiafrika humpa mwanamume nguvu nyingi hivi kwamba wakati mwingine hutumia mbinu hizi vibaya.

Mahusiano ya kimapenzi wakati mwingine huchangia dhuluma za kijinsia. Wanaume mara nyingi huwa wanashindana wao kwa wenyewe kusaka vidosho. Mashindano hayo hufanya wanaume kufanyiana ubabedume kwani hutaka kuonyesha usogora wao. Hata hivyo, vipute hivi huchangia dhuluma za kijinsia kwa jinsia zote mbili. Hapa washindani na wanaoshindaniwa huathirika kwa njia hasi. Tunaelezwa kuhusu mhusika Peterson alivyomtupia Hasara ngumi. Naye alivyojibu kwa makeke mpaka akayumba baada ya kutofautiana. Peterson aliendeleza ukatili kwa Hasara kupitia kumpiga ngumi.

Kupigwa ngumi kunasawiri mateso kwa wahusika kama Hasara wanaochukuliwa ni wa tabaka la chini. Naye Hasara alionyesha umahiri wake kupitia kujibu ngumi. Peterson hata alimtusi Hasara. Matumizi ya lugha chafu kama ya Peterson inasawiri vile wahusika wa jinsia mbalimbali wanaweza kudhulumiana kupitia semi zao. Semi ambazo hazina lugha ya maadili hutumiwa kudhalilisha wahusika kwa kuwadunisha. Hali kama hii inasawiriwa katika mahusiano ya Bon Kolo na Kandili katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka*. Tofauti zao zilikuwa zinaibuka kwa sababu ya ushindani wa mahaba ya mhusika Maua. Dhuluma za kijinsia zinaendelezwa na Bon Kolo kwa

Kandili. Hata Bon Kolo alidhihirisha dhuluma hizi kupitia kumzaba kofi Kandili. Dhuluma hizi za ndani kwa ndani ya jinsia moja zinachangia maenezi ya ubabedume.

Vijana wengi katika majaribio ya mapenzi hujikuta katika upashikaji wa mimba kiholela. Matokeo kama haya yanapotokea hali ya kulaumiana hujitokeza. Vijana wa kiume hata wakati mwingine hutorokea majukumu mapya. Wanaume mara nyingi hujaribu kuendeleza ubabedume kupitia kwa mahusiano na wanawake wengi. Dhuluma za kijinsia huendelezwa pale ambapo wahusika wa kike ni wanafunzi. Watoto hawa wa kike hukatiziwa masomo yao huku wale wa kiume wakiendelea. Hapa wahusika wa jinsia ya kike huwa wamedhulumiwa na jamii. Jamii huwaona kama viumbe visivyo na thamani. Wakati mwingine wahusika wa kike hupitia mapigo ya kimwili na wazazi wao baada ya kupata mimba. Utesi huu hufanya wengine hata kutoroka nyumbani. Dora inasemekana alitoroka baada ya kupigwa sana ili ataje aliyempachika mimba. Hivyo, suala la kupachikwa mimba kwa jinsia ya kike na jinsia kiume linatumiwa kuwadhalilisha. Matokeo ya kupata mimba huwa ni kuzaliwa kwa mwanaharamu anayekosa wa kumwajibikia kimatumizi kwani wale wa jinsia ya kiume huwatelekeza.

Kalulu alimwambia Kamkanda kuwa alikuwa mtoto mchanga ambaye bado alikuwa ananuka maziwa ya mama. Kalulu alikasirika sana kutokana na matamshi hayo. Usemi huu unatumiwa kuendeleza dhuluma za kijinsia. Maziwa ya mama hupatiwa mtoto mchanga akiwa ukembeni wake. Hata hivyo, neno hili linapotumika kwa jinsia ya kiume huonekana kuwa usemi wa matusi. Pia huonekana kama njia ya kudhalilisha jinsia ya kiume wakati huo. Pia usemi huu huonyesha vile jamii huendeleza maonevu kwa mwanamke. Usemi kama huu unatumika kama njia ya kurudisha nyuma maendeleo ya mwanamke.

Bon Kolo katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* Uk.117, alisema kuwa hakuwa na ndugu wala baba. Mamake Kolo alikuwa mmoja wa wale mamia ya wanawake waliojiuza mitaani ili kupata kipato. Wakati Bon Kolo alipokuwa anasoma mama yake alifariki kwa sababu ya majeraha yaliyotokana na kipigo kutoka kwa mabwana watatu ambao walimfumania. Tukio hili linadhihirisha dhuluma za kijinsia zilizokita mizizi katika jamii. Kitendo hiki kinaonyesha unyimwaji wa haki katika jamii. Hivyo wanawake hunyanyaswa na jinsia ya kiume bila usemi wowote. Wanawake hunyenyekea kwa waume wao au wahibu wao kwani huogopa kurejeshwa kwao nyumbani. Wanaume hujitokeza kama dhulumati katika jamii. Wanawake hujitokeza

kama viumbe wanyonge katika jamii kwani wao hawaruhusiwi kuwaongoza waume wao.

Mwanamke anayeshiriki uasherati huonekana mwovu katika jamii. Mwanamke asiye katika mahusiano ya ndoa huwa anadharauliwa na hata kukebehiwa. Huonekana kama kimada wa kunyakua waume wa watu. Dora alionekana kuwa malaya na Kandili baada ya kujifungua nje ya uhusiano wao. Kandili alimwona Dora kama msaliti mkubwa. Vile vile Maua alionekana alikuwa mwovu zaidi na malaya. Aliona kuwa alikuwa na mtazamo na mwendo wake ukiwa umalaya mtupu. Jamii ilikuwa na mtazamo hasi kwa wahusika kama Dora na Maua. Walionekana kama viumbe ambao ni dhaifu. Mwanamke anadhulumiwa kwa sababu ya maumbile yake. Jamii ni kana kwamba imehalalisha dhuluma hizi za kijinsia. Jamii inafaa itazame wanawake kama viungo muhimu wanaofanikisha masuala ya kifamilia, kiuongozi na kijamii kwa jumla. Wahusika wa kiume waliwachukulia wanawake kama vyombo vya starehe.

Wakati mwingine wahusika wa kike hutumiwa kwa njia mbaya. Wao hutumiwa kama vyombo vya kuendeleza maovu katika jamii. Wao hutumiwa kama chambo cha kunasa maadui na pia kuendeleza ufisadi katika jamii. Pia wahusika wa kike wakati mwingine hudhulumiwa katika harakati hizi. Harakati kama hizi za kufanikisha maovu katika jamii huwa hatari kwa maisha. Bon Kolo alimtumia Maua kama chombo cha kumnasia adui wake Kandili. Hii ni dhuluma kwa wanawake. Hata hivyo, ni vyema kubaini kuwa ukubalifu huu wa wahusika kama Maua huwa na msukumo wa tamaa ya mali. Hivyo hapa naye mwanamke anapata nafasi ya kudunishwa.

Tunaona kuwa Kandili alizubaa alipoona utupu wa Maua na hata baadaye aliumizwa na hasimu wake. Maua hapa anahusishwa katika kazi hatari ya kulipiza kisasi.

Msukumo wa kupata mali nyingi wakati mwingine husababisha dhuluma kwa jinsia zozote mbili. Haya yanasawiriwa katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* uk.39 na Uk.141. Uroho wa wahusika mbalimbali husababisha waja kueneza ukatili. Serikali ya Arusha ilikuwa inajaribu kuongeza uzalishaji wa dawa ya *Oxton* hata kama ilikuwa inafichwa na kuuzwa kwa magendo. Watu wengi waliteseka ikiwemo watoto wa jinsia zote ambao hawakuwa na hatia. Njama hizi ziliendelezwa na wahusika kama Bon Kolo. Biashara hizi za kimagendo zilidhulumu jinsia zote mbili kwani wengi waliaga dunia baada ya kukosa dawa ya *Oxton* ya kuzuia palala. Dawa ya *Oxton* ilikuwa ya kutibu

palala ila matajiri waliiuza kwa njia za kimagendo. Jamii ilikandamizwa sana. Hali ilikuwa vilevile katika serikali ya Idi Amin kwani ilikandamiza watu wengi. Wazazi wa Kamkanda walipondwapondwa kwa vifaru. Utawala wa Idi Amin uliendeleza ukatili wa jamii.

Katika mahusiano ya kila siku suala la dhuluma za kijinsia hujitokeza. Wengi hukosa kutekeleza wajibu wao hivyo kusababisha madhila kwa jamii. Hata wale watu huwa wametengewa nyadhifa za uongozi wao wakati mwingine hutelekeza kazi zao na kusababisha changamoto. Tunaona daktari wa Kamkanda akiwa radhi kumuua Kamkanda almuradi apewe mihela. Aliiona kazi ndogo sana akipewa laki. Hivyo daktari alikuwa anadhulumu wagonjwa kwa sababu ya tamaa ya mali. Daktari anaonekana yuko radhi kukandamiza haki za mgonjwa wake kwa sababu ya umero.

Ukatili uliotekelezwa na watawala wa umma uliwaumiza hata wale ambao hawakuwa na hatia. Udhalimu wa kijinsia ulileta kikwazo cha maendeleo na ufanisi wa taifa lolote lile. Mateso ambayo huibuka miongoni mwa jinsia mara nyingi husababishwa na jinsia ya kiume kwa ya kike. Hali hii husababisha maonevu ya kila aina kwa wahusika wasio na hatia. Mhimili wa utamaduni katika nadharia ya Ubabedume huwa unaelezea mtazamo wa jamii kuhusu jinsia zote. Ukiukaji wa haki za kijinsia huegemezwa katika misingi hii. Hulka ya wanawake kuwa watu watulivu, wapole, watiifu, wanyenyekevu na waaminifu kwa waume zao hutumiwa kuendeleza dhuluma za kijamii dhidi yao. Udhaifu huu wa jinsia ya kike hutumiwa kama kipengele cha kuwadhulumu wanawake.

### 4.3.3 Utabaka wa Kijinsia

Suala la utabaka katika Ugiriki na Roma uliongozwa na hali za uzalishaji mali na biashara ya watumwa ambapo watumwa waliuzwa kwa njia ya ubaguzi wa rangi, mali na jamii anayotoka mtu (Haji, 2018). Utabaka ni hali ya kuwepo kwa kundi la watu katika jamii linalojitofautisha na kundi jingine kwa misingi ya kiuchumi au kielimu. Ni hali ya kuwepo kwa pengo kubwa kati ya makundi ya watu hasa maskini na matajiri. Utabaka wa kijinsia ni kuwepo kwa pengo la kijinsia miongoni mwa watu katika jamii. Utabaka wa kijinsia huleta utengano, ukandamizaji na udunishaji wa baadhi ya watu wa jinsia fulani katika jamii. Fauka ya hayo, utabaka wa kijinsia huchangia kuwepo kwa ubaguzi wa kijinsia.

Katika jamii huwa kuna mgawanyo wa kijinsia mathalani jinsia ya kiume na jinsia ya kike. Mgawanyo huu huchangia kuibuka kwa matabaka ya kijinsia kwani jinsia ya kiume huchukuliwa kuwa tabaka la juu huku jinsia ya kike ikiwa tabaka la chini. Hali hii huchangiwa na mawazo pendwa ya kijamii. Utengano huu wa kitabaka huleta migogoro ya kijamii kwani kila jinsia huwania nafasi ya kupata hadhi ya juu. Tunaelezwa kuhusu Babake Dora alivyokuwa mkali katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* uk.87. Inadaiwa kuwa kama angemfahamu Kandili aliyempachika Dora mimba angemwadhibu. Tunaona kuwa Dora alitusiwa, akapigwa na kupewa vitisho na babake mzazi. Baba alimdhulumu mwanaye. Babake Dora anawakilisha tabaka la juu linalowakilishwa na jinsia ya kiume. Babake Dora aliwakilisha tabaka la juu la kijinsia lililotumia uwezo wao kitamaduni kukandamiza jinsia ya kike. Dora anawakilisha jinsia ya kike ambayo haina usemi. Kukosekana kwa usawa wa kijinsia kulichangia maenezi ya maonevu kwa tabaka la chini linalowakilishwa na jinsia ya kike. Ubaguzi huu wa kijinsia kitabaka unachangia madhila kwa tabaka ambalo halina nguvu. Unyonge unaodhihirishwa na jinsia ya kike na nguvu ambazo zimekubalika kijamii kwa jinsia ya kiume zinachangia utengano wenye mwanya mpana.

Utabaka wa kijinsia huchangiwa na tamaduni za jamii husika na pia uwezo wa kiuchumi wa wahusika. Kaida za jamii hutukuza jinsia ya kiume na kudhalilisha jinsia ya kike. Dora alipotorokea majengo Arusha, hakupata ajira ila waliotaka kumpa kazi walimtaka atoe rushwa na mapenzi. Dora anajitokeza kama mhusika katika tabaka la wachochole au walalahoi. Hata kile kibarua alichokipata kilimfaa kwa mlo na mavazi haba. Alipoandamwa na wanaume waasherati aliwasusia hadi wakamwita mwendawazimu. Dora alibaguliwa kwani alionekana ametoka kwenye tabaka la chini la kijinsia na kiuchumi. Wanaume hawa wanawakilisha tabaka la juu hata kijinsia lililo na nguvu.

Utabaka kama huu wa kijinsia unaonekana kuchangia migawanyiko katika jamii. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa wale wahusika wa jinsia ya kiume ambao hawana uwezo wa kiuchumi hubaguliwa na kutengwa. Utabaka wa kijinsia husababishwa uwezo wa kiuchumi na itikadi za kijamii. Utabaka huleta hali ya mapendeleo katika utambulisho wa watu. Utabaka wa kijinsia ni wa zamani kwani ulikuwepo tangu dunia ilipoumbwa. Adamu aliumbwa kama kiongozi wa shamba la Edeni naye Hawa kama msaidizi. Hii ni kusawiri utabaka wa kijinsia kwani jinsia ya kiume inapewa hadhi kuu huku jinsia

ya kike ikiwa na hadhi ya chini. Utabaka wa kijinsia huendelezwa pia na mizizi iliyokita ya mfumo dume katika jamii.

Katika riwaya ya *Dar-es-Salaam Usiku* kuna utabaka wa kijinsia. Utabaka huu unachangia kuwepo kwa ubaguzi wa kijinsia. Tunaelezwa kuwa katika harakati za kumtafuta mamake Peterson, mzee Kautipe alilelezwa kuwa watu hawakuwa wamemwona mwanamke huyo. Tena aliambiwa hawakuhitaji kumtia machoni. Walidai kuwa alikuwa mtu aliyelaaniwa. Nunu ambaye alikuwa mamake Peterson alibaguliwa na kuchukuliwa kama tambara bovu. Alibaguliwa kwa misingi ya kijinsia ni kana kwamba alitekeleza maovu katika jamii akiwa pekee yake. Hulka zake za uasherati zilichangia kubaguliwa kwake. Mwanamke alibaguliwa na kuchukuliwa kama kiumbe hafifu.

Jamii huwa haitambui mwanamke kama mchumi lakini huwa anasawiriwa kama mtegemezi. Hali hii hufanya wanawake kuingia madanguroni ili kujaribu kuziba pengo la ulitima. Ubaguzi wa kijinsia unaosababishwa na utabaka hufanya kujazwa hofu, maumivu na unyonge katika ngazi za kijamii. Ubabedume ambao wanaume huwa nao hutumiwa kwa njia hasi kusababisha ubaguzi wa kijinsia. Bon Kolo alitumia pesa kunasa wanawake. Uwezo wa kifedha ulimjaza kiburi hadi kuwabagua wanawake. Aliwaona wanawake kama viumbe duni walio katika tabaka la chini. Idrisa Kalulu naye alikuwa mwajiri aliyetia waajiriwa hofu ya kufutwa. Aliwatenga kitabaka na kuwabagua. Wafanyakazi wangefukuzwa kwa makosa madogo tu. La kusikitisha ni kuwa hata kama wangeomba radhi kwa machozi ya damu hangewasikiza.

Kandili alidai kuwa Dora hakuwa mwanamke wa kumkosesha utulivu. Dora alifukuzwa shuleni kwani alibaguliwa kijinsia baada ya kuwa mja mzito. Dora anabaguliwa kwa kuwekwa katika tabaka la wasio navyo. Tabaka hili linahusisha jinsia ya kike na wanaume wengine ambao hawana sifa angavu za kiume. Utabaka huu wa kijinsia kama wa kufukuza mtoto wa kike unachangiwa na mawazo pendwa katika jamii husika. Wahusika wa kiume wanaosababisha madhila haya wao hawachukuliwi hatua. Itikadi za kijamii ni kana kwamba zimehalalisha ubaguzi huu wa kijinsia.

### 4.3.4 Utepetevu

Utepetevu ni hali ya ulegevu na uvivu. Ni hali ya kukosa kuwajibika kazini. Ni hulka ya kupuuza wajibu au kazi ya mtu mwenyewe. Matarajio ya watu wengi ni kuwa

ukipewa jukumu unafaa kuajibika. Hata hivyo, watu wengi hukosa kujukumika na hivyo husababisha changamoto kwa jamii. Utepetevu huu husababishwa na ubwete, matatizo ya kimwili au kukosa uelewa wa jambo.  Waja wengi katika jamii huwa wanapewa majukumu kulingana na kijinsia. Jinsia ya kiume hutarajiwa kukidhi mahitaji ya kimsingi ya kinyumbani kwani wao ndio wachumi. Pia wanaume hutarajiwa kuangazia maslahi ya familia na pia shughuli za kindoa. Kwa upande ule mwingine wanawake hutarajiwa kutekeleza shughuli za kinyumbani na pia kuangazia maslahi ya mume na watoto. Wanajinsia hawa wanapokosa kutekeleza majukumu haya wao huonekana wakiwa watepetevu.

Katika riwaya ya *Dar-es-Salaam Usiku* Uk. 117, Peterson alipoenda kufanya mapenzi na mama Sonny alikosa kuwajibika. Mama Sonny alijaribu kumfanyia mwili wa Peterson shughuli zozote za kimahaba lakini hakuonyesha ishara yoyote ya utendakazi. Hali inasawiri kuwa Peterson alionyesha utepetevu kwa kukosa kushughulikia mama Sonny kimapenzi. Athari hii ilisababishwa na mahusiano ya nje ya kimahaba. Alikosa nguvu za kushughulikia mkewe kimapenzi. Ni kana kwamba alikuwa amekinaishwa na mapenzi ya Gloria. Isitoshe, alikosa kumhudumia Gloria kiafya mpaka hali ya afya ikazorota. Hata Peterson hakuamini alivyomwona Gloria akiwa amebaki mifupa mitupu kwa kutotunzwa. Taswira hii ya mifupa mitupu inaonyesha vile utepetevu ulikuwa umesababisha madhila kwa Gloria. Hii ni ishara kuwa Peterson alikuwa amekosa kuwajibika na kutelekeza mkewe.  Utepetevu huu ulikuwa umesababishwa na ubabedume kwani itikadi za kijamii huamini mahusiano ya kimapenzi na wandani wengi.

Uwezo wa kijamii ambao hushamiri miongoni mwa wanaume katika jamii wakati mwingine husababisha utepetevu. Nguvu hizi ambazo huwa zinanawiri kwa sababu ya utamaduni wa jamii huwa na athari hasi wakati mwingine.  Katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka*, Kandili Maulana licha ya kuwa na mali nyingi alikosa kuwajibika. Alichelea kufuata wosia wa mamake kuhusu ndoa. Aliendelea kustarehe na wasichana wowote wa mitaani. Aliendelea kustarehe na wengi ila hakuwapenda. Msingi wake kama mwanamume katika mahusiano ya ujenzi wa ndoa uliyumbayumba. Katika harakati za kuendeleza ubabedume kupitia mahusiano na vimada wengi alikosa kuwajibika.

Uozo wa kijamii wakati mwingine husababisha utepetevu. Njama za ufisadi na tamaa wakati mwingine husababisha hali ya kutowajibika. Wachunguzi wa kifo cha

Kamkanda baada ya kuteuliwa serikalini walijaribu kutekeleza wajibu wao lakini hawakutimiza wajibu huo walipuuza ushahidi muhimu. Kila mmoja alihongwa. Tamaa na ubinafsi wa baadhi ya watu husababisha utepetevu. Haki za kibinadamu hukiukwa kwani wenye kuwajibika hutelekeza wajibu wao.

Idrisa Kalulu alitumia kiburi chake kuwakandamiza wafanyakazi. Alionyesha mapuuza kwa wale wote waliokuwa chini yake kimamlaka. Kutowajibika kwa Idris Kalulu kulisababisha utepetevu kikazi kwani wafanyakazi hawakuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Mapuuza yake na pia dharau zake zilileta migogoro ya kikazi. Ubinafsi wa Kalulu ulisababishia kampuni madhila. Ukosefu wa busara ulisababisha utenda kazi wa Kalulu kuwa hafifu. Kandili sawa na Kalulu ni vielelezo vibaya kwa jamii kwani wanatelekeza majukumu yao. Utepetevu wa wahusika hawa unaendeleza maangamizi kwa jamii. Hali hii inaonekana kukitwa mizizi na dhana ya ubabedume. Hali ya kujiona kama jinsia yenye nguvu inasababisha maenezi ya kutosikiliza wengine hivyo kusababisha utepetevu.

### 4.3.5 Utapeli

Utapeli ni udanganyifu au hila au ujanja unaojitokeza katika biashara au masuala mengine ya kijamii. Utapeli huhusisha njia haramu katika kufanikiwa kwa jambo. Msukumo wa kutajirika haraka na pia tamaa ya uongozi hupalilia uozo huu. Tapeli hutumia njia za mkato kutekeleza azma yake. Ubabedume wakati mwingine hupalilia utapeli wa wanaume. Ushindani wa mafanikio katika maisha na pia kuzibua riziki ni baadhi ya sababu za kupalilia utapeli. Kandili alijaribu kushawishiwa na Bon ili anze biashara haramu. Biashara hii haramu hukusudia kutumia njama chafu za kuuza dawa ya *Oxton.* Dawa hii ilikuwa inazuia ugonjwa wa watoto uliojulikana kama Palala. Hivyo biashara hii iliwanyima wananchi wa taifa husika matibabu. Watoto wengi waliangamia baada ya dawa hizi kuuzwa kisirisiri. Mawazo ya kiutu yalikuwa yamewatoka binadamu. Njama hizi za kutapeli wananchi wasio hatia zilisababisha madhila kwa jamii.

Bon Kolo pia alikuwa akiendesha biashara zingine haramu. Alikuwa ananunua sukari, sabuni, betri, chumvi, unga, nguo dawa na kile alichokipata na kuvizika ardhini. Alivipata vitu hivyo kwa wingi baada ya kutumia rushwa. Vitu hivi alivizika ili kuviuza baadaye wakati bei ilikuwa imepanda. Fauka ya hayo, Kandili kwa sababu ya tamaa ya mali aliingilia biashara za kimagendo. Bon na Kandili waliendeleza biashara za

kimagendo kama kuuza pembe za ndovu, ngozi za chui, madini mbalimbali na fedha za kigeni. Hawa ni wanaume ambao wanatumia ujanja kuendeleza maovu katika jamii. Hulka ya wanaume kuwa jasiri na pia kuwa wasaka riziki huwasukuma wahusika hawa katika maovu haya. Biashara hizi za kimagendo zilikuwa kinyume cha sheria lakini waliziendeleza. Mifumo ya kijamii huwa inakweza mwanamume katika jamii kutokana na ubabedume.

### 4.3.6 Usaliti

Usaliti ni hali ya kukosa uaminifu kwa utoaji wa habari za siri. Ni utoaji wa habari za siri za mtu au nchi kwa adui yake. Wanadamu huwa wanaendeleza usaliti kwa sababu ya wivu au tamaa. Ubinafsi na ujanja pia huchangia ukosefu wa uaminifu. Rukia alivuta suruali ya mwenzi mmoja na kutoa pesa mfukoni mwake. Mfuko wa kwanza alitoa shilingi elfu mbili halafu shilingi elfu sitini. Baadaye alimpulizia dawa mteja wake. Kitendo hiki kinaonyesha usaliti wa hali ya juu. Rukia alitumia ujanja kusaliti mwandani wake. Tamaa ya mali ilimsukuma Rukia kumsaliti mwandani wake (Uk. 128). Mwanamume huyu alisalitiwa kimapenzi na Rukia. Pia msukumo wake wa kujihusisha na wanawake wengi ilisababisha kusalitiwa na baadhi yao. Hulka ya wanaume kuwa na wahibu wengi huchangiwa na ubabedume.

Viongozi pia husaliti wananchi kwa sababu ya tamaa ya mali. Kandili alikuwa mzalendo wa taifa lakini alibadilika. Utamu wa fedha aliokwisha kuonja na kuupenda ulifanya aendelee kushiriki katika ulanguzi na ufichaji wa vitu adimu. Tamaa ya mali ilimfanya kukosa utu na kusaliti jamii. Biashara zake haramu zilimfanya awe na uroho na hatimaye kusaliti utu na nafsi yake. Kandili anasawiri hulka ya kutaka kutajirika haraka kwa njia haramu. Anaendeleza ubabedume kupitia usakaji wa uwezo wa juu wa kiuchumi. Katika nadharia ya Ubabedume mwanamume anatambulika kama mhusika mwenye uwezo wa juu wa kiuchumi ili kukidhi familia na wengineo. Katika harakati za kufikia lengo hili wanaume hujipata wakitumia njia ambazo siyo halali kujinyakulia mali. Hali hii hufanya wasaliti utu wao pamoja na wananchi. Katika mchakato huu, wanaume huwa hawajali maslahi ya wengi kwani wao hupiga moyo konde.

Usaliti wa kimapenzi katika jamii hujitokeza mara nyingi. Wanaume mara nyingi husaliti wapenzi wao lakini pia wanawake husaliti wanaume. Wanaume ambao huwa na mahusiano mengi ya kimapenzi husaliti baadhi ya wapenzi wao. Kandili alimsaliti Dora. Kandili na Dora walikuwa wapenzi wa kimahaba. Kandili alikosa kuwa

mwaminifu kwa Dora kwa kujihusisha na vimada wengi mtaani. Kandili alimtelekeza mpenzi wake Dora kwa kumwacha katika maisha ya uhawinde. Kandili alikosa kumwajibikia Dora na hakutaka kuhusishwa na Dora. Itikadi ya wanaume kujihusisha na wanawake wengi ilisababisha usaliti katika mahusiano ya kindoa au kimapenzi. Usaliti wa kimapenzi ulifanya mahusiano ya kimapenzi kudorora. Uwezo wa mwanamume kuwa na mahusiano na wanawake ni itikadi inayotazamwa kama ukwasi katika jamii. Mwanamume wa aina hii huheshimiwa kwa kupewa hadhi ya juu kuliko wanaume wenye mke mmoja tu. Jamii huamini wakati wowote mwanamume huwa hana hatia. Mwanamume mwenye mahusiano ya wanawake wengi hufananishwa na msasi ambaye kila wakati huwa mawindoni. Msasi huyu huwa hatosheki na kila wakati huwa katika shughuli za mawindoni.

Usaliti wa kijamii mara nyingi huchangia kuwepo kwa migogoro. Mwanamume mara nyingi huendeleza ubabedume kupitia kwa nguvu zilizotambulika katika jamii. Uwezo wake kimaumbile na pia itikadi za kijamii hushamirisha usaliti wakati mwingine. Peterson alikuwa amemsaliti mkewe Gloria. Alihisi hatia kubwa. Alijuta vile alikuwa amemtelekeza mwanaye. Peterson alimhurumia mama Sonny na hata mwanawe. Machozi yalimlengalenga kwa sababu ya majuto. Peterson aliisaliti jamii yake kwa sababu ya mahusiano ya kimapenzi na vimada wa mitaani. Peterson alikuwa amekosa kuwajibikia familia yake kwa sababu ya vimada kama Rukia. Hali hii ilisababisha hata usumbufu wa kiakili kwa Peterson. Wanaume ambao huwa wanatambulika katika jamii huwa ni wale wenye wake wenza. Umiliki wa wake wenza huonyesha umwinyi na uwezo wa kijamii.

Hali ya kuwepo kwa ubabedume miongoni mwa wanaume ilichangia maenezi ya usaliti baada ya wivu kujikita katika nafsi zao. Uwezo wa kutimizia mahitaji wanawake wengi ulionekana kama jambo la kupigiwa mfano. Hata hivyo, ushindani miongoni mwa wahusika wanaume katika mahaba ulichangia usaliti. Katika jamii nyingi za Kiafrika wanaume huruhusiwa kuwa na wanawake wengi. Hulka hii huonekana kama ufanisi miongoni mwa wanajamii. Usaliti wa viongozi wa kifamilia mara nyingi husababisha utelekezaji wa wanajamii.

### 4.3.7 Anasa

Anasa ni hali ya raha na starehe yaani kitu kisicho muhimu kwa maisha. Anasa huambatanishwa na hali ya kubarizi baada ya kazi. Anasa huhusishwa na jinsia zote

mbili. Hata hivyo, jinsia ya kiume ndiyo hujipata katika kuponda raha. Anasa huhusisha matumizi ya pesa katika ulevi, wanawake, vyakula na njia zingine za matumizi.

Katika kuonyesha uwezo wahusika wa kiume mara nyingi huwa wanajiingiza katika anasa au starehe na kuwateka wahusika wa kike katika lindi la raha. Wahusika wa kiume huwa wanaendeleza uzinifu katika kumbi za starehe. Tunaelezwa kuhusu ukumbi maarufu wa Kinondoni ambao kulikuwa na vijana wawili wakiwa mtu na mpenzi wake. Pia kulikuwa na wanaume wanne ambao walikuwa wanahudumiwa na mwanamke mmoja mlevi kwa zamu. Wahusika hawa wa kiume walikuwa wamejikita katika lindi la raha. Kutokana na hali ya kutalii dunia wote walikuwa na wahibu waliokuwa wanastarehesha katika kumbi za anasa.

Msukumo wa kuingia katika anasa hutokana na itikadi za kijamii za mwanamume kuwa na mahusiano mengi ya kimapenzi. Mienendo hii husawiri mwanamume kama simba katika jamii. Haya yanadokezwa katika riwaya ya *Dar-es-Salaam Usiku* uk.25

> *Meza ile inao watu watano. Wanaume wanne mwanamke mmoja. Huyu mama yeye anaonyesha kuwa kalewa zaidi ya wenziwe.*

Anasa za dunia huhusishwa na ukwasi wa wahusika. Wanaume ambao hujiingiza katika raha za kilimwengu huwa wana uwezo mkubwa wa kiuchumi. Anasa za ulevini, uasherati, ubadhirifu wa mali ni baadhi ya ishara zake. Peterson alimwepuka Bougwan kwa sababu alipenda pombe na aliibugia sana. Hivyo Peterson aliogopa kuwa angeaibika mbele ya marafiki zake kwani wangefanyiana upuuzi baada ya kulewa. Bougwan alijiingiza katika uwanja wa anasa. Pia Peterson alikuwa mlevi chakari aliyefurahia ulevi. Katika anasa zake za ulevi angepatana na wahusika kama Rukia. Katika harakati hizi za anasa angejiingiza katika uasherati na kutelekeza mkewe. Ubabedume wa wahusika wa kiume uliwasukuma katika raha za ulimwengu. Katika harakati za kuonyesha makucha ya uwezo wao kijamii waliweza kuwateka wanawake wa kando ulevini.

Wanaume wengi hutambulikana kwa sababu ya matumizi yao. Bon Kolo alijulikana kwa starehe. Jina lake lilisifika katika baa kubwa zote. Daima akiandamana na vipusa wazuri ambao ndiyo walifahamu siri halisi ya matumizi yake. Tunaelezwa kuwa hakuhurumia pesa. Katika maelezo haya tunawaona wanaume kama vielelezo vibaya katika jamii. Wanaume walitumia uwezo wao wa kiuchumi kuendeleza matumizi

mabaya ya fedha. Utamaduni wa jamii za Kiafrika husawiri mwanamume kama kiumbe huru ambaye amekwezwa katika mfumo wa kijinsia. Wanawake nao wanajitokeza kama viumbe wategemezi wanaotegemea wanaume sana.

Katika kutekeleza raha za kilimwengu uozo wa kijamii huendelezwa. Njama za ufisadi huendelezwa katika sehemu za starehe. Tunaelezwa vile Bon Kolo alijaribu kumshawishi Kandili kwa kumpa kitita cha noti. Bon alitaka Kandili atekeleze unyama kwa kustareheshwa kwa fedha nyingi. Ukatili ungetekelezwa na Kandili baada ya kufurahia anasa. Ubinafsi wa Bon ungemsukuma Kandili kutekeleza ukatili. Wanaume mara nyingi hutekeleza ukatili kama njia ya kuangamiza mahasimu wa mahusiano ya kimahaba.

Wanaume wengi huonyesha ubabe wao katika sehemu za burudani kwa matumizi ya fedha kiholela. Anasa za maishani huwapa wanaume nafasi adimu ya kudhihirisha ubabedume. Pia huwa ni nafasi nzuri ya kuotesha mahusiano na wanawake wengi kimapenzi. Wahusika mara nyingi wanaojiingiza katika anasa au burudani huwa wana tamaa.

### 4.3.8 Unafiki

Unafiki ni hali au tendo la kujifanya kuwa mkweli au kujidai kuwa rafiki ilhali mtu ni adui. Vitendo vya mtu mnafiki huwa vya kama kuwa na ngozi ya kondoo kumbe ndani ni mbwa mwitu. Mnafiki huwa mtu mwongo. Wanaume kama Peterson walijawa na unafiki mkubwa. Alifurahia uhusiano wake na Rukia mpaka kupuuza mkewe. Peterson alijifanya mzuri kwa mama Sonny kumbe alikuwa anamwendea kinyume.

Mama Sonny pia kwa upande wake alikuwa amekata shauri kuwa hangepoteza machozi yake kwani Peterson hakuwa mwanamume pekee. Katika harakati za wanaume kusaka vimada wa nje wao hugeuka kuwa wanafiki. Katika mhimili wa itikadi, uwezo wa mwanamume huwa umekwezwa katika jamii hivi kwamba wako na nguvu za maamuzi na pia vitendo vyao.

> *Hakuna wakati mzuri wa kumpokonya mwanamume wa mtu zaidi ya wakati ambao uhusiano wake na mkewe unalegalega. Uk.110*

Bon Kolo alimtumia Maua kama chambo cha kumnasia adui yake. Maua alikuwa kivutio kwa wanaume na hata alionyesha kiburi. Maua alibagua wanaume kwa misingi

ya utajiri. Kutokana na tamaa ya mali, Maua alitumiwa kutekeleza maovu kwa sababu ya udhaifu wake. Tamaa ya mali ilifanya Maua kutekeleza madhila katika jamii. Hivyo basi, unafiki unaendelezwa kuwili na jinsia zote mbili. Wahusika wa kiume waliendeleza unafiki wakiwa na azma ya kunasa wahusika wengi wa kiume. Unafiki unajitokeza katika harakati za kusaka mali na mapenzi. Katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* uk.88 tunadokezewa haya:

> *Na alikuwa mwongo mzuri hata angeweza kumfanya mwanamume yeyote aamini kuwa ndio kwanza anamharibia ubikira wake*

### 4.4 Hitimisho

Sura ya nne iliangazia matokeo ya utafiti ili kutoa majibu kwa maswali ya utafiti. Kwanza ilibainika wazi kuwa riwaya teule zilisheheni sura mbalimbali za ubabedume. Sura zilizojidhihirisha ni kama vile utamaduni, kiuchumi, dhakari, kimaumbile, kisaikolojia na kisiasa. Sura hizi za ubabedume zilijitokeza miongoni mwa wahusika mbalimbali wa kiume. Uchunguzi ulithibitisha kuwa sura hizi zilijitokeza hasa tukiangazia mihimili mbalimbali ya nadharia ya Ubabedum. Uchunguzi wa mtafiti pia ulisawiri kuwa kulikuwa na athari za ubabedume kwa jinsia. Athari hizi ni kama vile ukahaba, unafiki, anasa, usaliti, utapeli, utepetevu, utabaka wa kijinsia na dhuluma za kijinsia. Athari hizi zote zilichangiwa na ubabedume kama inavyosawiriwa na mtafiti. Kwa kifupi, matokeo ya utafiti katika sura hii ni majibu mwafaka kwa maswali yalioongoza utafiti huu. Hii ina maana kuwa madhumuni yote mawili ya utafiti huu yaliafikiwa kikamilifu.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alitoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya matokeo ya utafiti huu na uchanganuzi wa data katika sura ya nne. Muhtasari uligusia mambo ya kimsingi yaliyozingatiwa ili kufanikisha utafiti huu. Miongoni mwa yale yaliyokuwa nguzo muhimu ya utafiti ni nadharia iliyozingatiwa, suala la utafiti na madhumuni ya utafiti. Sehemu ya hitimisho ilijumuisha hoja muhimu za matokeo ya utafiti kwa mujibu wa madhumuni husika kwa ufupi. Hatimaye, mtafiti alitoa mapendekezo yake mwenyewe hasa kwa kuzingatia suala la utafiti na madhumuni husika. Katika

kupendekeza mtafiti alizingatia suala la sura za ubabedume na athari za ubabedume kwa jinsia katika riwaya teule.

### 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Sehemu hii iliangazia mambo ya kimsingi ya utafiti huu katika kurasa tangulizi na kila sura kwa ufupi. Sehemu ya kurasa tangulizi ina mada ya utafiti, idhini, tabaruku, shukurani, yaliyomo, ikisiri, abstract, na maelezo ya istilahi muhimu. Sura ya kwanza ilishughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na hatimaye upeo na mipaka ya utafiti. Dira ya tasnifu ambayo ndiyo sura ya kwanza, iliangazia mambo ya kimsingi ya tasnifu ambayo hutoa mwelekeo kuhusu utafiti.

Kwanza usuli wa mada ambao hutupa ufafanuzi wa kimsingi kuhusu mada ya utafiti. Pili, suala la utafiti lilibainisha pengo la kiakademia lililohitaji kujazwa liliangaziwa. Tatu, shabaha ya utafiti huu ilifafanuliwa katika sura hii ili kuonyesha kusudi la utafiti. Pia sehemu hii ilishughulikia maswali ya utafiti kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Vilevile sura hii iliangazia natija na mchango wa matokeo ya utafiti huu kwa idara ya fasihi na jinsia kwa ujumla. Kadhalika, upeo na mipaka ya utafiti ulimulikwa kwa kina.

Katika sura ya pili mambo mawili ya kimsingi yaliangaziwa. Kwanza mtafiti alipitia maandishi ya wataalamu mbalimbali walioshughulikia mada zilizokaribiana na mada ya utafiti. Lengo kuu la mapitio ya maandishi lilikuwa kuonyesha na kubainisha mfanano na tofauti iliyopo kati ya utafiti na tafiti zingine zilizotangulia kwa minajili ya kujaza pengo la kiusomi.

Hatimaye, sehemu hii iliangazia misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu. Nadharia ya Ubabedume ilipambanuliwa huku mihimili yake muhimu iliyotumika kufanya utafiti ikibainishwa wazi. Ili kutambua na kubainisha sura za ubabedume katika riwaya hizi pendwa, mtafiti alitumia nadharia ya Ubabedume iliyoasisiwa na Raewyn Connell na kuendelezwa na Robert Bly. Pia nadharia hii ilisaidia katika upambanuzi wa athari za ubabedume kwa jinsia. Sehemu hii kwa kifupi ilikuwa muhimu sana katika utafiti huu kwani ilitoa msingi imara wa kufanya uamuzi wa mafanikio ya utafiti huu. Ili kutambua sura za ubabedume na athari za ubabe dume mtafiti alitumia nadharia ya ubabedume.

Utafiti huu haungefanywa na kukamilika bila mbinu za utafiti. Hivyo basi, sura ya tatu ilishughulikia mbinu za utafiti. Mahali pa utafiti paliwekwa wazi katika sura hii huku

njia zilizotumika kukusanya data na kuchanganua data hiyo zikiwekwa wazi. Muundo wa utafiti pamoja na kikundi lengwa ni sehemu zilizoangaziwa katika sura hii. Namna data ilivyoteuliwa vile vile ilielezwa na kupambanuliwa. Pia jinsi data ilivyokusanywa kwa kutumia upekuzi-changanuzi wa yaliyomo na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kiuthamano iliyotilia mkazo maelezo yakinifu ya mambo yanayojitokeza, ni masuala yaliyotiliwa mkazo katika sura hii.

Sura ya nne iliangazia matokeo ya utafiti na kutoa majibu kwa maswali ya utafiti. Sehemu ilichanganua data iliyokusanywa kwa kuegemea nguzo za nadharia ya Ubabedume. Kwanza ilibainika kuwa riwaya hizi za Ben Mtobwa zilishamiri ubabedume. Ubabedume huu ulijitokeza miongoni mwa wahusika katika mazingira tofauti. Wahusika hawa waliendeleza ubabedume kwa sababu ya itikadi za jamii. Sura mbalimbali za ubabedume zilijitokeza kama vile sura ya utamaduni, sura ya kisaikolojia, sura ya kiuchumi na sura ya kimaumbile. Pia athari za ubabedume kwa jinsia ziliangaziwa kama vile utabaka wa kijinsia, ubaguzi wa kijinsia, ukahaba na mengineyo. Mtafiti alibaini kuwa ubabedume una athari hasi kwa jinsia zote.

Hatimaye sura ya tano ilishughulikia muhtasari ambao ulieleza kwa ufupi mambo yaliyoshughulikiwa katika kila sura. Pia sura ya tano ilitoa hitimisho kwa kuangazia matokeo ya utafiti huu mintarafu ya kila madhumuni. Mwisho kabisa, sura hii ilitoa mapendekezo yaliyotokana na matokeo ya utafiti huu. Katika utafiti huu, mtafiti alichanganua riwaya za Ben Mtobwa mathalani *Dar-es-salaaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka*.

Data ya utafiti huu ilikuwa kuhusu sura za ubabedume katika riwaya husika. Fauka ya hayo, athari za ubabedume katika jinsia ilimulikwa. Ilibainishwa kuwa Ben Mtobwa alifaulu kuangazia sura mbalimbali za ubabedume katika jamii. Pia aliweza kuangazia athari za ubabe dume kwa jinsia zote mbili. Ben Mtobwa kutokana na utafiti huu alifanikiwa kusawiri ubabedume miongoni mwa wahusika kwa kina.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Kwa mujibu wa utafiti huu, imebainika kuwa makisio yote ya kitambo tuliyoyaorodhesha na maswali ya utafiti tuliyokusudia kuyajibu yamethibitishwa. Tasnifu hii ambayo ndiyo ya matokeo ya utafiti tuliyofanya imedhihirisha kuwa dhana

ya ubabe dume ilijitokeza katika riwaya hizi teule za Ben Mtobwa. Fauka ya hayo, sura mbalimbali za ubabedume na athari za ubabedume kwa jinsia zote mbili zilisawiriwa.

Mintaarafu ya madhumuni ya kwanza iliyohakiki sura mbalimbali za ubabe dume katika riwaya teule za Ben Mtobwa, imebainika kuwa vipengele hivi vinajitokeza. Katika kutathmini sura za ubabedume ni wazi kuwa riwaya za *Dar-es-salaam Usiku* na *Pesa Zako Zinanuka* zilidhihirisha haya kwa kina. Katika riwaya ya *Dar-es-salaam Usiku*, mhusika Peter alisawiriwa katika maumbo mbalimbali ya ubabedume. Pia wahusika kama Hasira na Hasara walisawiriwa kuwa na ubabedume katika jamii. Pia katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* wahusika kama Kandili Maulana na Bon Kolo walionyesha sura za ubabedume kama vile sura ya kitamaduni, kiuchumi, kimaumbile na kisaikolojia.

Kwa mujibu wa madhumuni ya pili yaliyohusu athari za ubabedume kwa jinsia, ilibainika bayana kuwa ubabedume ulikata kuwili kwani uliathiri jinsia zote mbili mathalani ya kiume na kike. Athari hizi ni kama vile utabaka wa kijinsia, dhuluma za kijinsia, ubaguzi wa kijinsia na ukahaba. Katika riwaya ya *Dar-es-salaam Usiku* mhusika kama Peter anaathiriwa na ubabedume kwa njia hasi. Hili linatokana na kujihusisha kimapenzi na wanawake wengi mtaani na kumtelekeza mkewe, Mama Sonny. Mama Sonny anaathirika kimawazo na hata kuugua. Fauka ya hayo, anakonda kama sindano. Naye Peter anakosa mwelekeo wa kimaisha kwani anayumbayumba sana kwa kuponda raha na vimanda kama Rukia. Kwa upande ule mwingine wahusika kama vile Rukia wanabaki kufungwa katika minyororo ya ubabedume na kutumbukia katika lindi la utegemezi na ukahaba.

Katika riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka* wahusika kama Dora wanatumbukia katika lindi la unyonge kwani wanategemea wahusika kama Kandili Maulana wasiowajali. Mhusika kama Kandili anatelekeza Dora licha ya uwepo wa uhusiano wao wa kimapenzi. Wahusika kama Maua wanageuka na kuwa makahaba wanaotegemea wanaume ili kujikimu kimaisha. Kutokana na haya ni bayana kuwa ubabedume unaathiri jinsia zote mbili na pia ubabedume una sura tofauti maishani. Kwa kweli malengo mawili yaliyolengwa kuafikiwa katika huu yalichanganuliwa na matokeo kuthibitishwa.

## 5.4 Hitimisho

Uchanganuzi uliofanywa ulidhihirisha kuwa suala la ubabedume linajitokeza miongoni mwa wahusika katika riwaya teule za Mtobwa. Fauka ya hayo, sura mbalimbali za ubabedume zinajitokeza kwa mujibu wa madhumuni ya kwanza. Baadhi ya sura hizo ni kama vile sura ya kitamaduni, kijamii, kisaikolojia, kimaumbile, kiuchumi na dhakari. Kwa kifupi kwa mujibu wa madhumuni ya kwanza, matokeo ya utafiti yalisawiri sura mbalimbali za ubabe dume miongoni mwa wahusika teule katika riwaya lengwa za Ben Mtobwa. Hata hivyo, ilibainika kuwa wahusika wote walioendeleza ubabe dume ni wale wa kiume.

Katika kujaribu kukabiliana na hali hii wahusika kama Rukia na Nunu katika *Dar-es-salaam Usiku* walijaribu kukata minyororo ya ubabedume. Pia Dora na Maua katika *Pesa Zako Zinanuka* walijaribu kujikomboa kutoka na dhiki za dhuluma za jinsia ya kiume. Hata hivyo, wahusika kama Peterson katika *Dar-es-salaam Usiku* waliendeleza ubabedume na kufanya ukite mizizi. Ngome hii ya ubabedume ilifanya wahusika wa kike kujaribu kujikomboa kupitia itikadi za kifeministi. Mathalani, Rukia katika *Dar-es-salaam Usiku* alijaribu kupingana na juhudi za wanaume kudhalilisha wanawake.

Vilevile kwa mujibu wa madhumuni ya pili, matokeo ya utafiti yalibaini kuwa mtunzi wa riwaya lengwa alisawiri athari za ubabedume kwa jinsia. Athari hizi mara nyingi zilikuwa hasi. Athari za ubabedume kwa jinsia zilikuwa kama vile ubaguzi wa kijinsia, utabaka wa kijinsia, utepetevu, ukahaba,utapeli na anasa. Athari hizi ziliathiri wahusika kama Rukia na Nunu katika riwaya za *Dar-es-salaam Usiku* na pia Hasara, Dora na Maua katika *Pesa Zako Zinanuka.* Matokeo ya utafiti huu yaliweza kutoa majibu sahihi kwa maswali ya utafiti.

Kwanza utafiti ulithibitisha kuwa kulikuwepo sura mbalimbali za ubabedume katika riwaya za Ben Mtobwa. Matokeo yalidhihirisha kwamba riwaya zote mbili wahusika waliendeleza ubabedume mathalani ya kitamaduni, kijamii, kiuchumi, kimaumbile, kisaikolojia na kidhakari. Pia matokeo ya utafiti yalibaini kuwa mwandishi Ben Mtobwa alionyesha athari hasi na chanya za ubabedume katika riwaya zake mbili. Hatimaye mtafiti aligundua kuwa Ben Mtobwa alifaulu kutimiza dhamira yake ya kuonyesha sura za ubabe dume katika asasi za kijamii na athari zake kwa wahusika.

## 5.5 Mapendekezo

Riwaya za Ben Mtobwa hazijatafitiwa kwa kina kama ilivyo katika riwaya za waandishi chipukizi. Utafiti huu ulijikita tu katika sura mbalimbali za ubabedume miongoni mwa wahusika teule na athari za ubabedume kwa jinsia. Kuna hazina kubwa ya kufanyiwa utafiti katika kazi za mwandishi huyu. Mathalani, suala la vijenzi vya ubabe dume ambapo mtafiti anaweza kuangazia nafasi ya wanaume katika ukombozi wa jamii ya ubabedume. Pia watafiti wa siku za usoni wanaweza kutafiti kuhusu athari za ubabedume katika kazi za wandishi chipukizi kwa kutumia nadharia ya maadili.

Fauka ya hayo, watafiti wa baadaye wanaweza kufanya utafiti kuhusu wahusika wanaume wasio na ubabe dume katika kazi za fasihi kwa kutumia nadharia ya Udenguzi na Uhalisia. Pia mtafiti anapendekeza waandishi wa kazi za fasihi waandike kazi zao ambazo zinasawiri usawa wa kijinsia baada ya migogoro dhidi ya ubabedume. Mtafiti anapendekeza kazi za fasihi zikiwemo riwaya zimulike uhalisia wa hali ilivyo katika jamii hasa kuhusu suala la umenke. Pia mapendekezo ya utafiti wetu ni wandishi wa kizazi kipya wajaribu kuandika kazi za fasihi kuhusu ubabedume na suluhisho la hali hii. Mtafiti vilevile anapendekeza wanajamii wamulike kuhusu nafasi ya mwanamume katika jamii. Utafiti wetu ulibaini wanaume wengi walikabiliwa na changamoto licha ya kuwa walikuwa na nguvu za ubabedume.

Mtafiti vilevile anapendekeza pawepo na mafunzo katika taasisi za elimu ili kuhamasisha wanajamii kuhusu dhana ya ubabedume na athari zake kwa wanajamii. Mafunzo haya yanaweza kufunzwa kutoka nyumbani hadi vyuoni. Mtafiti hatimaye anapendekeza kuwa wandishi wa kazi za fasihi wajaribu kuzingatia mabadiliko na kuwepo kwa usasa katika jamii mpya. Ni ukweli kuwa licha ya kuwa wanaume wamepewa nguvu na asasi za kijamii bado wako katika lindi la dhiki.

Vilevile wahusika wa kiume katika kazi nyingi za fasihi ikiwepo riwaya za Ben Mtobwa, wanasawiriwa kwa njia hasi. Hali hii inafaa kuepukwa kwa sababu ya ujenzi wa jamii mpya. Wahusika wa kike nao wanasawiriwa wakiwa na hulka mbaya hivyo inaleta picha bovu kwa wanagenzi. Hivyo basi, dhima ya fasihi ya kuwa kioo cha jamii pamoja na kufunza, kutahadharisha, kuzindua, kuleta maadili katika jamii na kutatua changamoto katika jamii itaafikiwa kwa ustadi mkubwa.

## MAREJELEO

Abudi, M. (2011). *Language, Gender and Power Relations*. MA thesis Egerton University

Ali, B. H. (2018) *Wahusika wa kimimi katika Riwaya za Kiswahili: Mifano kutoka Dunia yao Nyuso za mwanamke* Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania.

Anderson, K. J. & Accomando, C. (2002). *Real Boys? Manufacturing Masculinity and Erasing Privilege in Popular books on Raising boys. Feminism & Psychology* Vol. 12 Pg. 491-516

Baynon, J. (2002). *Masculinities and culture*. Buckingham: Open University Press.

Buliba, A., Gwachi, M. & Matinde, R (2014) *Misingi ya Nadharia na mbinu za utafiti.* Serengeti Educational Publishers, Tanzania.

Choti, J. N. (1998). *Language and hierachy, The linguistic portrayal of Gusii woman* (M.A Thesis) Kenyatta University, Kenya.

Connell, R. (1995). *Masculinities*. Cambridge: UK, Polity press.

Connell, R. (2005). *Hegemonic masculinity: Rethinking the concept.Gender and Society 19.*

David, D. S. & Brannon, R. (Eds) (1976). *The Forty-Nine Percenty Majority: The Male Sex Role.* New York: Random House

De Franzo, E. S. (2011). *What's the difference between Qualitative and quantitative research?* Snap Surveys

Donaldson, M. (1993). *What is hegemonic masculinity*? UOW: Australia

Eckert, P. & Mc Connell-Ginnet (2003). *Language and gender*. Cambridge: Cambridge University Press.

Edell, D. (2015). *Girls Uninterrupted*: *Using Interactive Voice Diaries as a New Girls' Research Method.* London Routledge Studies

Edell, D. (2015). *Girls Uninterrupted: Using interactive Voice Diaries as a New Girls Studies Research Method*. University of New York: Sunny Press

Frosh, S. Phoenix, A. & Pattman, R. (2002) *Young Masculinities*. Newyork: Palgrave

Gitu, P. M. (2016). *Discursive construction of masculinities in Gikuyu proverbs* (M.A Thesis). Laikipia Univesity, Kenya.

Gitu, P. M. (2024). *Linguistic Stigmatisation in Discourses Towards Involuntary Childless Women in the Gikuyu Community*. (Tasnifu ya PhD) Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya

Greer, G. (2000). *The whole women*. London: Anchor.

Habib, R. (2008). *A history of literary criticism.*Malden, Mass*:* Blackwell publishing. https://doi.org10.1177/1060

Haji (2018). *Uhalisia wa Utabaka katika Tamthilia ya Janga la Werevu na Kitumbua Kimeingia Mchanga*, Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Harwood, V. (2000). *Truth, Power and the Self: A Foucaultian Analysis of the truth of Conduct Disorder and the Construction of Young People's Mentally disordered Subjectivity*. PHD Thesis University of Australia

Holter, G. (2005). *Social Themes for researching Men and Masculinities: Direct Gender hierarchy and Structural Inequality*. University of Oslo

Izugbara, C. (2005) *Hypothesis on the Origin of Hegemonic Masculinity in Sexuality in African Magazine*. Lagos: Africa Regional Sexuality Resource Centre 2(1): 13-14

Kamau, P. (2023). *Wanawake na Mikakati ya Ukombozi katika Tamthilia za Kigogo na Chema Chajiuza*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya

Katola, E. (2006). *Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili*. (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya

Khaemba, J.M. (2013). *The discursive construction of hegemonic masculinities in selected rituals of the Bukusu of Kenya (*PHD thesis). Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Kibigo, M. L., Choge, C. C. & Wanjala,F. S. (2019). *Tamathali za semi zinazosawiri ubabedume katika majigambo ya miviga ya shilembe na mchezasili wa mayo ya Waisukha nchini Kenya kwa mtazamo wa semantiki.*East African Journal of Swahili Studies.4.

Kimani, C.W. (2003). *Suala la dhuluma ya wanawake katika fasihi ya Kiswahili* (Tasnifu ya M.A.). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Kimmel, M. S. (1997). *Masculinity as homophobia fear, Shame and Silence in the Construction of Gender Identity* ***Routledge***

Kimondiu, D. K. (2019). *Usawiri wa mwanamke katika nyimbo za sifo za Wakamba (*Tasnifu ya M.A.). Chuo Kikuu cha Machakos, Kenya.

Knights, B. (1999). *Writing Masculinities: Male Narratives in Twentieth Century fiction.* London Palgrave Macmillan

Kothari, C. R. (2008). *Research methodology: Methods and techniques*. New Delhi: New age international publishing Ltd.

Kweyu, D. (2007). *A Critical Analysis of Pariarchy and Masculinity in Kezilahabi's Rosa Mistika and Kichwa Maji.* MA Thesis University of Nairobi

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Dar-es-Salaam: Mture education publishers.

Makini G. (2015). *Udhihirikaji wa Kanuni ya Dahl katika Lugha ya Ekegusii*, Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Makini, G. (2015). *Udhihirikaji Wa Kanuni ya Dahl Katika lugha ya Ekegusii.* Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta

Malenya, M. (2022). *Uchanganuzi matini Kifeministi wa mwanamke wa kisasa katika nyimbo teule za Taarab*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Likipia.

Malonya, M. (2022). *Uchanganuzi wa Matini Kifeministi Wa Nyimbo Teule za Kisasa Katika Taarab*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu Cha Laikipia

Mboya, P. & Mohochi, S. (2018*).Dhuluma kama kichocheo cha mzinduko wa wanawake katika riwaya za Kiswahili*. International journal of social sciences and information technology. Vol 4 (II)

Mirikau, S. (2011). *Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Wamitila* ( Tasnifu ya M.A).Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

Morettini, F. (2016). *Hegemonic Masculinity: How Dominant Man Subjugates Other Men, Women and Society*. Global Policy Journal. www.globalpolicyjournal.com blog/2016

Mtobwa, R. B. (2005). *Dar-es-Salaam Usiku*. Dar-es-Salaam Mkuki publishers.

Mtobwa, R. B. (2015). *Pesa Zako Zinanuka*. Dar-es-Salaam Mkuki publishers.

Muchenje, J., Wandera, S., & Onyango, J. (2018). *Hegemonic Masculinity in Song Lyrics of Webuye Jua Kali Band*, Kenya. Journal of Research Innovation and Implications in Education, 2(4), 18-22.

Muleka, J. (2016). *Gendered Memory in Oral Narratives and Socialization of the girl child in the African society*. International Journal of humanities and social science invention. www.Ijhssi.org

Mulila, J (2009). *Usawiri chanya wa wahusika wanawake katika Tamthilia za Zilizala na Chamchela* (Tasnifu ya M.A.). Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

Mwikali, R. K. (2014).*Uchanganuzi wa uhusiano wa jinsia katika vipengele vya tamthilia za Kilio cha Haki na Sudana(*Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Nabangi, J. (2017). *Athari ya Uteuzi katika Uandishi wa Riwaya Teule ya Kiswahili*, Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ngumo, C. (2014). *Discursive construction of masculine identities in newspaper pull out magazines in Kenya* (PHD Thesis). Laikipia University, Kenya.

Njogu, S. K. & Chimera, R. (1999).*Ufundishaji wa fasihi : Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkumbo, D. Onyango, J. O. & Mayaka, G. J. (2018). *Usawiri wa jinsia katika lugha mwiko* na *ya tafsida miongoni mwa jamii ya Ameru*. *Coretrain journal of languages, humanities, social sciences and education.* Laikipia University*, 1, 119-130.*

Omar A. (2014). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Kuli na Vuta N'kuvute*. Tasnifu ya Uzamifu ya Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Ondoro, J. (2021) *Maudhui ya siasa na Athari zake katika jamii: Mifano kutoka Diwani ya Kaza Macho* Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

Onyango, J. (2015). *Discursive Masculinities and the War against AIDS. The Kenyan Experience* . Division of Research and Extension Egerton University

Onyango, J. O. (2007). *Masculinities in Kiswahili children literature in Kenya*. Swahili forum 14: 245-254.

Onyango, J. O. (2015). *Discursive masculinities and the war against AIDS*: *The Kenyan experience*. Division of research and extension, Egerton University.

Onyoni, J. (2012). Usawiri *wa wahusika wa kike katika tamthilia za Natala na Mama Ee* (Tasnifu ya M.A.). Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya.

Oyeronke, O.(ed). (2011). *Gender Epistemologies in Africa. Gendering Traditions*, *Spaces, Social institutions and Identities*: Newyork: Palgrave Macmillan.

Oyewumi, O. (1997). *The Invention of Women: Making an African Sense of Western Gender Discourses*. Minneapolis : University of Minnesota Press

Richmond, M. (1992). *Masculine and Feminine: Gender Roles over the Life Cycle* Pennsylvania State University.

Riro, M. S. (2006). *Usawiri wa mwanamume katika nyiso za Abakuria* (Tasnifu ya M.A). Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

Riro, M. S. (2015). *Uchanganuzi wa ubabe-dume katika majigambo (Amaibako) ya Abakuria (*Tasnifu ya uzamifu). Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya.

Senkoro, F. (1987). *Fasihi wakati wa Ubepari*. Dar-es-Salaam: Press & Re Publicity Press

Uchendu, E. (2007). *Masculinity and Nigeria youths.* Nordic journal of African studies, 16 (2), 279-297.

Uchendu, E. (2008). *Are African males men? Sketching African masculinities: Masculinities in contemporary Africa.CODESRIA.*

UNESCO (2013). *Hegemonic masculinity in media content.* Paris: Kareithi,P.J.

Waiganjo, J. (2014). *Uchambuzi wa upeketevu wa wanawake katika riwaya teule za Said A. Mohammed* (Tasnifu ya M.A). Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi, misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*.Nairobi focus publications.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi*. Nairobi: Focus publication Ltd.

Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi :Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi Phoenix Publishers

Wandera, S. (2015). *Taswira za Kimenke katika Hadithi za Abanyala (Mumbo) Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo kikuu cha Laikipia.

Wellek, R. & Warren, A. (1973). *Theories of literature*. England: Penguin Books.

Wells-Wilbon, R. & Haland, S. (2001). *Social Learning Theory and the Influence of Male Role Models on African American Children in Project 2000.* The *Qualitative Report*, 6(4) https://doi.org/10.46743/2160-3715/2001.1994

Wilson, A. (2000***).*** *Patriarchy in feminist theory*. Routledge International Encyclopedia of Women: Global Women's Issues and Knowledge Vol. 3, P. 1493-1497

Yego, E. (2013). *Nafasi ya Mwanamke: Jinsi inavyotetewa Katika Nyimbo za Taarab za Zanzibar*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi

Zaharia, M. (2018). *Taathira za Ubabedume kwa mwanamume mwenza wa Kizanzibari kupitia Nyimbo za Taarab Asilia* (Tasnifu ya M.A). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Barua ya Chuo

LAIKIPIA UNIVERSITY

P.O. Box 1100-20300,
NYAHURURU,
KENYA

TEL: +254-(0) 20 2671779, 20-2671771;
Cell: +254 0729285902, 0729281902
bpgs@laikipia.ac.ke; www.laikipia.ac.ke

**OFFICE OF THE DIRECTOR**
**GRADUATE SCHOOL**

**Ref: MK22/2520/18/7**
17th March 2021

TO WHOM IT MAY CONCERN

**RE: WANJOHI SIMON NGURE - MK22/2520/18/7**

The above named student is a Postgraduate student at Laikipia University undertaking a Master of Arts degree in Kiswahili and Communication in the School of Humanities and Development Studies.

His research proposal entitled "**UCHANGANUZI WA WAHUSIKA TEULE KWA MISINGI YA KIBABE DUME KATIKA RIWAYA ZA BEN MTOBWA**" was **examined and approved** by the Board of Graduate School.

He is hereby authorized to conduct his research.

Any assistance accorded to him is highly appreciated.

Thank you.

**S. Muchendu**
**For DIRECTOR**

*Vision: A University for Valued Transformation of Society*
*Mission: To serve students and society through research, education, scholarship, training, innovation, outreach and consultancy*
Laikipia University is Certified to ISO 9001:2015 and ISO/IEC 27001:2013

## Kiambatisho II: Barua ya Idhini Kutoka NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NACOSTI

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION**

Ref No: 336249

Date of Issue: 20/April/2021

### RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Mr.. Simon Ngure Wanjohi of Laikipia University, has been licensed to conduct research in Nyandarua on the topic: UCHANGANUZI WA WAHUSIKA TEULE KWA MISINGI YA KIBABE DUME KATIKA RIWAYA ZA BEN MTOBWA for the period ending : 20/April/2022.**

License No: NACOSTI/P/21/9877

336249

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

National Commission for Science, Technology and Innovation